Kikao cha Sita – Tarehe 04 Oktoba, 2017

Kikao kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mwanzoni mwa Mkutano huu, Mhe. Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Afya na Mhe. Naibu Waziri wa Afya aliahidi kujibu kwa maandishi. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 40(4) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, namuomba Waziri wa Afya asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo. Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue nafasi hii kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nikijibu swali Namba 41, Mhe. Shaib Said Ali aliuliza swali la nyongeza, ambapo alitaka kujua kwa nini vifaa vya *X-Ray* viliopo katika hospitali ya Micheweni vinaharibika bila kufungwa, na ametaka kujua lini jengo litamalizika ili vifaa hivyo vifungwe.

Jibu la swali hilo ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ufafanuzi wa maelezo hayo ni kwamba, wizara imefanya ujenzi wa jengo litalotumika kwa huduma za "*theatre*" kwa ajili ya kinamama katika hospitali ya Micheweni. Kwa vile, matengenezo yalikuwa hayajakamilika, vifaa kwa ajili ya "*theatre*" hiyo havifungwa. Hivyo, vifaa walivyovikuta Waheshimiwa Wajumbe ni vifaa vya "*theatre*" na siyo vya *X-Ray* kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi. Ahsante Mhe. Spika.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya hotuba ya uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano, naomba kuweka hati mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Ripoti ya Utekelezaji

kwa Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Salum Haji (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuweka hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2016/2017 kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 100

Umuhimu wa Kuenzi Majengo ya Viongozi wa Nchi

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Zanzibar ni muhimu kuwa na nyumba ya kumbukumbu ya Rais wetu wa kwanza Mhe. Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na viongozi waliomfuatia baadaye.

Kwa kuwa, wananchi wetu pamoja na vizazi vyetu wanahitaji kumbukumbu ya viongozi wao. Je, ni lini serikali itaamua ujenzi wa jengo hilo la kumbukumbu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi yetu inahitaji kuwa na Kituo cha Kumbukumbu za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo. Kwa sasa kumbukumbu hizi zinatunzwa kupitia vyombo na taasisi mbali mbali pamoja na mtu mmoja mmoja. Hivyo, ili kuzikusanya kumbukumbu hizi kunahitaji kuwepo na miongozo ya kisheria na maridhiano ili kufanikisha jukumu hili.

Mhe. Spika, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hivi sasa imo katika hatua za kurekebisha Sheria Nam.10 ya mwaka 2002 ya Kuwaenzi Viongozi. Kupitia Sheria hii, wajibu na utaratibu wa kuweka kumbukumbu za Viongozi wetu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utawekwa wazi. Ni matumaini yangu kuwa sheria hii itakamilika katika mwaka huu wa fedha. Hivyo basi, kazi ya utunzaji wa kumbukumbu za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa itaanza kutekelezwa mara tu baada ya kupitishwa kwa sheria hii. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze wizara kwa kuliona suala hili linafaa hasa tukizingatia pia tumepitwa na wakati, lakini pia nitoe pongezi za pekee kwa kumbukumbu za Mhe. Rais wetu wa kwanza na viongozi wetu wengine kwamba vyombo vya habari au Maktaba zetu za habari zinatoa hotuba za viongozi hawa na wananchi wetu huelewa mambo mengi yaliyopita.

Je, kwa kuzingatia muda na tumeambiwa kwamba mwaka huu wa fedha mpango huu huenda ukafanyika, ni wapi huko kutakojengwa jumba hilo la Makumbusho, ili wananchi wajue.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tunategemea kukamilisha jambo hili la kisheria. Katika jambo hili serikali kupitia Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais tutatizama sehemu ambayo itakuwa nzuri kwa ajili ya kuweka kumbukumbu hizi kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye. Kwa hiyo, wapi kwa sasa tunatumainia baadaye tutakuja tutaelekezena na serikali itakuja kutoa muongozo katika jambo hili. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza kama hivi ifuatavyo.

Je ni lini sheria hii inategemewa kuletwa Barazani, ili kuweza kuzitunza kumbukumbu za viongozi wetu wapendwa wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, ndani ya jibu langu la msingi narudia tena kwa sasa serikali ipo katika hatua za mwisho za kufanyia marekebisho Sheria Nam.10 ya 2012. Kwa kweli, nilichokisema ndani ya jibu langu la msingi kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tunategemea sheria hii itakuwa tumeshamaliza kuifanyia marekebisho, na itakapofika wakati tutaeleza katika Baraza hili, na Waheshimiwa Wajumbe wapo watapata fursa ya kutoa baadhi ya ushauri pamoja na michango yao, ili kuifanyia maboresho zaidi. Kwa hiyo, Mhe. Spika nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tunategemea kulikamilisha hilo na jambo hili litakuja Barazani. Nakushukuru.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, suala hili limekuwa ni la muda mrefu sana na hata wale waasisi wake wengine wa wazo hili wameshatangulia mbele za haki wakiwemo kina Mrembo na tangu ya Ofisi ya Waziri Kiongozi. Je, ni lini hasa serikali itajenga jengo hili na nina hakika kwamba tulikuwa tumeamua tujenge Mwere Kiongoni, lini litajengwa jengo hili kwa kuwaenzi viongozi wetu hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake moja la nyongeza. Mhe. Spika, swali la Mhe. Mwakilishi linalingana sana kabisa na lile ambalo aliliuliza Mhe. Ali Suleiman Ali. Sasa lazima tukubaliane tunachokifanya sasa kwanza ni kukamilisha utaratibu wa kisheria, tutakapokamilisha utaratibu wa kisheria tutakwenda sasa katika maeneo stahiki ambayo yatakuwa mazuri kwa jambo ambalo tunategemea kulifanya. Sasa wapi *location* itakuwa tunatumaini serikali inayajua maeneo yote, inayajua majengo yote, inajua sehemu zote ambazo zitastahiki kuwekwa kwa kumbukumbu hizi. Itakapofika wakati tutaambizana tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wavute subra katika hili. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Machano Othman Said kwa kuwa yeye ni Waziri Mstaafu katika Ofisi ya Waziri Kiongozi anaijua vizuri *process* ya jambo hili. Kwa kweli, huko nyuma mazungumzo yalikuwa tukizungumzia kuhusu Kiungoni Mwera kuwa ndio lijengwe jengo hili, kwa sababu ilikuwa ndio asili ya Mzee wetu Abeid Amani Karume pale. Kwa hiyo, bado fikra hizi zimo kichwani kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri pale ambapo tutafikia maamuzi ya mwisho kuhusu fikra ambazo zimeanzishwa tutaendelea kuziheshimu. Inaonekana ni wazi kwamba mawazo yatakuwa sana hapa Kiungoni kwa sababu ya uasili wake na kwa sababu sote tunajua jitihada za Mzee wetu Abeid Amani Karume katika kuiokomboa nchi hii, kwa hivyo kila kinachomuhusu yeye inakuwa ni kumbukumbu ya maendeleo yetu kwa pamoja.

Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi tuvute subra tumalize utaratibu wa sheria kama ambavyo Mhe. Naibu Waziri amesema najua umeanza utaratibu huu wa sheria sasa tunakamilisha vizuri, baada ya kukamilika vizuri basi yote haya yatafanywa kama ambavyo ilivyokusidiwa na serikali. Ahsante sana.

Nam. 29

Ukodishaji wa Sehemu za Kutangaza Biashara

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hutenga sehemu za kutangaza biashara kwa wafanyabiashara na sehemu hizo huwa zinakodishwa. Lakini katika miji yetu, eneo hilo halijawekwa vizuri kibiashara na kutofahamika vizuri kwa wananchi.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa ukodishwaji wa maeneo hayo.

(b) Je, kuna elimu gani iliyotolewa ya kulitangaza eneo hilo.

(c) Hatuoni umuhimu wa kutoa bei za wazi kwa matangazo ya maeneo hayo ili kuwa rahisi kwa mfanyabiashara kuelewa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, utaratibu unaotumika hivi sasa katika suala la ukodishwaji wa matangazo ya biashara kwa wananchi na wafanyabiashara kuwasilisha maombi yao katika Mamlaka za

Serikali za Mitaa ambapo baada ya mamlaka husika kujiridhisha, waombaji hupewa maelekezo kuhusu uwekaji wa matangazo hayo kulingana na masharti na mahitaji ya mipango miji.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa maeneo kama hayo ni machache, bado hakujawa na haja na ulazima wa kutoa elimu na kuyatangaza maeneo hayo.

(c) Mhe. Spika, ofisi inakubaliana na ushauri uliotolewa na Mhe. Mwakilishi kuhusu umuhimu wa kutoa bei kwa uwazi kwa matangazo ya maeneo hayo ili kuwa rahisi kwa mfanyabiashara kupata uelewa. Tunaahidi kuufanyia kazi ushauri huo kwa kushirikiana na taasisi nyengine kwa kadiri maeneo hayo yatakavyopatikana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana kwa majibu yake mazuri Mhe. Waziri lakini nina swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Je, serikali haioni umuhimu wa kuyatayarisha au kuyajenga maeneo hayo kwa ajili ya wafanyabiashara ambao kwa sasa hivi wanayahitaji maeneo hayo, ili na serikali ipate mapato.

b) Je, serikali haioni kuwa umefika wakati kwa kujipanga na kuweza kuupamba mji kwa matangazo wakati serikali inahitaji mapato na wafanyabiashara wanahitaji kutangaza matangazo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba jambo hili hutegemea na mipango miji ilivyo. Kwa hiyo, hatuoni haja ya kupanga eneo maalum kwa ajili ya shughuli hizi kwa sababu shughuli hizi huwa zinafanyika na wafanyabiashara kwa mahitaji yao. Na pale ambapo tutapaona kwamba panafaa kwa ajili ya kuweka matangazo hayo basi ndipo sisi tunapotoa ruhusa.

b) Mhe. Spika, tunatambua kwamba upo umuhimu wa kuweza kuweka mkazo na ndio maana jambo hili sasa limewekewa utaratibu maalum kwa mujibu wa kanuni za matangazo na bei na kila kitu kwa sababu suala hili ni sehemu ya kuingiza mapato ya Halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar.

Nam. 61

Ubovu wa Barabara

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Wananchi wa Jimbo la Chumbuni waliopo katika Manispaa ya Mjini, kwa muda mrefu barabara yao kutokea kiwanda cha maziwa eneo la Maruhubi hadi kituo cha Afya cha Chumbuni ni mbovu na huleta kero hasa kwa kinamama wajawazito na wananchi wengine.

(a) Serikali ina mpango gani kupitia Manispaa ya Zanzibar kuitengeneza barabara hiyo.

(b) Ni hatua gani za dharura zitachukuliwa katika kukabiliana na ubovu wa barabara hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikao, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vipengele (a) na (b) na kabla ya kumjibu swali hilo naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Barabara ya Kiwanda cha Maziwa Maruhubi hadi Kituo cha Afya – Chumbuni yenye urefu wa kilomita moja ni barabara ya ndani (*feeder road*) inayopaswa kuhudumiwa na Ofisi ya Rais, Tawala ya Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria Nam. 7/2014. Naomba nikiri kuwa barabara hiyo ni kiungo kizuri kati ya Barabara ya Maruhubi na Barabara ya Mkapa na kufanyiwa matengenezo katika kiwango cha lami. Hatua hiyo, itasaidia pia kuondoa usumbufu hasa kwa akinamama wanaofuata huduma za afya katika Kituo cha Afya cha Chumbuni.

Mhe. Spika, baada ya maelelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa barabara hiyo kijamii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ haijapanga kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa muda huu, kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 tayari zimeshapangwa kutumika katika matengenezo ya barabara nyengine.

(b) Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa – Mjini na viongozi wa Jimbo la Chumbuni, itaangalia hatua za dharura zinazoweza kuchukuliwa katika kukabiliana na ubovu wa barabara hiyo muhimu ikiwemo hatua ya kuifanyia matengenezo katika eneo korofi, ili iweze kupitika na kuwapunguzia wananchi adha iliyopo hivi sasa.

Mhe. Saada Ramadhan Mwenda: Mhe. Spika, ahsante namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya kuvunja moyo kwa sisi wanawake wa Chumbuni. Lakini nataka kuuliza kwamba, hayo mashirikiano ya Manispaa pamoja na Waheshimiwa wa Jimbo la Chumbuni ni lini angalau tutawekewa hicho kifusi wanawake wapate wapungue mateso ya kuzaa njiani bila ya kufika hospitali. Mhe. Spika, naomba tarehe. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikao, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwenda swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza napokea pongezi kwa jibu ambalo nimelitoa, lakini kama

nilivyosema katika jibu mama kwa sababu barabara hii haimo katika ule mpango makhsusi wa ujenzi wa *feeder road* na barabara zinazoshughulikiwa na Serikali za Mitaa. Kwa hivyo, nilichosema ni kwamba Baraza la Manispaa kupitia makusanyo yake tutashirikiana na uongozi wa Jimbo la Chumbuni akiwemo Mbunge, Mwakilishi na Madiwani na hata yeye Mhe. Saada Ramadhan Mwenda kwa sababu ni mkaazi wa jimbo hilo, basi tutahakikisha tunakaa nao tunazungumza nao ili kwa muda mfupi tuone uwezekano wa kuweza kuzifanyia marekebisho zile sehemu korofi ili tuweze kuwapunguzia wananchi matatizo yao. Ahsante sana.

Nam. 62

Operesheni za *ZRB* Barabarani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mnamo tarehe 18/7/2017 watendaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) walikaa eneo la Jozani na kukamata gari zinazopita hapo huku nyengine wakizifungua nambari.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea *ZRB* wafanye operesheni kama hizo.

(b) Sheria za Mapato zinasemaje kuhusu wajibu wa *ZRB* kuhusiana na operesheni kama hizo

(c) Kwa nini gari zinazobeba watalii zinasimamishwa wakati zikiwa na wageni ambao hupotezewa muda wao na watendaji wa *ZRB* na kuleta taswira mbaya kwa wageni hao hasa katika soko la utalii.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kujibu swali Nam. 62 la Mhe. Jaku Hashim Ayoub lenye vipengele (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, *ZRB* inafanya operesheni mbali mbali ikiwemo za kukagua magari yasiyolipiwa kodi kwa lengo la kubaini waliokwepa kodi, lakini pia kwa lengo la kugomboa kodi hiyo na tatu kusimamia vyema sheria za kodi nchini.

(b) Mhe. Spika, Sheria za Mapato zinatoa jukumu kwa *ZRB* kusimamia Sheria zote za Kodi iliyokasimiwa kuzisimamia. Usimamizi huo unahusisha kuwatambua walipakodi, kuhakikisha kuwa kodi yote inalipwa kwa wakati, kubaini wasiolipa kodi, na kuchukua hatua za kiutawala za kisheria kugomboa kodi ya serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa kipindi cha Mwezi Aprili hadi Agosti, 2017, Bodi ya Mapato imefanya mazoezi 3 ambayo yamepelekea kugomboa jumla ya shilingi 42,484,000.00.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza, lengo la *ZRB* sio kuleta taswira mbaya na usumbufu kwa wageni, bali ni kuhakikisha kuwa kila anaepaswa kulipa kodi anatimiza wajibu wake huo wa kisheria. Kwa mlipa kodi ambaye analipa kodi zake kwa wakati, zoezi hilo halimletei usumbufu wowote. Hivyo, naomba kutumia fursa hii kwa mara nyengine tena kuwasisitiza walipakodi wote nchini watimize wajibu wao huo wa kisheria

kwa taifa letu kwa kulipa kodi zao kwa ukamilifu na kwa wakati. Tunaendelea kuwaomba viongozi wote, ikiwemo sisi Waheshimiwa Wawakilishi kama kawaida yetu kuendelea kuungana mkono serikali katika kuhakikisha kila kodi inakusanywa ipasavyo. Wakwepa kodi wasipewe nafasi ya kutetewa bali wachukuliwe kuwa ni wahujumu wa uchumi wetu na sote tuungane kuwaelimisha ili nao waondokane na mtizamo huo hasi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kumuulisa maswali madogo ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b).

(a) Je, *ZRB* wamepewa mamlaka kisheria kufungua *plate number* za magari na kama hivyo, gari imefunguliwa *plate number* huku ikitembea ikawa haina *plate number* na ikagonga mtu kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu ajalie isitokea si kesi nyengine tena hiyo. Pia kuna sheria au kifungu gani cha kulipa kodi kilichowapa kufungua *plate number* hizo ili wananchi wapate kujua.

(b) Kwa kuwa watalii ndio nguzo yetu kubwa na usumbufu wanaopata katika operesheni hizi inaleta taswira gani katika kutangaza Zanzibar. Lakini duniani kote wakusanyaji kodi huwa na maneno mazuri na maneno mazuri ni sadaka vile vile, lakini baadhi ya watendaji wa *ZRB* wamekuwa na usumbufu kwa wafanyabiashara duniani kote, kwa kukusanya kodi huwa marafiki wanafanya biashara. Je atatoa elimu gani kwa wafanyakazi wa *ZRB* kwa kutumia lugha zilizokuwa za kistaarabu.

Mhe. Waziri wa Afya na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongea lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Moja kwamba *ZRB* imepewa nguvu ya kisheria na sheria ya Usimamizi wa Kodi (*Tax Administration Act)* ya mwaka 2009. Ndani ya sheria hiyo *ZRB* umewekwa utaratibu wa kisheria wa *ZRB* kufanya ukaguzi, lakini vile vile kukamata na kusitisha shughuli za kibiashara kwa mtu yeyote ambaye amekwepa kulipa kodi. Kwa hivyo, hilo suala lipo kwa mujibu wa sheria (*Tax Administration Act*) nguvu hiyo ipo kwenye sheria hiyo. (*Makofi*)

Vile vile nakubaliana sana na Mhe. Jaku Hashim kwamba ni vyema kujenga urafiki na walipa kodi na ndio maana *ZRB* mara zote inatoa taaluma na kuwataka walipa kodi wote walipe kodi zao kwa hiari. Lakini ndani ya hao wakorofi ambao wanakwepa kulipa kodi ndio pale *ZRB* inapotakiwa kuchukua hatua za kisheria, ili kuhakikisha kwamba kodi ya serikali inalipwa. Tutaendelea kuwaelimisha walipa kodi wote na tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kuwaelimisha wananchi na walipa kodi wote ili walipe kodi zao kwa mujibu wa sheria na bila ya shuruti yoyote. Kwa kufanya hivyo, itatupunguzia pia gharama za ufuatiliaji wa kodi ya serikali, itakuwa fedha nyingi sana za kufuatilia kodi hizo pindi wananchi wote wakielimika na kuchukua hatua za kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za nchi zilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuulia swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na inaonesha mikakati mizuri kwa wizara hii.

Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri alisema operesheni hii iliokoa karibu shilingi 42 milioni, lakini mimi nilitaka kujua katika swali langu.

(a) Operesheni hii *ZRB* ilifanya wenyewe au waliingiza wakala.

(b) Katika sura zote mbili kama walifanya wenyewe au waliingiza wakala ni gharama gani zilitumika katika kufanikisha operesheni hii. Kwa sababu lazima chochote hiki kinakwenda na gharama mana isijekuwa tumeokoa lakini hatujui ile gharama iliyotumika katika kufanikisha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. *ZRB* wanapoendesha zoezi hili wanafanya wao wenyewe lakini wanashirikiana na Jeshi la Polisi, vile vile wanashirikiana na Kamisheni ya Utalii. Kwa hiyo, ni zoezi ambalo linafanyika na taasisi ambazo zinahusika katika masuala haya na linafanyika katika taratibu za kawaida kama kazi za kawaida ambapo wafanyakazi wa *ZRB* wanapangiwa kutekeleza majukumu yao. Hivyo, wanalipwa mishahara yao ndio gharama inayotumika katika zoezi hili, hakuna gharama ya ziada zaidi ya mafuta wanayotumia lakini vile vile na mishahara yao ambayo tayari wanalipwa kwa kila mwezi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa bado wapo wafanyabiashara ambao wanakwepa kulipa kodi. Je, ni lini *ZRB* itawatangaza wasiolipa kodi hadharani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Yussuf Hassan Iddi kama ifuatavyo. Ziko njia nyingi za kuhakikisha kwamba *ZRB* inazitumia kuhakikisha kodi ya serikali inalipwa na moja ya njia hizo ni hili zoezi ambalo wamekuwa wakiliendesha. Lakini pia njia nyengine ni kuwapiga faini wale ambao wanakutwa na makosa hayo na uko utaratibu ambao unatumika katika nchi mbali mbali ya kwamba hawa watu wasiolipa kodi mbali ya hatua hizo basi pia nao watangazwe hadharani, hatujafikia huko lakini ikibidi ni moja ya njia ambayo inaweza kupaswa kuchukuliwa, ikibili lakini kwa sasa hivi zaidi tunatumia kuwaelimisha, kutoa taaluma zaidi sio kufedheheshana na wengi wao pale wanapokutwa na hatia basi wanakubali na wanalipa kodi zao. Kwa hivyo, ikibidi kwmaba twende na hatua hiyo ya kuwatangaza hilo ni suala ambalo tunaweza tukalizingatia.

Nam. 65

Walimu Kufanya Biashara za Kukopesha Skuli

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mhe. Spika, ahsante sana na mimi hivi sasa niko tayari kusikiliza majibu ya swali Nam. 65 lakini kujibiwa naomba nifanye marekebisho yafuatayo. Baada ya Afisa wa Elimu ya Sekondari Msingi na Kati Afisa wa Walimu ya Sekondari kabla ya kujibiwa Mnamo tarehe 13/7/2017 kuna taarifa zimenukuliwa kutoka kwa Afisa wa Elimu Sekondari, Bi. naomba isomeke Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi na Kati. Baada ya maelezo hayo niko tayari kusikiliza majibu.

Safia Rijal kuwa kuna mtindo wa baadhi ya walimu wa skuli mbali mbali kujihusisha na biashara za kukopesha wanafunzi wakiwa skuli na majukumu ya kulipa mikopo hiyo yanawakabili wazazi wa wanafunzi hao.

(a) Je, Wizara ya Elimu imefanya uchunguzi kujua ukubwa wa tatizo hilo na athari zake.

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kwa walimu waliobainika kufanya vitendo hivyo na wizara inatoa kauli gani kwa walimu watakaobainika kuendelea na vitendo hivyo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Manaibu Mawaziri ambao mtakuwa mnakuja kujibu ambaye anafuata basi angekuwa anakaa kile kiti cha mbele, ili kuokoa muda kujiandaa kuja huku. Wizara inayofuata Naibu Waziri akae pale inakuwa rahisi zaidi kuliko kutokea huko nyuma.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 65 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo. Lakini pia Mhe. Spika, na mimi kwa ruhusa yako naomba kwanza nitoe marekebisho, kwamba Bi. Safia Ali Rijali si Mkurugenzi wa Maandalizi Msingi na Kati, bali ni Mkurugenzi wa Idara ya Elimu, Maandalizi na Msingi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Baada ya marekebisho hayo naomba kujibu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya ufuatiliaji na inaendelea kufanya hivyo ikiwa ni sehemu ya kazi za kila siku kwa lengo la kubaini tatizo hili na kuwasaidia wazazi na watoto wa skuli zinazojihusisha na ufanyaji wa biashara wanapokuwa kazini.

Mhe. Spika, wizara imebaini kwamba suala hili linaleta athari kubwa hasa katika uwajibikaji wa walimu katika majukumu yao ya kila siku. Pia, wizara kwa kupitia Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi imechukua hatua zifuatazo kwa skuli ambazo tumepokea malalamiko kutoka kwa wananchi, ikiwemo Skuli za Kijitoupele A na B, Chumbuni, Migombani, Mfenesini, Nyerere na Sebleni. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kupiga marufuku kwa walimu wote kufanya biashara wakati wa masomo, Walimu Wakuu wametakiwa kusimamia suala hili lisiendelee, kuzungumza na walimu wote wa skuli zilizohusika na kadhia hii na kuzungumza na wanafunzi katika kupata ukweli wa suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Wazri lakini shida mtu ndiyo inayomfanya mtu kuhangaika. Kwa kuwa, serikali imepiga marufuku biashara kufanyika skuli wakati biashara hizo zinaendelea.

a) Je, wiara imejipanga vipi kuangalia maslahi ya walimu kutokana na kazi kubwa wanayoifanya. Nilisema dhiki ndio inayomfanya mtu kuhangaika.

b) Kwa kuwa, walimu wamekuwa na mada yao katika wizara ikiwemo posho la kikazi, nauli na usimamizi wa mitihani mpaka hivi sasa walimu wangapi hawajalipwa posho zikiwa na likizo zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kuhusu maslahi ya walimu na maslahi mengine yote ya wafanyakazi hili limeanza kushughulikiwa na kutokana na kushughulikiwa kwake tumeona hivi karibuni walimu pamoja na wafanyakazi wengine wameongezewa mishahara yao. Lakini kadiri hali itakavyoruhusu serikali itaendelea kuangalia wafanyakazi wake wakiwemo hawa walimu. Pia kuna maposho mengine ambayo yanahusiana na walimu kwa mfano ya likizo, malimbikizo na mengineyo. Hii wizara inaendelea kuwalipa hatua kwa hatua.

Sasa kuhusu takwimu tutampatia kwa maandishi baadaye.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla sijauliza swali la nyongeza naomba nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza sana Mkurugenzi huru Bi Safia Rijali kwa kazi anazozifanya za vitendo za kufanya ziada katika skuli mbali mbali, ili kuona matatizo ambayo yanajitokeza katika skuli hizo. Kwa hiyo, naomba na wengine basi waige mfano kama huo wa mwanamke huyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba niulize swali la nyongeza. Pamoja na matatizo haya ambayo yamegundulikana, lakini pia Mhe. Spika, kuna tatizo kubwa na la muda mrefu katika skuli hizi. Kuna baadhi ya walimu wanauza biashara lakini biashara zile wanapofika skuli wanawapa wanafunzi ili wawauzie biashara zile, kiasi ambacho kinamfanya mwanafunzi yule baada ya kushughulikia masomo lakini anashughulikia biashara ya mwalimu huyu.

Je, Mhe. Waziri tatizo hili lini litakomeshwa katika skuli.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Kwanza tunachukua pongezi na tutampelekea Mkurugenzi wetu ambaye anafanya kazi na napenda niseme tu, kwa bahati mbaya sana labda ndiye anayesikika lakini Wakurugenzi wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanafanya kazi namna kama hii. *(Makofi)*

Pili niseme kwamba, suala la biashara katika skuli na hasa kwa walimu tumelipiga marufuku. Kwa hivyo, hatokuwepo mwanafunzi hata mmoja ambaye atafanya biashara kwa niaba ya mwalimu, kwa sababu tumefanya biashara. Hata hivyo, na wanafunzi wenyewe pia tumewapiga marufuku sio kazi yao kufanya biashara. Kwa hivyo, tunasema kwamba hakutokuwa na biashara ambayo itafanywa na walimu ama wanafunzi katika maeneo ya skuli. Ahsante.

Nam. 6

Tatizo la Maji Zanzibar

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza:-

Pamoja na jitihada za ziada za serikali kutatua tatizo la maji kwa wananchi wake. Mamlaka ya maji (*ZAWA*) imeshapata misaada mbali mbali ya wahisani wa Japan kupitia mradi wa (*JICA*) yapata miaka 10, hata hivyo, wafadhili hao na wengine wanatumia pesa zao katika miradi ya maji lakini mpaka leo tatizo hili halijaondoka na wananchi wetu wanaendelea kupata tabu.

(a) Je, ni lini tatizo hili litaondoka mijini na vijijini.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika katika kipindi cha miaka kumi iliyopita katika miradi ya maji na kwa nini mpaka leo tushindwe kupata maji safi na salama ndani ya visiwa vyetu.

(c) Ni maeneo gani yaliyofaidika na miradi hiyo ya maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tatizo hili la upungufu wa maji safi na salama kwa mijini na vijijini litaondoka au kupungua kwa kiasi kikubwa baada ya kukamilika kwa miradi ya uimarishaji wa miundombinu ya maji mijini inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Serikali ya India na Serikali ya Japani kupitia *JICA.*

Aidha, uendelezaji wa visima vya *Ras-el-Khaimah* na mradi wa uchimbaji wa visima na usambazaji wa maji, unaofadhiliwa na Serikali ya Watu wa China utatatua tatizo hilo kwa upande wa vijijini .

(b) Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita serikali imetumia Jumla ya shilingi 178,251,400,000/= kwa miradi ya maji safi na salama nchini, ambapo shilingi 160,698,400,000/= kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi 17,553,000,000/= ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, huduma ya maji safi na salama inapatikana ndani ya visiwa vya Zanzibar, ingawa tunafahamu kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo kwa baadhi ya maeneo kunakosababishwa kwa kiasi kikubwa na uchakavu wa miundombinu ya maji.

Hata hivyo, serikali inaendelea na jitihada zake katika kuimarisha miundombinu ya maji kwa kubuni miradi mipya ambayo itaifanyia ukarabati miundombinu hiyo, hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

(c) Mhe. Spika, maeneo yaliyofaidika na miradi hiyo kwa upande wa Unguja ni maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia Mradi wa Maji Mkoa wa Mjini Magharibi chini ya ufadhili wa *JICA* awamu ya kwanza na ya pili, miji mikuu mitatu ya Pemba na vijiji 9

vya Unguja na Pemba kupitia mradi wa maji safi na usafi wa Mazingira *AfDB*, maeneo 150 katika mikoa yote ya Unguja na Pemba kupitia mradi wa uchimbaji visima wa *Ras-el-Khaimah*. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri yenye kutia matumaini kwa asilimia fulani. Naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Pamoja na matumzi yote na miradi yote hii ya maji, mpaka sasa hivi unapozungumza hapo mbele Zanzibar mjini tumeweza ku-*cover* kwa asilimia ngapi upatikanaji wa maji.

(b) Inavyoelekea kwamba sasa hivi kuna ujenzi wa mtaro wa Mpendae kuja Jang'ombe, kuna ukatwaji wa mabomba ya maji na kupelekea uhaba au usumbufu wa maji kwa wakaazi wa Jang'ombe maeneo ya Lofi na maeneo mengine.

Je, serikali ina mpango gani mbadala kama unavyofanywa kwa upande wa *ZECO,* kutoa taarifa kuondosha maguzo na kuweza wale kuendelea na kazi zao za kuchimba. Je, ina mpango gani wa kuhamisha bomba zile, ili kuondokana na kukatwa kupelekea usumbufu kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, angerejea nimemsikia vipande vipande.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, lipi nirudie.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, swali lipi arudie, la pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, yote nilimsikia vipande vipande

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Spika, narudia tena, anisikilize kwa makini naomba.

(a) Pamoja na gharama zote zilizotumika za serikali na miradi yote hii mpaka sasa hivi ni asilimia ngapi ya maji yanayopatikana kwa wananchi wetu mjini.

(b) Sasa hivi kuna ujenzi wa mtaro wa maji machafu unaoshughulikiwa na *ZUSP* kutoka Mpendae kuja Jang'ombe, kuna ukatwaji au usumbufu wa mabomba ya maji safi na salama kwa wananchi na kupelekea kupata matatizo.

Je, wana mpango gani wa kudhibiti zile kama wanavyofanya kwa *ZECO* kuondoa nguzo za umeme kwanza na watu wakaja kuchimba mtaro. Je, kwa upande wa maji mna mpango gani wa kulifanya hilo ili kuondoa usumbufu wa upatikanaji wa maji katika maeneo ya Jang'ombe?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuhusiana na asilimia ngapi ya upatikanaji wa maji, hili lina- *differ* kutokana na siku hadi siku. Lakini kwa sasa kama sasa hivi mashine nyingi ziko vizuri, kama asilimia 75 maji yanapatikana katika maeneo mengi ambayo mtandao wetu upo. Lakini kama nilivyokuwa nimesema inategemea kuna siku nyengine *breakdown* zinakuwa nyingi na maji yanapungua, inawezekana leo yako 75 lakini kesho isifike hivyo, kwa hivyo sio kwamba imechukuliwa kama ni *constant*.

Lakini la pili kuhusiana na ukataji huo mara nyingi tunakuwa tunashirikiana, panapokuwa panafanywa mradi wataalamu wetu wanakwenda kuona ni namna gani mabomba yapo salama. Inapotokezea bahati mbaya katika maeneo mengine, basi taarifa tunaletewa haraka, lakini kwa mradi mkubwa kama huo, mara nyingi wataalamu wetu wanakuwa wapo ili kuhakikisha namna gani mabomba hayaharibiki. Kwa hivyo, kama kuna taarifa nyengine yoyote, labda mabomba yameharibiwa, tafadhali atupe taarifa, ili twende tukatengeneze, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kuna ukosefu wa maji katika Shehia ya Bububu Kihinani, na huu unakaribia mwezi wa tatu tena tokea tatizo hilo litokee.

(a) Je, Mhe. Waziri wizara yako mnalijua hilo na kama mnalijua ni hatua gani ambazo mtazichukua ili kuweza kulitatua tatizo hili, na tukiangalia wanaopata shida ni wanawake ndio wanaosumbuka na kadhia hii ya maji kwenda kuyatafuta maji haya. *(Makofi)*

(b) Mhe. Spika, kuna msemo ambao wananchi wale wanalalamika wanasema kuwa mashine ile muliichukua mukaipeleka katika sehemu nyengine. Je, hilo ni kweli na kama ni kweli ni kwa sababu gani mukaichukua mashine ile na mukaipeleka katika sehemu nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, ni kweli ilikuwa Kihinani Bububu kuna ukosefu wa maji kulikosababishwa na kuungua kwa pumpu. Lakini siku tatu zilizopita mashine tayari inafanyakazi na taarifa nilizonazo kabla ya kuingia humu ndani maji yanapatikana. Kwa hivyo, kama ulikuwa una taarifa hiyo hebu naomba ulifuatilie tena hili.

(b) Mhe. Spika, ni kweli mashine iliondolewa kwa sababu ilikuwa tayari imeharibika na ndio maana ikatafutwa nyengine na sasa hivi imeshawekwa nyengine inafanyakazi. Lakini sio kwamba iliondolewa kwa kupelekwa sehemu nyengine kwa matumizi

mengine. Iliondolewa kwa sababu haifai imeharibika na ndio maana tukatafuta nyengine ambayo inatumika hadi sasa, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba na mimi nimuulize swali lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kuna tangi la maji ambalo limejengwa na ufadhili wa *Ras-el-Khaimah* katika eneo la Mchekeni, eneo la Kipandoni. Pia kuna kisima kimechimbwa katika eneo hilo hilo.

(a) Je, ni lini serikali itaunganisha ili kuwapelekea maji wananchi wa Kiwengwa pamoja na Kipandoni ili wapumzike na wao kunywa maji ya chumvi.

(b) Katika upembuzi yakinifu uliofanyika ni kiasi gani cha fedha kitatumika katika kufanya maji haya yaweze kutumika na kuwanufaisha wananchi wa Kiwengwa pamoja na Kipandoni, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba pale kuna *tank* na kisima cha *Ras-el-Khaimah* kama ambavyo nimesema. Visima vya *Ras-el-Khaimah* vipo vingi, lakini ni mipango ya serikali kwamba kila baada ya awamu tunaviunga kutokana na upatikanaji wa fedha. Sasa nimuombe tu kwamba tunakijua na kimo katika mipango ya kuungwa kusudi wananchi hawa wapate maji.

(b) Mhe. Spika, takwimu halisi hapa sina kwa eneo lile, naomba tu nije nikujibu kwa maandishi baada ya kufanya uchanganuzi wa bei, ahsante.

Nam. 35

Upotoshaji wa Taarifa Kupitia Vyombo vya Habari na Mitandao

Mhe. Suleiman Sarhan Said - Aliuliza:-

Baadhi ya wanahabari na vyombo vya habari na hata mtu mmoja mmoja wakati mwengine hutoa habari zisizo na uhakika ambazo bado serikali haijazitolea taarifa rasmi kwa kuwa zinahitaji uchunguzi.

(a) Je, serikali haioni suala hilo kuwa linaweza kusababisha taharuki kwa wananchi na upotoshaji mkubwa.

(b) Je, sheria za kuwadhibiti watu hao hazipo na kama zipo wanachukuliwa hatua gani.

(c) Je, serikali ikikaa kimya haioni inawapa nafasi watu na vyombo hivyo kutumia nafasi hiyo kwa lengo au malengo waliyokusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataallah*, ambaye ametuwezesha tena kurudi katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake namba 35, lenye vipengele (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Sekta ya Habari na Utangazaji ni moja ya sekta za huduma za jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama inavyotamkwa kwenye Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 18(1)(2) ya Katiba, naomba kunukuu:

Ibara ya 18(1)(2)

1. "Bila ya kuathiri sheria za nchi kila mtu yuko huru na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi na pia ana uhuru wa mawasiliano yake".

2. "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali chini na duniani kote, ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii".

Mhe. Spika, dhima ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelemisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na vyombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majarida, televisheni, filamu, *video*, *internet*, picha, vipeperushi, katuni na mabago. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano yamerahisha upataji na utoaji habari.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali lake Mhe. Suleiman Sarahan Said namba 35 lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakiri kuwa suala hili linaweza kusababisha taharuki kubwa kwa wananchi na upotoshaji mkubwa. Sheria Nam. 5 ya mwaka 1988 inayohusu Magazeti, Majarida, na vitabu inasisistiza ulazima wa waandishi wa habari na vyombo vyao kuzingatia sheria na katika kuandika na kutangaza habari za uhakika na za kweli. Wakati wote waandishi wa habari wanatakiwa kufuata Maadili na Kanuni za uandishi wa habari katika kuripoti habari za kweli na bila kutia chumvi au kubuni.

(b) Mhe. Spika, sheria za kuwadhibiti zipo kama nilivyoeleza awamu katika maelezo yangu kuwa Sheria Nam. 5 ya mwaka 1988 inayohusu magazeti, majarida na vitabu inaeleza bayana kabisa wajibu wa waandishi wa habari na vyombo vyao. Ikitokeza kuna mwandishi wa habari amekiuka Sheria basi kwa kupitia Sheria hiyo ataweza kuchukuliwa hatua.

(c) Mhe. Spika, serikali haikai kimya, kwa kupitia Idara ya Habari Maelezo, inajitahidi kuelimisha na kutoa ufafanuzi kuhusu habari ambazo zimepotoshwa na pia kuwaita

waandishi wa habari kuwaelekeza na kuwakumbusha wajibu wa kazi zao katika jamii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa sasa umefika wakati wa kwamba teknolojia imepanuka zaidi na kwamba sio lazima waandishi wa habari na vyombo ndio vinavyoweza kutapakaza habari ama za kweli ama za uovu, hata mtu mmoja mmoja anaweza kujitengenezea na akaweza kuirusha dunia nzima vitu kama hivyo.

(a) Je, serikali inawadhibiti vipi watu hawa na wanachukuliwa hatua gani.

(b) Kwa kuwa, serikali yetu imetoa nafasi kubwa sana ya kuweza mtu kutoa uhuru wake na kuweza kufanya maelezo yake mtu anavyojihisi mwenyewe katika uhuru wake. Lakini pia wakati mwengine ule uhuru unazidi mpaka unakuwa anavuka mipaka.

Je, serikali haioni sasa tukaiga baadhi ya nchi nyengine, tukatengeneza eneo maalum mtu akaenda huko akatukana, akafanya mambo yake mpaka akamaliza halafu akarudi katika jamii

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Suleiman Sarahan Said, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba kuna hatua mbali mbali ambazo wanachukuliwa waandishi wa hawa wa habari. Lakini pia na kwa wale au mtu mmoja mmoja kwa njia ya *internet* kama nilivyoeleza. Suala hili tumekuwa tukichukua hatua, lakini pia tuna wenzetu wa *TCRA* ambao wanahusika na mambo ya mitandao na mawasiliano, tunakaa nao kwa pamoja na ikibidi kama mtu huyu kakiuka masharti basi tunamchukulia hatua, ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe Naibu Waziri katika jibu lake (b) amesema kwamba ikitokezea mwandishi wa habari amekiuka sheria basi kwa kupitia sheria hiyo ataweza kuchukuliwa hatua.

Je, Mhe. Spika, katika mwaka 2016/2017 haijawahi kutokezea na kama imetokezea ni hatua gani ambazo zimechukuliwa na wizara yako na ni mwandishi gani, na kwa taasisi gani za habari, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Bahati Khamis Kombo, swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, hatua ambazo tunazichukua kwa waandishi wa habari ambao wanakiuka taratibu na sheria au kwa vyombo vya habari. Mhe. Spika, kwa sasa hivi kwa mtu mmoja mmoja kwa waandishi wa habari, bado hajajitokeza mwandishi wa habari aliyekiuka sheria. Lakini hatua tunazokuwa tukizichukua ni kuwafutia vibali vya kufanyia kazi, kusimamishwa kwa muda au kufikishwa Mahakakani.

(b) Mhe. Spika, vyombo ambavyo vimejitokeza kukiuka sheria kwa mwaka 2016/2017 vimejitokeza vyomb viwili, ambavyo ni Gazeti la Mtanzania Daima na Gazeti la Mwananchi. Vyombo hivi tulichukua hatua ya kutaka waombe radhi vile vyombo husika ambavyo wamevikosea na wao walifanya hivyo wameomba radhi. Mhe. Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi nianze kukupongeza wamba leo meza yako mbele imependeza na wanaume tunaweza na sisi pia. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, hao waandishi wa habari ni mmoja kati ya sehemu muhimu sana katika jamii yetu ambapo hupenda kuonyesha jamii na kuwasomesha mambo tofauti, lakini pia hufanya kazi katika mazingira mgumu ambapo wakati mwengine hunyooshewa vidole.

a) Je, ni utaratibu gani unaotumia wizara yako kuhakikisha kwamba waandishi wanashiriki katika mikutano hasa ndani ya Afrika ya Mashariki, na hasa yale ambayo yanafanyika Tanzania Bara ambayo inaandaliwa na *Medium Council* ya Tanzania pamoja na Tanzania *Editors Forum*.

b) Tumeona nchi nyingi huwapongeza waandishi kwa mambo mazuri ambayo wanafanya, ni aina gani ya tunzo ambazo serikali yetu hii kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, pamoja na wizara yake Mhe. Waziri imeandaa au mikakati kwa siku za mbele na miezi ya mbele, ili kuhakikisha tunawalinda na kuwapa moyo hawa wajasiri ambao ni waandishi wa habari katika kuhakikisha kwamba tunawalinda, tunawapenda na tunawaenzi.

Mhe. Spika: Mhe. Simai Mohammed Said, hilo swali ni jipya naomba ulilete kwa maandishi.

Nam. 54

Matumizi ya Kilimo cha *Green House* Kwa Wakulima Wadogo Wadogo:

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na sekta binafsi na Kampuni ya ZAIDI na TAHA kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 wamefanya kazi ya uhamasishaji wakulima katika kilimo cha umwagiliaji kwa matone *green house*, na kwa sababu vijiji vingi vya shehia ya Mtambwe Kusini vina rutuba nzuri kwa ajili ya kilimo kama vile vanilla, hiliki na vinginevyo ambavyo vina bei kubwa na vinaweza kuwapatia maslahi makubwa wakulima hao.

(a) Je, wizara kupitia mpango huo wa "*green house*" imewashajihisha vipi wakulima wa *spices* wa vijiji vya Bwagamoyo, Daya, Mkanjuni, Makongeni Mavuika na Tondooni kulima *spices* kwa kutumia mpango huu.

(b) Ni wakulima wangapi walionufaika na mpango wa kilimo cha kumwagilia kwa matone yaani "*green house*".

(c) Ni mafanikio gani ya mavuno waliyoyapata wakulima baada ya kulima kwa kutumia *green house* ukilinganisha na kilimo cha kawaida.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 lenye vipengele (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Napenda kufafanua kwamba umwagiliaji maji kwa njia ya matone *(drip irrigation)* na "*green house*" ni teknolojia mbili tofauti na zinaweza kutumika katika mazingira tofauti. Umwagiliaji wa matone unaweza kufanyika ndani au nje ya *"green house*". Zoezi la kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima kutumia teknologia ya umwagiliaji kwa matone na "*green house*" limefanywa na Asasi Zisizo za Kiserikali *(NGO's)* ikiwemo *TAHA* katika juhudi za kuleta maendeleo ya kilimo jambo ambalo wizara yangu inaliunga mkono.

Teknolojia hizi zina gharama kubwa na zinahitaji utaalamu zaidi ukilinganisha na ukulima wa kawaida. Wakulima wadogo wadogo wanahitaji kujengewa uwezo wa kuwa na mtaji na taaluma ya kutosha. Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Programu za kuimarisha huduma za Kilimo na Mifugo *(ASSP/ASDP)*, imeweza kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima wapatao 180 kwa kuwapa vifaa vya umwagiliaji kama vile matenki na mipira ya kumwagilia kwa wale wakulima wenye vyanzo vya maji.

Mhe. Spika, baada ya maelezo mafupi naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi haijaanza kazi ya kuwashajihisha wakulima wa *spices* wa vijiji vya Bwagamoyo, Daya, Mkanjuni, Makongeni Mavuika na Tondooni kulima mazao hayo kwa kuzingatia kuwa wakulima hao hawatoweza kumudu gharama zake na pia utafiti wa kina unahitajika, ili kuweza kujua na kuwapatia ushauri unaofaa kwa ajili ya mazao hayo.

(b) Wakulima 600 (400 Unguja na 200 Pemba) wamenufaika na mpango wa kilimo cha kumwagilia kwa matone na kwa upande wa *"green house"* kuna *green house* 15 (9 Unguja na 6 Pemba). Baadhi yake zinamilikiwa na zaidi ya mkulima mmoja.

(c) Wakulima wanaotumia *"green house"* yenye ukubwa wa mita 25 x mita 12 huvuna kwa wastani wa tani 2.5 za tungule au pilipili mboga. Hata hivyo, baadhi ya wakulima walipata changamoto za kutumia aina za *"green house"* ambazo hazikubaliani na hali ya hewa na mazingira yetu, hali hii iliwasababishia mimea kutokuota vizuri na uzalishaji

kupungua. Kupitia *NGOs* wakulima tayari wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza *"green house''* zenye kukidhi hali ya hewa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa sababu amezema kwenye jibu lake kwamba wakulima wa Kijiji cha Daya, Bwagamoyo vijiji vile nilivyovitaja ambavyo viko katika shehiya ya Mtambwe Kusini hawajawahi hata kuwafikia wizara kwa upande wa Pemba. Jambo hili ni jambo la kusikitisha kwamba wakulima wenyewe wameanza kuhamasika, sasa kwa kuwa wakulima tayari wameshahamasika kulima na kwa sababu wakulima wanaendelea kupanda na wizara kwa upande wa Pemba haijafanya hata kwenda kuwaona kuwapa ule moyo kama alivyoeleza yeye mwenyewe nataka nijue.

a) Ni sababu gani kwa wizara Pemba ambayo hadi leo imewafanya isiwafikie wale wakulima angalau kwenda kuwashajihisha kwa sababu wameonesha moyo mzuri na uwezo mzuri wa kuzalisha hizo *spice*.

b) Lakini pili nilitaka nijue ni kiasi gani cha gharama ambazo zingehitajika kwa mkulima kuanzia kwa hiyo gharama ya umwagiliaji kwa mkulima ambazo wanaweza hawawezi kuzimiliki.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kama nilivyomwambia Mhe. Mwakilishi kwamba kilimo hichi kinahitaji gharama kubwa zaidi sio kama hatujawafikia, tumewafikia na tumewatembelea na tumeona maendeleo yao. Lakini kama wapo tayari na wewe mwenyewe upo tayari kuwasaidia wakulima hawa basi na sisi tupo tayari kuwachukua wakulima hawa kuwaunganisha na taasisi hizi *NGO's* ambazo zina utaalam huo.

b) Mhe. Spika, kutokana na kwamba anahitaji gharama gani inachukua kwa kilimo hichi nitaomba nimjibu kwa maandishi ili niwe na uhakika zaidi wa gharama hizo.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri leo na kutokana na majibu niliyojibiwa juzi na serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto katika swali langu Nam.13 inaonesha dhahiri kwamba serikali yetu haifanyi kazi kwa mashirikiano. *(Makofi)*

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba jawabu hizo kutuletea hapa ni jawabu za mkanganyiko. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba arudie kutokana na yale makofi yaliyopigwa pale sikusikia nini kilichoendelea.
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tusikilizane. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma naomba urejee swali.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Mhe. Spika, kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi ya leo hii ukilinganisha na majibu ya Mhe. Naibu Waziri Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika swali langu Nam.13 ya kwamba kutokana na mazingira ya Zanzibar kwa kilimo cha *green house* haiwezekani.

Mhe. Spika, je. hawaoni kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi na serikali kwamba hawafanyi kazi kwa mashirikiano. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Sikusema hakiwezekani, isipokuwa nimesema kinawezekana lakini inategemea na *material* yenyewe na kama hakiwezekani, basi zisingekuwepo hizi *green house* 15 ambazo Unguja tunazo 9 na Pemba tunazo 6. *(Makofi)*

Nam. 113

Usumbufu Kwa Madereva wa Gari za Kokoto Kusini Unguja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mnamo tarehe 27/7/2017 katika eneo la Paje, madereva wa gari za kokoto walisimama kupatiwa risiti kwa ajili ya kupakia kokoto ambapo walielezwa kuwa mpaka hapo watakapopakia mzigo ndipo watapatiwa risiti hizo. Hata hivyo, wakati wakirudi na mzigo walisimamishwa njiani kwa madai ya kupakia mzigo huo bila ya risiti za malipo wakati awali walishaambiwa kwanza wakapakie ndipo wapatiwe risiti hizo.

(a) Je, kwa nini madereva wa gari hizo hawaelezwi kwa uwazi taratibu za upakizi na badala yake wanasumbuliwa.

(b) Kwa nini Maafisa wa Maliasili wanawasumbua madereva hao hata baada ya kufuata maelekezo ya Maafisa hao. Je, madereva hao wakalalamike wapi wanapohisi wameonewa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nitoe maelezo kuhusu utaratibu wa uchimbaji, usafirishaji na uuzaji wa maliasili zisizorejesheka ambao unaongozwa na Sheria Nam. 3 ya 2015 ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni nam. 17 ya 2003. Sehemu ya 7 ya Sheria Nam. 3, Kifungu Nam. 33 kinaeleza kwamba hakuna mtu yeyote atakayechimba, kuzoa, kusafirisha au kuuza maliasili zisizorejesheka zikiwemo kokoto bila ya kupata kibali kinachotolewa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Kifungu hicho kiko wazi na hakina utata na msingi wake ni kuwa muombaji anatakiwa akate kibali kwanza kabla ya kuchimba, kusafirisha au kuuza maliasili hizo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, madereva wengi wanaofanya kazi za uchimbaji na usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka zikiwemo kokoto wanaufahamu vizuri utaratibu huu wa kisheria. Utaratibu huu ndio unaotakiwa kufuatwa. Aidha, ningependa kueleza wazi kuwa hakuna mtendaji yeyote aliyeruhusiwa kubadilisha vifungu vya sheria iliopo na ninawaomba sana madereva wazielewe taratibu na kuzifuata na wasikubali kuelekezwa kinyume na taratibu. Miongoni mwa taratibu hizo ni pamoja na:
   a) Kukata kabali cha usafirishaji maliasili zisizorejesheka kabla ya kupakia.
   b) Kibali hicho kitafanya kazi kwa siku moja tu ya tarehe iliyooneshwa.
   c) Hairuhusiki kusafirisha maliasili baada ya saa 12 za jioni.
   d) Kibali kitafanya kazi kwa gari iliyoainishwa tu.

   Mhe. Spika, utaratibu huu ndio unaotumika na ndio unaofuatwa. Dereva anayekwenda kinyume na utaratibu huu anakuwa anatafuta urahisi lakini mwisho wa siku atapata usumbufu.

(b) Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu haijapokea malalamiko ya kusumbuliwa madereva au mwananchi yoyote yanayohusu ukataji wa vibali vya kusafirishia maliasili huko Paje. Hata hivyo, wizara yangu ipo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi bila ya usumbufu wowote. Iwapo kuna dereva au mwananchi yeyote ambaye anapata usumbufu wowote katika kusafirisha maliasili zisizorejesheka huku akiwa amefuata utaratibu nilioainisha, namuomba sana awasilishe malalamiko yake kwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka au kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo au hata kwa Waziri na Naibu Waziri wa wizara hii.

   Mhe. Spika, ninaahidi atasikilizwa na hatua mwafaka zitachukuliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kama kuna wizara inayoongoza kwa kujibu majibu marefu Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na hayana tija yoyote kwa wananchi.

Mhe. Spika, ndipo pale tunapowaambia Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri kwamba wanapopewa swali wakafanye utafiti, kwa sababu nimetaja tarehe, pahali na eneo husika. Sasa leo anakuja kujibu mambo haya msururu mzima ambayo hayana faida yoyote wala tija kwa wananchi, na wala sihitaji sheria ama kanuni.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kauli yako ulianza nayo kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanajibu majibu marefu nilitegemea wewe swali lako lingekuwa fupi sana kama mfano, lakini sasa hivi wewe ndio unatoa maelezo naomba umuulize swali tu Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba kumpa changamoto Mhe. Naibu Waziri kwa kutaka tushirikianekwa ajili ya kwenda kuthibitisha tukio hilo, pindipo ikithibitika kwamba maofisa wako wamefanya kitendo hichi uko tayari kujiuzulu, ili tupate uhakika wa swala hili. Mhe. Spika, kuna mtu anaitwa Haji wa Haji huyu ni nani katika Wizara ya Kilimo, Maliasili,

Mifugo na Uvuvi, mwanzo sheria unaambiwa ukapakie mzigo ili ukate risiti, sasa unapakiwa mzigo unafuatwa njiani, ili ukalipishwe tunafanya nini kwa wananchi, hichi cheo ni dhamana Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika: Swali lako Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali ni kwamba pindipo tukifuatana mimi na yeye yuko tayari kujiuzulu tukipata ukweli wa tatizo hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jibu swali la kufuatana na yeye lakini kipande cha kujiuzulu kiache.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsane sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo. Nipo tayari kufuatana na wewe kwenda kuhakikisha na kama kuna mtu amekosea, basi tupo tayari kumuadhibu na Haji wa Haji ni Afisa wa Idara ya Misitu, Maliasili Zisizorejesheka. *(Makofi)*

Nam. 76

Ujenzi wa Hospitali ya Kijitoupele

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Ujenzi wa Hospitali ya Kijitoupele umegharimu kiasi cha shilingi za Kitanzania milioni 74.

Je, Mchango wa serikali ulikuwa kiasi gani.

Mhe. Naibu Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisanaomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba ujenzi wa jengo la Kijitoupele ni ujenzi wa Kituoa cha Afya na sio hospitali, kuna tofauti baina ya kituo cha afya na hospitali, lakini pia ujenzi wa jengo hili umegharimu jumla ya shilingi milioni 84 na sio 74 kwa maelezo ya viongozi wa Jimbo la Kijitoupele.

Mhe. Spika, kwa kawaida majengo ya Wizara ya Afya iwe kituo au nyumba ya *staff* ambayo yanajengwa kwa nguvu za wananchi, taasisi au Kamati ya Maendeleo katika maeneo husika, serikali huwa haiingizi mchango wowote hadi pale wahusika, wa ujenzi huo watakapoomba au kuonesha nia ya kwamba wanahitaji kusaidiwa katika hatua iliyofikia ujenzi huo.

Hivyo basi, ujenzi wa kituo cha Afya Kijitoupele, ulianza kwa nguvu za Viongozi wa Jimbo la Kijitoupele na kupitia katika hatua mbali mbali, na hadi sasa bado uko katika mikono salama ya uongozi wa jimbo hilo.

Mhe. Spika, katika hatua za awali na kwa mashirikiano na uongozi wa jimbo, umelikagua jengo hilo katika vipindi tofauti, na kufanya mazungumzo na uongozi wa jimbo kisha kukubaliana kushirikiana katika kukamilisha ujenzi wa jengo hilo.

Mhe. Spika, hadi sasa bado hakujawa na mchango wa kifedha kutoka Wizara ya Afya, bali wizara inatoa miongozo mbali mbali ya ujenzi huo, katika kutafuta njia za kusaidia kupata wahisani watakaosaidia kumaliza ujenzi huo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) madogo sana tu.

a) Kwa kuwa, wananchi wana hamu Kijitoupele kuona hospitali hiyo inakamilika, Wizara imejipanga vipi kuongeza nguvu hizo kukamilisha ujenzi huo uliobaki.

b) Je, ni lini wizara itakwenda katika mradi huo kuona ukweli wa jengo hilo lilivyo.

Mhe. Naibu Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, wizara inajitahidi kutafuta wafadhili ili kulikamilisha jengo lile haraka iwezekanavyo, kwa sababu baada ya kulikagua imeliona kwamba ni jengo ambalo litawasaidia sana wananchi wa Kijitoupele pamoja na maeneo jirani.

b) Lini tutakwenda katika ujenzi wa jengo lile. Mhe. Spika, kwa kawaida ya kila baada ya mwezi mmoja huwa tunapita pamoja na uongozi wa jimbo kuliangalia na ku-*create* nini tufanye, ili tuweze kukamilisha kwa haraka. Kwa hiyo, ni kitu ambacho tunafanya mara kwa mara.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze Wizara ya Afya kwa kuwa suala hili limetokana na viongozi wa jimbo hilo pamoja na wananchi wenyewe kujenga kituo cha afya hichi ni muhimu kwa upande wetu. Lakini nasema tu kwamba mashirikiano mazuri tuliyopata kati ya viongozi na Wizara ya Afya baada ya mchango mkubwa uliotokea wa shilingi milioni 88 nikiasi kikubwa kwa uwezo wetu.

Mhe. Spika, Mbunge aliyepita Mhe. Haji Juma Sereweji na Mwakilishi Mstaafu Mhe. Shamsi Vuai Nahodha walichangia 64 milioni. Kwa upande wangu katika kuendelea jengo hilo Mfuko wangu wa Jimbo milioni 20 nimezitumbukiza hapo hapo. Kwa kweli, hivi sasa plasta tayari, madirisha tayari, *fitting* ya umeme tayari. Je, kwa kuzingatia ubora huo tulioufikia na kazi ilibakia ni *tails* na *hard bord* juu, serikali kupitia wizara itachukua hatua gani za haraka haraka kulimaliza jengo hilo ambalo akinamama watajifungu hapo na akinababa na watoto watapata huduma hapo, lini watafanya hilo kwa kushirikiana na sisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Wizara ya Afya katika hatua mliyofikia inaumwa kulikoni mnavyoumwa nyinyi na jengo lile la Kijitoupele. Lengo la Wizara ya Afya ni kuhakikisha

wananchi wa Kijitoupele na maeneo jirani wanapata huduma zilizo bora haraka iwezekanavyo katika jengo lile.

Hivyo, basi naomba nikuhakikishia kuwa Wizara ipo mbioni kuhangaika, kutafuta wafadhili pamoja na kuongeza kile ambacho kitabidi kuongezwa kuhakikisha kwamba jengo lile linakamilika na *Inshallah* kwa uwezo wa Mungu kwa sababu juhudi zipo na mashirikiano baina ya wizara na viongozi ya jimbo yapo na yanaonekana, tunaamini kwamba tutalikamilisha haraka. *(Makofi)*

Nam. 55

Madereva Wanaoendesha Gari Wakiwa Wamelewa

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa moja ya sababu za ajali za barabarani ni madereva kuendesha gari hali wakiwa wamelewa. Na kwa sababu kwa sasa hatujaanza utaratibu wa kuwasaka na kuwakamata madereva wanaoendesha gari wakiwa wamelewa.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kukabiliana na suala la madereva wanaoendesha gari wakiwa wamelewa.

(b) Je, serikali haioni kwamba ipo haja ya kudhibiti kutoa leseni ya vyombo vya maringi mawili kwa ajili ya kulinda maisha ya vijana wetu hasa T 1 ambao wanaangamia na kusababisha hasara kubwa kwa taifa kwa kupoteza nguvu kazi yake.

(c) Je, wizara kwa kushirikiana na Idara ya leseni haioni kwamba wakati umefika kuzifuta leseni za kila mwendeshaji chombo cha maringi mawili atakayepatikana na hatia ya kusababisha ajali kwa uzembe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali kwa kutumia kifungu cha 123 cha Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 inawakamata madereva wote watakao bainika kuendesha gari wakiwa wamelewa.

(b) Serikali imeona ipo haja ya kudhibiti kutoa leseni kwa madereva wa vyombo vya maringi mawili.

(c) Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Usafiri na Leseni pamoja Jeshi la Polisi tayari wameandaa mpango wakuwaorodhesha madereva wote wanaosababisha ajali kwa kupunguza alama katika leseni zao *(demerit point system).*

Mhe. Spika: Ahsante sana kwa majibu mafupi na mazuri.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya kitaalamu ya Mhe. Waziri lakini ningependa nijuwe ni utaratibu gani au utaalamu gani utakaotumika kuweza kubaini wale madereva ambao watakuwa wanaendesha vyombo hivyo vya moto wakati wakiwa wamelewa.

a) Ni utaalamu gani wanaotumia kwa kuwabaini kwamba huyu sasa hivi anaendesha gari hali ya kuwa amelewa.

b) Na kwa sababu tumezungumza kwamba kuna mpango wa kusitisha idadi ya utoaji wa leseni. Mhe. Spika, naomba kujua je, kuna totauti gani ya leseni zilizotolewa kati ya mwaka 2016 na hii 2017 kwa wale waendeshaji vyombo vya maringi mawili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu viwili (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Jeshi la Polisi ndiyo wenye chombo hicho, tunakiri kwamba wana vyombo vichache kila Mkoa wana chombo kimoja ambacho hicho ndicho kinachotumika sehemu zote hata Tanzania Bara katika kumpima dereva wakati akiendesha chombo kama ametumia kilevi na kwa kiwango gani cha kilevi.

b) Kama nilivyosema kwamba suala hili lipo katika mpango wa kulifanyia kazi. Kwa hivyo, mpaka sasa hivi leseni zote zinazotolewa ndizo zile zile na kwa *class* zile zile, ambazo tumejiwekea na wala hamna mabadiliko yoyote.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni kweli kwamba tunalo tatizo juu ya suala zima na majibu aliyoyatoa. Lakini niulize swali dogo.

a) Ni utaratibu gani unaotumia wizara kuhakikisha kwamba magari ya abiria yanayopakia wageni kama watalii, pia na wale ambao wanakuja kutembelea visiwa vyetu, lakini pia magari yanayobeba wanafunzi kuwapeleka maskulini asubuhi kwamba wale madereva wanakuwa hawana kiwango, kuhakikisha kwamba kiwango chao kipo cha wastani au hakijapindukia cha ulevi kichwani wakati wanatimiza majukumu yao.

b) Pia katika suala zima la madereva wetu hawa wanaokuwa wanaendesha magari huku wakiwa na kiwango cha kupitilizia ndani ya vichwa vyao, wamekuwa pia kuna mapungufu ambayo yanajitokeza kuwa na nuru ndogo ya macho yao kuweza kuona. Je, Mhe. Waziri unatumia utaratibu upi kuweza, ili kuhakikisha kwamba madereva haya macho yao wanapata aidha miwani au msaada, ili waweze kutimiza majumu yao hawa wale wanaobeba abiria pamoja na wanafunzi nyakati tofauti. Ahsnte sana

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kweli, kama nilivyosema kuna utaratibu maalum ambao tumejiwekea sisi kwa magari yote ya abiria na yanayochukua watalii, kuna utaratibu ambao umewekwa na viwango vyao vya ada maalum vimewekwa, ambavyo kila dereva anatakiwa avifuate wakati wa kwenda kuchukua leseni yake na wakati wa kwenda kulipa kwa ajili ya kuruhusiwa gari zake kufanya kazi.

Mhe. Spika, sisi tunapendelea sana madereva hasa wanaoendesha vyombo hivi vya kuchukulia abiria wawe na uoni mzuri sana. Ndio maana sasa hivi dereva kila baada ya miaka miwili anapofanyiwa majaribio ya kutaka kupanda daraja, lazima tuhakikishe kwamba tunapata taarifa za Wizara ya Afya kuhusiana na uoni wake wa macho. Vile vile, sisi huwa tunapendelea sana madereva wanaoendesha vyombo hivi vya abiria wawe na uoni mzuri zaidi na hatupendi wawe wanatumia miwani.

Nam. 66

Ubovu wa Baadhi ya Barabara za Mijini Kutokana na Athari ya Mvua

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) inastahili pongezi kwa kazi kubwa wanayofanya ya kufanya matengenezo ya barabara huku wakiwa na changamoto ya upungufu wa vifaa vya kutendea kazi hizo. Pamoja na hatua kubwa idara hii ilizochukuwa za kuziba sehemu zilizoharibiwa na mvua za masika, bado sehemu kadhaa zimebakia hazijazibwa.

(a) Je, ni lini Idara ya UUB itamalizia kuziba viraka hivyo katika barabara ya Michenzani Makontena, Saateni JKU-Kwajumapweza, Bububu Jeshini na maeneo mengine ya barabara kuu.

(b) Katika kukamilisha kazi hizo, serikali imejipanga vipi kuisaidia Idara ya UUB kwa kuiongezea vifaa zaidi vya kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, baada ya kupokea pongezi hizo sasa napenda kumjibu kma ifuatavyo:-

(a) Wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara inatambua kuwa bado yapo maeneo ambayo hayajazibwa mashimo yakiwemo baadhi ya maeneo ya barabara ya Saateni JKU-Kwajumapweza, Bububu Jeshini, sehemu ya Michenzani Makontena na maeneo mengine

ya barabara kama Koani, vile vile Pete hadi Jonzani, Chuini kwa Unguja na hata maeneo mengine ya Pemba.

Maeneo aliyoyataja Mhe. Mjumbe hasa eneo la Saateni JKU na ZBC- Michenzani makontena, Mtoni *(depot)* kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa kuwa haya masuala yalikuja kabla hatujaanza ile kazi, tayari hivi sasa tumeshaanza kuyafanyia kazi na sote mashuhuda, Makontena pale tunaendelea na kazi na vile vile Saateni tunaendelea na kazi na Bububu Jeshini vile viraka tumeshaviziba. Hapo baadaye tunategemea kazisa kwamba tutaifumua sehemu ya bubu pale jeshina kama tulivyoifumua sehemu ya michenzani na Saateni.

(b) Mhe. Spika, serikali, inafanya mchakato wa kuwapata wazabuni wa kuleta baadhi ya mitambo na zana za ujenzi wa barabara, ambapo kwa upande wa Unguja mchakato wa ununuzi wa mtambo wa kisasa wa kupikia lami uko kwenye hatua za mwisho sambamba na mchakato wa ununuzi wa mtambo wa kusambaza lami ya kupika *(paver)* na gari la lami (*bitumen trunk)* kwa upande wa Pemba nao unaendelea vizuri.

Serikali, inatambua kuwa Idara ya UUB inakabiliwa na upungufu wa nyezo mbali mbali za kazi za barabara, nyenzo ambazo gharama zake ni kubwa. Hivyo, serikali itaendelea kuiimarisha Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa kuitafutia nyenzo husika kwa awamu ili kuiwezesha kufanyakazi zake za matengenezo ya barabara kwa urahisi na kwa muda mfupi na gharama nafuu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, wizara imefanya tathmini gani katika ujenzi wa barabara kujua baada ya muda mfupi hasa wakati wa mvua barabara hiyo huanza kuchimbika na serikali kupoteza fedha nyingi.

b) Barabara zinazojengwa zinahitaji viwango vya ubora na zinahitaji kufanyiwa ukarabati. Je, baada ya muda gani zinahitajiwa ukarabati huo.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Jaku, Hashim Ayoub, leo unauliza vizuri sana masuali yako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kama ulivyosema barabara ina muda wake maalum wa kuishi, barabara nyingi zinamuda wa kuishi kuanzia miaka 10 mpaka 15 na nyengine inakuwa na miaka 20. Kwa hiyo, kwa utaratibu kila wakati barabara inakiwa ifanyiwe *routine maintenance*, ili kuhakikisha kwamba ile barabara inadumu kwa muda mrefu.

b) Lakini kama ulivyosema tunatambua kwamba kuna baadhi ya wakati barabara zinapojengwa zinakuwa zinajengwa kwa mujibu wa barabara husika. Kwa hivyo, sisi tunapojenga barabara kuu tunahakikishwa kwamba zinajengwa kwa viwango vyote na ndiyo maana baadhi ya wakati huwa tunatoa zabuni, ili kuhakikisha kwamba zile barabara zinajengwa katika kiwango cha kimataifa. Kutokana na hali hiyo, ndio maana unakuta barabara ya Bububu mpaka Mkokotoni na barabara nyengine hivi sasa tupo katika hatua ya mwisho ya kumtafuta mkandarasi.

   Mhe. Spika, huo ndio utaratibu unaotumika lakini barabara nyingi tunahakikisha kwamba zinajengwa kwa viwango, ili zipate kudumu kwa muda ambao unahitajika kwa mujibu wa mkandarasi ambao wamezijenga barabara. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri barabara ambazo ziliathirika kwa mvua za vuli moja wapo ikiwa ni barabara ya Ukutini kwa Mtora katika sehemu ya Fueni na Mteng'ombe na wananchi walilazimika barabara zile kufikia mashimo na milima pia imeshuka. Je, ni lini barabara ile itafanyiwa matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba sisi wakati wowote tunataka kuhakikisha kwamba barabara zote tunazijenga kwa kiwango ambacho kitapitika wakati wowote, ili kuwaondoshea kero wananchi. Kwa kweli, pale tunapopata fedha basi barabara zile tunazifanyia matengenezo ili zipitike kwa haraka.

Vile vile, tunajenga barabara kwa mujibu wa mpango wa bajeti tulioleta hivi sasa. Nina imani kwamba kuna barabara kupitia kwake tunaijenga ya Ole Kengeja. Kwa hivyo, naomba atustahamilie, wakati wowote tutakapopata fedha basi tuangalie namna gani za kutatua zile sehemu zizokuwa na matatizo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umekwisha kwanza nitoe shukrani kwa namna ambavyo tumeweza kuyaendesha maswali leo. Lakini bado nasisitiza serikali ijitahidi kujibu kwa ufupi hasa masuala ya nyongeza.

Pia na Waheshimiwa Wajumbe, mnapouliza haya masuala ya kupongeza watu muyapunguze, ili muda wetu uwezi kutosha kama ulivyotosha leo. Pia nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa namna ulivyouliza maswali yako dakika za mwisho kwa ufupi sana, huo ndio utaratibu ambao unapendeza ndani ya Baraza. Ahsante sana kwa utaratibu huo umeanza nao natagemea utaendelea. *(Makofi)*

Baada ya hayo, Waheshimiwa Wajumbe hakuna matangazo ya wageni na tunaendelea na shughuli inayofuata. Lakini kuna Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniona, naomba kusimama kwa kanuni ya 26. Nilikuwa nataka kuzungumza juu ya kadhia ya wafanyakazi wa Mkoa wa Kusini ambao walituhumiwa kula pesa za posho za wazee, katika kipindi cha Bajeti nilizungumza na Wizara ya Utumishi wa Umma juu ya kuweza kujadiliana lakini mpaka leo sikupata jibu. Sasa kwa idhini yako naomba uniruhusu niweze kulizungumza.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe umesimama kwa kifungu cha 46 kifungu hicho kinasema Hoja kuhusu haki za Wajumbe

> "46(1) ni Mjumbe anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki, fursa na kinga za Wajumbe au uwezo wa Baraza atafanya hivyo wakati unaofaa kutuatana na mfululizo wa shughuli uliowekwa na Kanuni na 27(1) na atamuarifu Spika, mapema kuhusu kusudio lake hilo na jambo ambalo anataka kuliwasilisha"

Bahati nzuri uliniwasilishia kusudio la kusimama ingawa hukunipa jambo mahususi ambalo unataka kulizungumzia. Lakini jambo unalotaka kulizungumzia halihusiani na haki za Wajumbe linahusiana na wafanyakazi wanaotuhumiwa nafikiri, hebu liweke vizuri maana yake haliko vizuri sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru kwa maelezo yako mengi mazuri tu na wala sitaki kupingana na kiti chako na sithubutu kufanya hivyo. Uki- *refer* kifungu cha 27(j) katika haki na fursa ya maelezo binafsi ya mjumbe ambayo ndiyo ninayotaka kuyatoa hapa kutokupata taarifa kamili ambayo niliiarifu na Kamati ya Matumizi na wewe ndiye uliyekuwa Mwenyekiti, ulielekeza nishirikiane na wizara, ili nipate taarifa zile sahihi kwa waajiri wangu wananchi, ndiyo nataka kulielekeza pale.

Mhe. Spika: Ahsante. Nadhani Mhe. Mjumbe hakuna haja ya kulijadili hapa, lakini ilivyokuwa serikali imelisikia nafikiri serikali italifanyia kazi halafu litaletwa, ili sote tuweze kufaidika na hilo.

Vile vile, nikuombe uonane na serikali, ili uwaekee wazi zaidi hayo maeneo ambayo unakusudia, ili waweze kuyafanyia kazi na hatimaye tuweze kuletewa hapa halafu tutaweza kuyasikia sote kwa pamoja.

Baada ya maelezo yangu hayo Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKAI

Ripoti ya Wizara ya Ardhi Maji, Nishati na Mazingira ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa Mwaka 2016/17

Mhe. Spika: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, ili awasilishe hiyo ripoti. Waheshimiwa Wajumbe, walioomba kuchangia ni wachache mpaka sasa hivi kwa hivyo nafasi bado zipo mnaweza kuendelea kuleta maombi yenu. Mhe. Waziri tafadhali sana.

Samahani Mhe. Waziri kabla hujaanza naomba nimkaribishe Naibu Spika aje kukalia kiti. Mhe. Naibu Spika karibu.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri endelea.

Waziri wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa ushauri wa maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano iliwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi ripoti ya shughuli zao kama ilivyoekezwa na Kanuni ya 108(1) Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo ya 2016, katika ripoti hiyo Kamati ilitoa maagizo 29 ambayo yanapaswa kutekelezwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza kazi zake kamati ilitembelea Idara na taasisi zote zilizochini ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na kupokea taarifa za utekelezaji, ufatiliaji pamoja na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ilipokea maagizo hayo na kuyatekeleza kama ifuatavyo:

Agizo la 1. Kamati inashauri Wizara ya Ardhi Maji Nishati na Mazingira iwe na chanzo kimoja, Kitengo cha Kusajili Ardhi katika Taasisi zake zinazohusiana na masuali ya ardhi.

Utekelezaji. Wizara ya Ardhi Maji Nishati na Mazingira imeanzisha Chombo cha Usajili wa Ardhi ambacho ni Afisi ya Mrajis Ardhi Tokea mwaka 2007. Taasisi hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Ardhi Nam. 10 ya 1990. Miongoni mwa kazi zake ni kusimamia na kuratibu shughuli za usajili wa ardhi hapa Zanzibar. Hivyo, ofisi hiyo ndio yenye dhamana ya kusajili ardhi yote Zanzibar.

Agizo la 2. Kamati inaiomba Kamisheni ya Ardhi iandae mpango maalum wa kuwapatia mafunzo ya masuala ya ardhi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwemo masuala ya upimaji, usajili, utambuzi, umiliki na matumizi ya ardhi.

Utekelezaji. Kamisheni ya Ardhi inategemea kutekeleza agizo hilo baada ya kukamilika Sera ya Ardhi, ambayo itapekea urekebishwaji wa sheria zitakazowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Hivyo, Kamisheni ya Ardhi itatoa taaluma kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na washirika wengine kabla ya kuwasilisha miswada ya marekebisho ya Sheria za Ardhi.

Agizo la 3. Kamati pia inaiomba Kamisheni ya Ardhi ifanye utafiti maalum kuangalia mahitaji ya wananchi juu ya makaazi, ili kuondokana na migogoro mtambuka ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kabla ya kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Miji na Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi *(National Special Development Strategy)* ilifanya tafiti juu ya matumizi mbali mbali ya ardhi ikiwemo makaazi bora.

Mipango hii Mikuu ya Ardhi ni matokeo ya tafiti zilizofanywa na imeainisha maeneo ya makaazi kwa mahitaji ya wananchi kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Matarajio ya wizara ni kwamba mipango hii ambayo imeainisha mahitaji ya wananchi ya makaazi itasaidia kwa kiwango kikubwa kuondosha migogoro ya ardhi.

Agizo la 4. Kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kwa ujumla kuipatia Mahkama ya Ardhi jengo jengine la kufanyia kazi, ili kunusuru afya za wafanyakazi wake kutokana na uchakavu wa jengo linalotumika hivi sasa.

Utekelezaji. Wizara imefanya mawasilisano na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ili kujua hali halisi ya uimara wa jengo hilo.

Baada ya Mamlaka kufanya ukaguzi na tathmini ya jengo hilo ambayo inaonesha kwamba mihimili *(structure)* ya jengo hilo bado ipo imara, hata hivyo inahitaji matengenezo ili kuzuia athari zilizoanza kujitokeza na kuliboresha zaidi. Tathmini ya gharama za matengezo imeshafanywa na kwa sasa Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango juu ya uwezekano wa kupatiwa fedha kwa ajili ya matengenezo.

Agizo la 5. Vile vile, kamati inaiomba wizara iharakishe kuyapima maeneo yanayotengwa, kwa ajili ya shughuli pamoja na miradi ya maendeleo na wahusika kupatiwa hati, ili kuepusha uvamizi wa sehemu hizo.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Wizara imepokea agizo la kamati na upimaji wa miradi ya maendeleo inaendelea kwa mujibu wa maombi na mahitaji yanavyojitokeza. Aidha, wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi, inaendelea kupanga maeneo hayo kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi.

Agizo la 6. Kamati inaitaka wizara impatie eneo jengine mmiliki wa *FK Enterprise Company*, ili kupisha mradi mkubwa wa uwekezaji, ambao uko tayari kuanza katika eneo la uwekezaji huko Nungwi.

Utekelezaji. Eneo hili tayari limesharudi serikalini.

Agizo la 7. Kamati, inaiomba Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) ifanye uhakiki wa kutosha na kukagua upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu yake na baadaye kutoa ripoti kwa wadau wote ikiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Utekelezaji. Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) imekua na utaratibu wa kukagua miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji. Aidha *ZAWA* kwa kushirikiana na mradi wa *JICA* imefanya juhudi za makusudi kuhakiki na kukagua upotevu wa maji katika maeneo ya mjini Unguja.

Agizo la 8. Kamati, inaendelea kuishauri Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kuweka afisa husika wa maji katika kila jimbo ambaye atafuatilia vizuri na kwa ukaribu zaidi masuala yote yanayohusiana na maji katika jimbo husika.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Maji tayari imeshaweka Maafisa katika Wilaya zote Unguja na Pemba ambao wanahusika na kufuatilia masuala ya maji ndani ya Wilaya hizo. Aidha Mamlaka itaongeza maafisa wa maji katika maeneo hayo kadri ya uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

Agizo la 9. Kamati, inaitaka Mamlaka ya Maji iendelee kudhibiti uvamizi wa vianzio vya Maji kwa kuviwekea vizuwizi (uzio) na matangazo yanayokataza ujenzi, uchimbaji wa mchanga kiholela hali ambayo husababisha uharibifu wa mazingira katika sehemu hizo.

Utekelezaji. Mamlaka ya Maji inaendelea na kazi ya kuvijengea uzio vianzio vya maji katika maeneo ya Kinumoshi, Kianga, Mwembemchomeke, Chaani, Kiboje, Mgonjoni, Mwanyanya na Mtopepo.

Agizo la 10. Kamati, inaiomba Mamlaka ya Maji kufikiria kuanzisha huduma ya kuchangia maji kwa njia ya simu za mkononi, ili kuweza kurahisisha huduma ya ulipaji maji na kudhibiti mapato yatokanayo na huduma hiyo kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Kwa upande wa kulipia huduma ya maji kwa njia ya simu suala hili tayari limekwishafanyiwa kazi ambapo Mamlaka ya Maji inategemea kuingia Mkataba na benki ya *NMB* na *PBZ* pamoja na mitandao ya simu ili kuharakisha au kurahisisha huduma ya malipo kwa wananchi, zoezi hili lipo katika hatua za kusaini mikataba na kuanza kazi.

Agizo la 11. Kamati, inaishauri Mamlaka ya Maji kushirikiana kikamilifu na viongozi wa majimbo au wafadhili wanaotaka kuanzisha miradi ya maji kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya kuanzishwa kwa miradi hiyo.

Utekelezaji. Mamlaka ya Maji imekua na utaratibu wa kutoa elimu kwa kila shehia pamoja na viongozi wake juu ya umuhimu wa kushirikiana wakati wa kuanzisha miradi ya huduma za maji katika shehia na majimbo, ili kuwepuka changamoto mbali mbali zinazoweza kujitokeza.

Mhe. Naibu Spika, agizo la 12. Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji kuhakikisha inayapima na kutafuta hati miliki za maeneo yote ya vianzio vya maji Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Mamlaka ya Maji imelipokea agizo hilo na kazi ya kuyapimisha maeneo ya viazio vya maji ili kuyapatia hati miliki tayari imeanza na hadi hivi sasa maeneo yafuatayo tayari yameshapimwa.

Maeneo hayo ni:-
Shakani, Kwarara, Kijitoupele, Dimani, Maungani, Kiashange Chaani, Kiashange Kibeni, Nyakurungwi Jumbi, Nyakurungwi Ubago, Chunga, Mwembemachomeke na Kianga kwa

upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Taifu Wete, Ole kianga Chake Chake na Miembeni Chake Chake.

Agizo la 13. Kamati inaliomba Shirika la Umeme (*ZECO*) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, izungumze na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kuweka utaratibu wa malipo ya umeme kuingizwa moja kwa moja katika *Account* za *ZECO* badala ya kuingizwa katika *OC* za taasisi husika.

Utekelezaji. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Shirika la Umeme imefanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango ambayo imeahidi kulifanyia kazi suala hili kwa kuangalia uwezekano wa wizara hiyo kulipia matumizi ya umeme ya Taasisi za Serikali moja kwa moja katika akaunti za *ZECO* badala ya kuingizwa katika *OC* za taasisi hizo.

Agizo la 14. Kamati, inaendelea kulishauri Shirika la Umeme kuongeza ulinzi katika vituo vyake vyote vya uzalishaji na usambazaji umeme hususani katika maeneo ya Fumba, Mtoni pamoja na Ras – Kiromoni.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Shirika la Umeme (*ZECO*) linaendelea kuimarisha hali ya ulinzi katika vituo vyake vyote hususani vya kupokelea umeme vya Fumba na Mtoni. Sambamba na kuweka walinzi wa vikosi vya Serikali (Polisi na KMKM), vile vile shirika limechukua hatua ya kufunga kamera za ulinzi (*CCTV*) katika vituo hivyo.

Agizo la 15. Kamati, pia inaliomba Shirika la Umeme kufanya utaratibu wa kuyapima na kuyatafutia hati miliki maeneo yote ya vianzio vya umeme na vituo vya umeme kwa Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, shirika limeshaanza taratibu za kutafuta hati miliki kwa maeneo yake yote ikiwemo ya vianzio vya umeme vya Unguja na Pemba. Aidha, baadhi ya maeneo hayo tayari yameshapatiwa hati miliki zake baada ya kukamilika taratibu maeneo ya vituo vidogo *(sub station)* yafuatayo yamepimwa na kupatiwa hati miliki maeneo yenyewe ni Kariakoo, Mwembetanga, Mkele, Mombasa, Mtoni Kidatu, Kajificheni, Malindi, Darajani, Fumba, Saateni, Shangani, Mkokotoni na Gamba kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Wesha, Mkumbuu na Tibirinzi. Taratibu za upimaji kwa maeneo mengine zitaendelea hatua kwa hatua.

Agizo la 16. Kamati inaiomba Idara ya Nishati na Madini ijiandae vyema katika kuwaandaa wafanyakazi wake katika usimamizi wa fani ya Mafuta na Gesi Asilia.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika Idara ya Nishati na Madini inaendelea na hatua za kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani za Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, hivi sasa wafanyakazi watatu (3) wako masomoni kwa ngazi ya shahada ya pili nchini Norway na China. Vile vile, mfanyakazi mmoja (1) tayari amesharipoti kazini baada ya kumaliza masomo yake ya shahada ya pili nchini Norway katika fani ya mafuta na gesi asilia.

Agizo la 17. Kamati inaitaka idara ianze mchakato wa kuwajiri vijana walioko masomoni wanaosomea fani ya mafuta na gesi asilia, ili iwadhibiti mapema kwa manufaa ya taifa.

Utekelezaji. Mhe. Niabu Spika wizara tayari imechukua jitihada za ziada katika kuwaorodhesha wanafunzi wanaosoma masomo ya mafuta na gesi asilia katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Aidha, wizara tayari imeshapeleka barua ya maombi ya uajiri wa vijana waliomaliza masomo yao katika fani ya mafuta na gesi asilia.

Agizo la 18. Kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Idara ya Nishati na Madini kuendelea na hatua ya kutoa elimu kwa wananchi, ili waweze kuelewa umuhimu na faida ya rasilimali hiyo.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Nishati pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar *(ZPRA)* inaendelea na mchakato wa kutoa elimu kwa wananchi, Taasisi za Serikali, Serikali za Mikoa na Taasisi za elimu, ili kuhakikisha suala la mafuta na gesi asilia linaeleweka vizuri Unguja na Pemba.

Agizo la 19. Kamati, inaitaka serikali kwa kushirikiana na wizara kuharakisha uanzishwaji wa taasisi pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Mafuta na Gesi Asilia kama sheria inavyoelekeza.

Utekelezaji. Mhe. Niabu Spika, katika kuhakikisha kuwa suala la mafuta na gesi asilia linasimamiwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshaanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar *(ZPRA)* mnamo mwezi wa Machi, 2017 kama ilivyotakiwa na Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2016 ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

Taasisi hiyo tayari imeanza shughuli zake rasmi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iko katika hatua za kukamilisha usajili na uanzishwaji wa Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia ya Zanzibar (*ZPDC*).

Agizo la 20. Kamati inaishauri wizara kwa kushirikiana na mamlaka kubadilisha mfumo wa uagiziaji na uingizaji wa mafuta nchini kwa kutumia mfumo wa uagiziaji wa pamoja.

Utekelezaji. Agizo limetekelezwa na wizara kupitia *ZURA* ambapo zabuni ya kwanza ilitolewa mwezi wa Julai, 2017 na Kampuni ya *Augusta Energy* ya Uswisi ilishinda zabuni kwa ajili ya kuagiza na kuingiza mafuta nchini kwa mwezi wa Septemba na Oktoba.

Agizo la 21. Kamati inaomba wizara husika pamoja na serikali kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya mafuta ikiwemo bandari na bohari ya mafuta hapa nchini.

Utekelezaji. Agizo limepokelewa ambapo serikali itatekeleza dhamira ya ujenzi wa miundombinu ya mafuta ikiwemo Bandari na Bohari ya mafuta hapa nchini. Ujenzi huo umetengewa eneo la Mangapwani ambalo limetangazwa katika Gazeti la Serikali Nam. 54 ya mwaka 2017 kuwa ni eneo maalum lilotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa shughuli za mafuta na gesi.

Agizo la 22. Kamati inaomba wizara kuzifanyia mapitio sheria zote za sekta zinazodhibitiwa na mamlaka hii ili ziende sambamba na majukumu ya *ZURA* yaliyopangiwa kwa mujibu wa Sheria husika.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati, Wizara kupitia *ZURA* kwa Mwaka 2017/2018 itabainisha Mamlaka ya *ZURA* kwa mujibu ya sheria yake na kuzitaka taasisi zinazodhibitiwa (*ZAWA* na *ZECO*) *ZURA* ili ziende sambamba na mipaka ya kisheria.

Agizo la 23. Kamati inaitaka wizara iipatie *ZURA* eneo la ujenzi wa afisi zake za kudumu, ili kupunguza gharama wanazoendelea kulipia kutokana na kodi ya pango.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Wizara ilizingatia agizo la kamati na tayari *ZURA* imeshakabidhiwa hati ya umiliki wa eneo la ujenzi za ofisi katika eneo la Maisara.

Agizo la 24. Kamati inaomba serikali kuanzisha utaratibu wa kuweka *"reserve tank"* ya mafuta ili iweze kutumika wakati wa dharura.

Utekelezaji. Wizara imepokea agizo hilo na kwa kushirikiana na taasisi ya *ZURA* ambapo utaratibu huo wa kua na *"reserve tank*" umeingizwa katika mpango wa matumizi wa eneo la Mangapwani.

Agizo la 25. Kamati inaiomba serikali kupitia wizara kuwa na taasisi moja tu inayoshughulikia masuala ya uchakachuaji na ukusanyaji wa mapato ya mafuta.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Kabla sijaongea utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kufanya marekebisho katika swali hili kwa kuwa wakati tumekaa na kamati swali hili lilikuwa utekelezaji wake bado haujafanyika, lakini sasa hivi utekelezaji wake tayari umefanyika hivyo naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Baada ya kukaa na kupitia Sheria ya *ZURA* na Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) na tumeona kuna mgongano wa sheria kwa *ZRB* wana mamlaka ndani ya sheria ya kusimamia shughuli hii. Hivyo, taasisi hizi mbili zimekubaliana kazi hiyo ya usimamizi itakuwa chini ya Mamlaka ya Uthibibiti *ZURA*.

Agizo la 26. Kamati inaiomba Wizara kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la Wakurugenzi wawili kujibana katika Ofisi moja hali ivyopelekea kukosekana kwa usiri wa utendaji wa kazi.

Utekelezaji. Kwa ajili ya kupata Ofisi ya Kudumu ya Sekta ya Mazingira ambayo inajumuisha Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tarehe 28 Julai, 2017 imeiandikia barua Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Ombi la kupatiwa nafasi iliopo jirani na Ofisi za Mazingira kwa ajili ya utanuzi wa Ofisi za Mazingira.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niliengezee jibu hili kwamba wizara sasa hivi inahamisha kitengo kimoja katika jengo lile na kupeleka ofisi zilizokuwa Idara ya Nishati

kwa maana Idara ya Nishati itahamia katika jengo jipya hili lilokuwa la PBZ ambalo maswali ya uchimbaji wa mafuta asili watakuwa juu na wao watakuwa pale chini. *(Makofi)*

Agizo la 27. Kamati, inaiomba wizara kwa kushirikiana na Mamlaka pamoja na Idara kuhakikisha inaanzisha mradi wa kuhifadhi maji machafu, ili kuliokoa eneo la Maruhubi linalotumiwa na waanika wa madagaa na kuokoa mazingira ya eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika Utekelezaji. Kupitia Mradi wa Huduma wa Miji Zanzibar *(Zanzibar Urban Support Project – ZUSP)* kutajengwa sehemu ya kusafisha maji machafu yanayotapishwa kwenye vyoo na makaro. Sehemu hiyo itajengwa katika eneo la Kibele na itatumika kwa ajili ya kusafisha maji machafu yanayotapishwa kutoka kwenye vyoo na makaro ambayo hivi sasa yanatupwa Maruhubi.

Tathmini ya Athari za Kimazingira *''Environmental Impact Assessment '' (EIA)* juu ya ujenzi wa sehemu ya kusafisha maji machafu na jaa la Kipele imeshafanyika. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi wa Septemba, 2017, ramani za ujenzi wa jaa na sehemu ya kusafisha maji hayo na gharama husika za ujenzi huo zipo katika hatua za mwisho za matayarisho. Ujenzi unategemewa kuanza rasmi mwezi wa Machi, 2018 na kumalizika baada ya miezi 15.

Mhe. Naibu Spika, agizo la 28. Kamati inashauri mamlaka ishirikiane kikamilifu na wamiliki wa mradi mkubwa wa uwekezaji wa Kampuni ya Bakhresa katika eneo la Mtoni, ili kuhakikisha kwamba ujenzi huo unazingatia suala la mazingira.

Utekelezaji wake. Tarehe 23/08/2017, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira iliandaa ziara ya wadau kutoka taasisi mbali mbali za serikali na wawakilishi wa Kampuni ya Bakhresa, kwa ajili ya kutembelea eneo la ghuba ya Mtoni, ili kuangalia athari ziliopo. Kufuatia ziara hiyo, tarehe 24/08/2017 kulifanyika kikao cha wadau cha kujadili na kukubaliana juu ya hatua zinazofaa kuchukuliwa za kukabiliana na athari hizo.

Taasisi zilizohudhuria ziara na kikao hicho ni Idara ya Mazingira, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, *ZIPA*, Kamisheni ya Ardhi, Wilaya ya Magharibi A samahani hapa kidogo Magharibi A siyo B, Baraza la Manispaa ya Magharibi A, Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, Shirika la Bandari, Sheha na Wawakilishi wa Shehia ya Mtoni na Uongozi wa Kampuni ya Bakhresa. Makubaliano ya kikao hicho yamesaidia kupatikana kwa mapendekezo ya ripoti hiyo ambayo tayari imeshawasilishwa serikalini na kuridhiwa mapendekezo yaliyomo kwa hatua za utekelezaji.

Lengo la mapendekezo hayo ni kuondoa kasoro na changamoto za kimazingira ziliopo kwenye eneo la ghuba ya Mtoni. Kwa kuwa, utekelezaji wa mapendekezo hayo unahusisha taasisi mbali mbali, hivyo ripoti hiyo imeshawasilishwa kwa taasisi husika kwa hatua za utekelezaji. Aidha, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira itaendelea na hatua za ufatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo haya.

Agizo Nam.29. Kamati inaitaka Mamlaka iandae safari za *field attachment* nchini Norway, ili kujiandaa kukabiliana na athari za kimazingira zitakazotokana na maendeleo ya mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira imefanya mazungumzo na mamlaka ya usimamizi wa mazingira ya Norway na kujenga mashirikiano ya usimamizi wa mazingira. Kufuatia mazungumzo hayo Serikali ya Norway imekubali kuisaidia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kupitia programu ya *Oil for Development* (*OfD*) ya nchi hiyo.

Kwenye programu hiyo Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar itapata fursa ya kujenga uwezo wa kusimamia masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kimazingira. Programu hiyo pamoja na mambo mengine itahusisha uandaaji wa miongozo ya kimazingira inayohusika na mafuta na gesi asilia, kujenga uwezo wa wafanyakazi na kutayarisha Mkakati wa Kimazingira wa Sekta ya Mafuta (*Strategic Enviromental Assessment- SEA*) kama Sheria ya Mafuta na Gesi ilivyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na uwasilishaji wa taarifa hii naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili kwa mashirikiano yao makubwa yanayowezesha wizara yangu kufanya kazi zake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, aidha wizara yangu inaahidi kuwa ipo tayari kupokea ushauri, maelekezo na kuyafanyia kazi ipasavyo kutoka kwa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano, Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Sasa anayefuatia ni Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2016/2017 kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili tikufu na kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2016/2017 kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kuweza kuwasilisha kwa mara ya kwanza utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kama Kanuni ya 108(15) inavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani zangu za pekee kwa Waheshimiwa Wajumbe na makatibu wa kamati yangu, ambao

tumeshirikiana kwa pamoja kuyapitia na kuyachambua Maagizo ya Utekelezaji kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu, kuthamini na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa kutekelezeka. Naomba sasa niwataje kwa majina Waheshimiwa Wajumbe na makatibu wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

1	Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2	Mhe. Suleiman Sarahan Said	Makamo Mwenyekiti
3	Mhe. Nassor Ali Salim	Mjumbe
4	Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	Mjumbe
5	Mhe. Said Omar said	Mjumbe
6	Mhe. Khadija Omar Kibano	Mjumbe
7	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
8	Mhe. Mohamedraza Hasanali MohamedAli	Mjumbe
9	Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu
1	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kwa idhini yako na ya Baraza nianze kuwasilisha utekelezaji wa Ripoti ya Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Ambapo jumla ya Maagizo 29 yaliagizwa na kamati hiyo kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, kamati inaipongeza wizara kwa kazi nzuri ya ufuatiliaji na utekelezaji wa maagizo hayo kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, kamati imetoa ushauri mbali mbali kwa baadhi ya utekelezaji wa maagizo ambayo bado hayajakamilika ipasavyo, miongoni mwa maagizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri serikali kwa kushirikiana na wizara husika kuwashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kikamilifu katika hatua ya awali ya uandaaji wa Sera ya Sheria yoyote inayotarajiwa kupitishwa. Kutokufanya hivyo kutapelekea kukosekana kwa baraka na michango ya Waheshimiwa Wajumbe katika utekelezaji wa sera hizo.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 4, kamati inaiomba pia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kukaa pamoja na Wizara Fedha na Mipango, ili kuweza kulitafutia ufumbuzi mbadala wa kifedha kwa ajili ya kulihami jengo la Mahakama ya Ardhi. Jengo ambalo linahatarisha maisha ya watendaji wa Mahakama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 8, katika utekelezaji wa agizo hilo kamati yangu baada ya kufanya ziara ya kimafunzo huko Tanzania Bara na kukutana na DAWASA. Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kufanya mageuzi ya Mamlaka ya Maji, ili kuweza kutoa fursa kwa Mamlaka kuwa na wakala atakayeshughulikia masuala yote ya miundombinu ya usambazaji wa maji kwenye mitaa kama ilivyo DAWASA, ili kuweza kuondosha matatizo ya maji hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati inaishauri Mamlaka ya Maji (*ZAWA*)kuanzisha Bodi ya Mamlaka ya Vianzio vya Maji katika Mikoa yote. Bodi ambayo kazi yake itakuwa ni kuvilinda vianzio vya maji mjini na vijijini, kwani imeonekana kuwa uvamizi wa vianzio vya maji ni moja ya sababu ya uhaba wa maji katika visima vya maji.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 12, kwa kuwa zoezi la upimaji wa vianzio vya maji na kuvipatia hatimiliki linaendelea, kamati inaiagiza Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kabla ya kuwasilisha bajeti ya 2018/2019 mbele ya Baraza hili, inaitaka mamlaka kuwasilisha ripoti kwa kamati kuhusu maeneo yote ya vianzio vya maji yaliopimwa na kupatiwa hatimiliki.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 15 kamati inashauri Shirika la Umeme (*ZECO*) kukaa pamoja na watendaji wa idara na kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi katika jitihada za kukamilisha upimaji wa vianzio vya umeme na kupatiwa hatimiliki baada ya taratibu kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 16 kamati inaishauri Idara ya Nishati na Madini kuzidisha kuwapatia elimu wafanyakazi wao, ili kuongeza wataalamu katika fani ya mafuta na gesi asilia kwa kuwa idadi ya wafanyakazi walioko masomoni bado ni ndogo sana na hairizishi.

Mhe. Naibu Spika, agizo Nam.17 kamati inaishauri serikali kuharakisha uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya *ZPRA*, ili iweze kurahisisha utendaji wa kazi zao kwa ujumla kama sheria inavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 20 kupelekea kutokea kwa mripuko katika moja ya viwanda vya mbao vilivyojengwa karibu na sheli ya mafuta, kamati inaagiza wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*) kufanya yafuatayo:-

Ukaguzi wa makusudi katika sheli zote za Zanzibar zilizojengwa kinyume na taratibu zilizowekwa na Sheria ya *ZURA* pamoja na Kanuni zake, ili kuepusha kutokea kwa athari za makusudi kama ilivyotokea katika Kituo cha Mafuta Gulioni.

Aidha, kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika kuanza ufungaji wa vituo vya mafuta vilivyokiuka taratibu za uanzishaji wa vituo hiyo. Vituo ambavyo vipo karibu ya maeneo ya biashara na shughuli za kijamii hali ambayo kupelekea athari kubwa kwa taifa pale ambapo janga linapotokea.

Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 22 kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), Shirika la Umeme (*ZECO*) kukaa pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*), ili kuweza kuandaa usimamizi imara katika huduma hizo zinazotolewa kwa wananchi, ili kuongeza pato la serikali.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu kwa naiba ya kamati pamoja na kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wa wizara hii tena kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza wa kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa kamati hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaanza na mchango na mchangiaji wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali na baadaye atafatia Mhe. Jaku Hashim Ayoub na ajitayarishe Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia ripoti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, nakupongeza kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo sasa tukizingatia kwamba wajibu wetu tuisaidie wizara na taasisi zake. Nazipongeza taasisi zote za wizara hizi kwa kazi nzuri wanazofanya hasa tukizingatia kwamba maji na umeme ni uhai na mambo mengineyo mabayo yanakidhi haja, ili tuishi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa na maswali kidogo baadhi ya maeneo, lakini nazungumzia Mamlaka ya Maji. Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na taarifa naikumbuka na kila wakati ninayo kwamba Zanzibar tulipata mkopo kutoka nchi ya India, mkopo huu una *US Dollar* 92 milioni, tukichukua fedha ya Tanzania tukiingia kwenye mahesabu tunakwenda karibu bilioni 200 zaidi. Je, nataka kujua tu huu umefikia wapi ili wananchi waelewe.

Mhe. Naibu Spika, nilisema fedha hizi kama zingepatikana katika Mkoa wa Mjini Magharibi tatizo la maji litabakia historia, wananchi watafaidika na maji kwa asilimia mia moja au mia mbili zaidi. Na nikatoa ushauri kama pana uwezekano zigaiwe kwa Zanzibar nzima Unguja na Pemba kila jimbo lipate bilioni moja tu. Bilioni moja basi tunatumia bilioni 54 Zanzibar yetu itakuwa historia hakutokuwa na tatizo la maji tena.

Mhe. Naibu Spika, lakini na usimamizi pia wizara kwa jitihada zake na mamlaka yetu ambayo inafanya kazi vizuri lakini na viongozi wa majimbo kama Wawakilishi na Wabunge washirikishwe, hapo ndio tutapata maendeleo. Hilo ni suala la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, la pili tuliambiwa kwamba katika taarifa hii wenzetu wamefanya juhudi kubwa za kutoa maeneo kuchangia au kutoa maoni, kwamba maagizo yaliyotoka ukurasa wa 3. Ukurasa huu wa 3 Mhe. Naibu Spika, unazungumzia agizo la 7, naomba ninukuu mheshimiwa.

> “Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) ifanye uhakiki wa kutosha na kukagua upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu yake na baadaye kutoa ripoti kwa wadau wote wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi”.

Mhe. Naibu Spika, ndio sisi hapa. Lakini utekelezaji wake, Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) imekuwa na utaratibu wa kukagua miundombinu ya maji, ili kupunguza upotevu wa maji. Aidha, *ZAWA* kwa kushirikiana na Mradi *JICA* imefanya juhudi za makusudi kuhakiki na kukagua upotevu wa maji katika maeneo ya Mjini Unguja.

Mhe. Naibu Spika, napongeza hili lakini bado kazi ya upotevu wa maji ipo sehemu kubwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo unaweza kutoa taarifa kwamba maji yanapotea unaomba wataalamu inaweza kufika wiki au wiki mbili hawapiti. Bahati nzuri wakati mwengine Mhe. Waziri yupo, mimi likitokea janga kama hili huwa namtafute yeye, lakini pia katika Mamlaka ya Maji wapo wazuri tu unapokwenda unapewa ushauri mzuri baada ya makelele ya hapa na pale tunakubalika sasa hivi na tunafahamika. Unapata kwa wengine ushauri mzuri sitaki kuwataja lakini wengi wao ni wazuri lakini wengine hawajielewi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ni shahidi katika haya kuna wakati napiga kelele mimi mpaka namtafuta yeye anapigiwa mfanyakazi simu anazima au hapokei, lakini anapopiga yeye Mhe. Waziri basi upesi upesi anapokea, anasema simu yako Mhe. Shihata sikuisikia mimi au sikuiona, hilo ni tatizo naliomba liondoke. Mhe. Naibu Spika, maji ni uhai na maji tunayategemea na maji ni rasilimali ambayo muhimu kwa mambo yote kama kilimo, binadamu, wanyama na mengineyo. Kwa hiyo, naiomba *ZAWA* kutokana na ushiriki wake wa kazi hizi waende vizuri ili tushirikiane. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika *ZAWA* kuna kisima sasa hivi kipya cha *Ras-el-Khaimah* kiko maduka saba Tomondo, kiko Jimbo la Kijitoupele. Lakini nataka maji yaende pande zote, yaende Kijitoupele, yende jimbo jengine lolote maji ni huduma na rizki ya Mwenyezi Mungu. Lakini kwa bahati mbaya maji haya yameelekezwa sehemu moja, na wakati hapo kisima cha zamani Tomondo na kisima hiki kinapeleka maji sehemu hiyo hiyo wanayopelekwa na haya mengine.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika naiomba wizara kupitia Mamlaka ya Maji mimi kama mwakilishi wa jimbo lile pamoja na viongozi wenzangu tufatane kuna eneo la maduka sita tokea ilipotengenezwa barabara yetu ile ya Melinne, yaani kutoka barabara ya Fuoni hadi Mwanakwerekwe mpaka leo Mhe. Naibu Spika maji hayapatikani na mabomba yote yameelekezwa katika mtiririko ule unaopatikana maji ya sehemu ya kwanza.

Hivyo naiomba *ZAWA* kwa makusudi hapa ndio pakusema na wananchi wamenileta hapa niwasemee, tuombe utaratibu wao wanaopanga ni mzuri, wameweka “T” au sijui kutakuwa na mambo yao ya utaalamu na mimi hii thuluthi, maana Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa Mikunguni nilikuwa matata sana, thuluthi zote za maeneo ya maji nazijua. Kwa hiyo, niombe sana *ZAWA* tushirikiane na huu upande unaokwenda kwa wenzetu ambao wanapata tabu maduka sita wapate maji, kisima hiki kielekee zote mbili kwa manufaa ya wote sio manufaa ya upande mmoja. Namuomba sana Mhe. Waziri tushirikiane kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa kuwa wenzetu kamati walifanya kazi nzuri hawatofika sehemu zote nataka kujua tu, tuliambiwa kwamba sehemu ya Kwarara Madina, yaani sehemu ya Kidutani juu kabisa kutajengwa *tank* kama la juu au la chini. Kwa sababu ni sehemu ya juu, lakini naja mafundi hao watakuwa ni Wachina wataalamu, hili limefikia wapi. Kama lipo namuomba Mhe. Waziri wananchi wapate jibu, kwa sababu maji ni kilio kikubwa katika jimbo langu na Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Magharibi 'B' na Magharibi 'A', lakini nitasemea mimi jimbo langu la Kijitoupele.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio makubwa kwa upande wangu niliyoona niseme kwa upande wa maji.

Kwa upande wa umeme Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na *ZECO*. *ZECO* Mhe. Naibu Spika, kama fedha wanazopata misaada Mamlaka ya Maji wangekuwa wanapata *ZECO* nafikiri tungeelea katika nchi hii kwa umeme, tungekuwa hatuna matatizo mpaka zile *train* za kwendea umeme zingekuwa zimeshatengenezwa kama zile Tanzania Bara wanazoziandaa. *(Makofi)*

Wenzetu wanafanya kazi nzuri na kwa juhudi, Mhe. Naibu Spika hata saa saba za usiku ikitokea dharura ukiwapigia simu watu wa *standby* wanaokuwepo kazini wanafika. Kwa hivyo, nawapongeza mimi kama Mwakilishi wa Kijitoupele lakini nawapongeza pia kuwa mwakilishi wa wananchi wote. Umeme ni jambo hatari na jambo muhimu linapokatika wakati wowote wenzetu wanafuatilia na wanafanya kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niipongeze wizara kupitia hii *ZECO* kwa muda wa miezi mitano baada ya kuwa tumo katika Baraza la Wawakilishi, Mhe. Waziri baada ya kukaa naye na kumuelekeza kwamba kuna tatizo la umeme kwa hao wenzetu wa huko Kwarara Madina hawajapata. Kwa kweli, leo kwa asilimia 95 umeme umekamilika na keshokutwa katika sherehe za mwenge unazinduliwa. Ombi langu tu hili naongeza nguvu, *transformer* walioiweka ni kubwa inafanya kazi vizuri, lakini kuna *transformer* pale Kwangulangwa ya zamani imezidiwa sana. Najua meneja ni mtu mzuri, hodari pamoja na mambo aliyokuwanayo ya hapa na pale lakini anafanya kazi nzuri. Hivyo, naiomba wizara kupitia *ZECO* tupatiwe *transformer* kwa ajili ya wananchi wa Kwangulangwa, ili tatizo la umeme liondoke kabisa katika jimbo langu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho niombe tena wenzetu kwa jumla wameweka kitengo kizuri hiki cha *ZURA*. *ZURA* naipongeza, *ZURA* ni suala ambalo linatuwekea mafuta kuwa yanapatikana kwa wakati na bila ya kukosekana. Hapa katikati nafikiri baada ya kikao chao cha hapa na pale walikuwa bado wanaweka mipango sawa yalipungua mafuta, lakini baada ya kupatikana mletaji wa mafuta moja kwa moja hili ni suala zuri ambalo litaondokana na adha ya bei kuwa huyu kapanga yake au kaona huyu anaonewa. Kwa hivyo, niiombe wizara kupitia *ZURA* waongeze bidii wafanye kazi zao kwa bidii ili maendeleo yapatikane.

Mwisho kabisa naipongeza ripoti hii, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa idara mbali mbali, *managers* wote pamoja na kamati kwa ripoti hii nzuri waliyoifuatilia. Baada ya hayo naunga mkono ripoti hii na hayo niliyoyaomba yafanyiwe kazi, ili wananchi wafaidike. Nisionekane adui katika kulitoa hili, lakini ni maelekezo ambayo yana manufaa kwa wananchi wetu. Naunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahmani Rahiim.* Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitachangia machache kwenye Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mambo ambayo yamo humu ndai na mengine nitayoyazungumza yatahusiana na ripoti hii kwa ujumla.

Kwanza ningependa kujua katika ukurasa nambari 3 agizo lililotolewa na kamati, kamati inaitaka wizara impatie eneo jengine mmiliki wa *FK Enterprises Company*, ili kupisha mradi mkubwa wa

uwekezaji. Ningependa kujua kampuni hii ni ya nani, inamilikiwa na nani na kwa nini wapatiwe eneo kuna tatizo gani lililotokezea.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna mambo machache ambayo nimeyaandika yanayohusiana na ripoti hii kwa ujumla. Ushauri wangu natoa, sisi Waheshimiwa Wajumbe nafikiri waliopita na sisi tuliokuwepo tutapatiwa ardhi ambazo kwa ufupi tutagaiwa na serikali. Lakini naomba Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein akawaona wananchi wote wanyonge wa Unguja na Pemba kuweza kuwapatia ardhi bure, ili waweze kujenga nyumba zao za makaazi na sisi kwa muda huu bora ardhi zetu tusipewe, wapewe wanyonge katika kila familia iliyokuwa haina uwezo, wapewe eneo hata la *square meter* 300, 400, ili wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wote waweze kupewa maeneo ya kujenga nyumba zao na sio muhimu sisi kwa sasa hivi. Mhe. Naibu Spika, ikibidi hivyo sisi tupewe tutashukuru si tatizo.

Lakini mwanzo tumuomba Mhe. Rais aangalie maeneo yaliyokuwa makubwa matupu waweze kukatiwa Wazanzibari kupewa maeneo hasa familia zile zilizokuwa hazina uwezo kila familia wakapewa kiwanja kimoja ambacho kitakuwa hakiwezi kuuzwa kwa mtu yeyote. Hicho kitakuwa ni mali yao kifamilia, kama ataamua mzee kumpa mtoto au mjukuu lakini itakuwa ni cha familia yake. Huo ni ushauri natoa kwa serikali.

Jambo jengine suala la maji Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Ali Suleiman Ali kasifu sana wizara ni jambo zuri. Lakini ninachotaka kusema tuzungumze ukweli maji bado Zanzibar ni tatizo tena kubwa. Kwa mfano, tukiangalia hapo mjini tu nyumba za Michenzani watu wanapata maji nafikiri kwa wiki mara moja, maeneo mengine jimboni kwangu mimi hakuna. Kinyasini nzima jimboni kwangu maji hakuna muda mrefu, Kikobweni tokea wakati kabla ya Mapinduzi maji hakuna, leo nikija kusema kwamba tatizo la maji wameliweza kuli-*solve* ni jambo ambalo si la kweli, isipokuwa wamejitahidi tu. Naishukuru serikali pamoja na Mhe Rais wangu wa Zanzibar anajitahidi, lakini bado kiukweli hatujafikia kiwango cha kujisifu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kujua tokea miaka kumi iliyopita mpaka hivi leo wizara imeshatumia shilingi ngapi kwenye miradi ya maji, na fedha hizo nataka zigawanyike kwa namna mbili, shilingi ngapi imetumia serikali fedha zake taslimu na shilingi ngapi imekopa pamoja na kudhaminiwa na nchi ambazo zimetoa pesa hizo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza Kinyasini Mhe. Naibu Waziri anajua, mimi nilitoleshwa fedha ya umeme nikalipa nikaamini kwamba nikilipa watatia mabomba na mambo mengine, lakini cha kushangaza hizo bomba wanataka watie Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge na hilo sio tatizo, kama wataahidi hapa nikifanya mimi thamani ile shilingi 13 milioni kuwa wananchi wa Jimbo la Chaani hawatolipishwa maji mpaka watakufa mimi niko tayari kugharamia.

Kwa kweli, suala la ku-*supply* miundombinu ni wajibu wa wizara sio wajibu wa mbunge wala mwakilishi. Sisi tuna haki kuchangia kwa wananchi kwa mambo mengine muhimu na hata ya maji, lakini sasa imefika wakati wizara inatupia mzigo kwenye waheshimiwa tu wa majimbo na mpaka hivi leo muda mrefu si Kinyasini wala Kikobweni hakuna maji. Mhe. Naibu Spika, naomba nije nipate jibu la busara kabisa, kwamba watafanya utafiti au maarifa gani kuweka umeme, bomba za maji Kinyasini Sokoni, Kisongoni na Kikobweni kwenye tangi la Mchina

lililochimbuliwa Ketwa kuletwa mpaka Kikobweni wananchi wakapata maji. Kazi ya ku-*supply* maji nitafanya mwenyewe lakini bomba kubwa za *connection* za maji wa-*connect* wao Mhe. Naibu Spika.

Jambo jengine suala la umeme. Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida kwenye wizara nakuwa sisifu kwa sababu ukimsifu mmoja wengine wataona choyo, lakini ninapozungumza haya kila yanayemgusa atajua nimemgusa nani. Suala la umeme, kwanza naweza nikatoa pongezi kwa watendaji wa chini, kwenye wizara zote watendaji wa chini ndio wanaofanya kazi sio viongozi baadhi yao wa juu, yaani wanaohangaika ni wafanyakazi wa chini ukiona wanasifika Shirika la Umeme ni wafanyakazi wa chini, ukiona Idara ya Maji ni wafanyakazi wa chini ndio wanaokwenda mbio na ukiona pia jimboni kunasifiwa sana watendaji wa chini madiwani na wengine ndio wanaotusaidia sisi, kwani kutwa tuko mjini kwenye vikao. Kwa kweli, watendaji wa chini maisha yote ndio wanaofanya kazi na wakubwa wanapata sifa, lakini sasa kama wale wa chini sio waaminifu na wakubwa wanapata jina baya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza kazi ya Shirika la Umeme ni kazi yao binafsi ku-*supply* miundombinu kote vijijini na mjini. Lakini leo cha kushangaza shirika lile linawatolesha watu kuanzia fedha ya yule dereva ambaye atatoka pale kwenye Shirika la Umeme mpaka atakokwenda, pesa ya nguzo, pesa ya *wire*, pesa ya *connector*, pesa ya kila kitu. Nimekuja na karatasi za jimboni karibu sita hizi za Shirika la Umeme, huwezi kuamini Mhe. Naibu Spika. Hivyo, mwananchi anataka kuungiwa umeme nguzo moja tu au mbili thamani yake hii hapa hakuna iliyokuwa chini ya shilingi mlioni moja na laki tano. Hivi kweli wanyonge hawa ambao mshahara wao wengine hata shilingi 300,000 haufiki, tushukuru wa serikalini waliopandishiwa shilingi 300,000/=, sasa ukamwambie alipe shilingi 1,800,000/= wakati Shirika la Umeme wao ndio wanaofaidika.

Mhe. Naibu Spika, nchi za wenzetu zote duniani wanapeleka umeme mpaka eneo husika bure na nchi nyengine za kitajiri wanakutilia mpaka TUKUZA ndani ya nyumba, bure hulipi shilingi. Sasa wao wanachofaidika utaponunua ndio wanapata ile faida, lakini nathubutu kusema Shirika la Umeme naweza kusema wanatapeli wananchi na kwa ufupi ni utapeli kazi yao ni kufanya kazi zote sio kwenda kutolesha wananchi wanyonge pesa nyingi kama hizi. Kwa kweli, ninazo karatasi za jimboni nimeshaletewa zaidi ya shilingi 40 milioni, kama na hili wataniahidi nikilifanya mimi umeme utakuwa bura kwa wananchi wangu nitalipa mimi hizi hapa. Lakini wasitumie utapeli wa kuwalipisha wananchi mpaka fedha za magari, fedha za posho za madereva halafu leo umeme wanawauzia, umeme wa shilingi 10,000/= Zanzibar unakatwa kodi karibu shilingi 3,500. Hivi kwa kweli tunawaumiza wananchi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimesimama hapa kutetea wananchi na ndio walionichagua, naipenda serikali, nchi, nampenda Rais wangu pamoja na chama changu, lakini kwenye masuala kama haya siyanyamazii. Ninachoomba kwamba Shirika la Umeme kazi yao wafikirie kwamba wapeleke miundombinu yote bure kwa wananchi na yule atayetaka kuingiza katika nyumba yake ndio wamlipishe gharama ya TUKUZA au *wire*. Lakini, leo anataka kutoa nguzo barabarani analipishwa kuanzia nguzo zote na *wire* na vitu vyote. Suala linasikitisha na mimi vitu kama hivi nakuwa sivisifu kabisa kwa sababu haviko sawa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni la ardhi. Wizara hii nzito mimi wala simuonei mtu wala sitaki kumsema mtu, nafahamu kwamba uwaziri na unaibu waziri mzito na majukumu haya hata mimi katika maisha yangu siyaombi. Kwa kweli, katika moja ya vitu *headache* ni hivi, vina majukumu makubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ardhi Zanzibar wanyonge wengi hawana hatimiliki kwenye nyumba zao. Mimi ningeshauri wizara ingewatolea hatimiliki wanyonge wote bure bila ya kuwataka kuwalipisha fidia kubwa kubwa na badala yake wafanyabiashara wakubwa ambao wana-*invest* kwenye mahoteli na -*real-estate* ndio waweze kuwalipisha kwenye masuala ya hatimiliki. Lakini wale wanyonge hatimiliki wafanyiwe bure waweze kuwa na hatimiliki zao kwenye nyumba zao. Sambamba na hilo, ninachotaka kutahadharisha kwenye wizara hii kuna watendaji ambao wamo ndani ya Wizara ya Ardhi wanashirikiana na wafanyabiashara, wanashirikiana na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, jana nilitoa mfano Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mkunduchi anachukua maeneo anajenga kibanda maeneo ya watu anajitoa fahamu, ana watu kwenye Shirika la Ardhi anawachukua kwenda kupima kiholela Makunduchi na sehemu nyenginezo, kachukua maeneo ya watu mengi kutumia *power* yake ya uheshimiwa pamoja na wafanyakazi wake wizarani wamo. Kwa kweli, suala hili juzi Mkuu wa Wilaya ya Kusini nilimsifu kwa sababu kaweza kufuta hati zile, kazikataa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, naomba sana Wizara Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira hii wale wanaoshirikiana kutapeli watu wawafukuze na haina haja ya kuwaweka. Mhe. Naibu Spika, kazi yao kuna baadhi ya Waheshimiwa wanatumia watendaji kwenda kutapeli wananchi wa hali ya chini, na hili suala hatuwezi kulinyamazia.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine naomba kujua hadi hivi leo kuna ardhi ngapi za *investment*, ambazo hazijafanyiwa mambo ya maendelezo. Kwa mfano, maeneo ya baharini maeneo mangapi ya baharini hadi hivi leo hayajafanyiwa *any investment* ndani yamekaa tu watu wameyamiliki. Maeneo haya mengi ukiangalia yanamilikiwa na watu wakubwa, lakini leo kwenye masuala kama haya wananchi wa chini waliokuwa wanyonge watakuja kusemwa mbio mbio hapa. Kwa hivyo, tunataka kujua maeneo yanayomilikiwa na watu wakubwa mangapi, ambayo hayajafanyiwa *any investment* hadi hivi leo na wale waliokusudiwa kunyang'anywa ni wepi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba kulizungumza suala la umeme. Hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi lini itategemea umeme kutoka Tanzania Bara. Kwa kweli, ni vizuri ndugu tena Muungano, lakini tuliona ilivyoharibika *cable* watu miezi minne hapa hakuna umeme watu wanatumia majenereta waliokuwa matajiri, waliokuwa masikini wamekaa na vibatali vyao. Hivyo, ni lini serikali itaweza kutafuta miundombinu ya umeme wao wenyewe ndani ya Unguja na Pemba, ili kuweza kuleta uchumi zaidi wa mambo ya biashara na vitegauchumi tukawa nao wenyewe na bei ikapungua. Mhe. Naibu Spika, walizungumza kwamba bei wanaolipishwa wao ni sawa sawa na bei wanayouziwa watu *retail* wakati wao wananunua umeme ni *whole sale*. Sasa nataka tujue hadi hivi leo serikali imeshakaa na makampuni mengine kutafuta njia mbadala za kumiliki umeme wetu wenyewe Zanzibar au bado tunategemea umeme wa *TANESCO*, siku wataoamua kutuzimia tunazimiwa na siku itakayoharibika *pipeline* ile inakuwa umeme hatuna. Tunataka tujue wamefikia hatua gani hadi hivi leo.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri *time* yangu ya kuchangia mambo ya wizara hii yako mengi, lakini napenda kufahamu kwamba agizo jengine lilitolewa na kamati kuhusu *ZECO* hii. Mimi ndio maana ripoti nakuwa sipendi kuzisoma kwa sababu *headache,* ndio maana nachukua *point* nazisema mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, haya niliyoyazungumza napenda sana nije nijibiwe tuyafahamu na tuangalie wamejipanga vipi wizara kuhusu watu wanyonge kuweza kuwasaidia, hasa kwenye masuala ya ardhi niliyoyazungumza, masuala ya umeme na masuala ya maji. Kwa kweli, hapa tusiseme uongo bwana hatujafika popote kwenye masuala ya maji na umeme, bado tuna kazi ya kutosha tunatakiwa tuifanye.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf muda umekwisha na hayo uliyoyazungumza wameshasikiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru mimi nangojea majibu yangu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, narudia tena niliyoyasema jana na juzi, tunajadili utekelezaji wa maagizo, waziri hana jukumu la kujibu lile ambalo halimo humu. Haya mengine yatakuja baadaye. Kwa hiyo, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf umetaka majibu, lakini nakwambia hayo ndio maelekezo tunayoelekezwa na Kanuni yetu, kwamba tunachangia maagizo sawa. Kwa hiyo, mengine yatakuja kuna muda wake utajibiwa yote hayo, lakini kwa sasa hivi utajibiwa yale ambayo yanahusiana na maagizo ambayo yametolewa na utekelezaji wake.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kutumia busara zako za kuwabeba wizara mara kwa mara. Hii ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inahusiana na mambo yote niliyozungumza mimi, maji nimezungumza inahusiana na wizara hii, umeme pia, tukingojea huko hii ripoti imewabeba sana haina maana yoyote humu ndani. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Lakini ripoti hii siikubali mpaka nijibiwe masuala yangu, wakinijibu nimeikubali hawakunijibu siikubali. Huo ndio uwazi wangu mimi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kukushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi na mimi ili niweze kutoa mchango wangu katika ripoti hii ambayo ni muhimu kwa maslahi ya wananchi wetu Wazanzibari wote juu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi.

Pia nimpongeze rafiki yangu, kaka yangu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil maarufu kwa jinsi alivyoisoma ripoti yake ikiwa ni tofauti na wengi ambao tumekuwa tunapata mazoea, alisoma kwa upole na kila neno ulikuwa unalisikia. *(Makofi)*

Lakini nimpongeze na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pia dada yangu Mhe. Salama Aboud, kwa jinsi ukiangalia ripoti ina taarifa nyingi, lakini alikwenda bila ya kunywa maji, alisoma kwa haraka huku Mhe. Naibu Waziri wake alikuwa anamshanga jinsi waziri wake anavyosoma, naamini na yeye pia alikuwa anajifunza. *(Makofi)*

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, na mimi niende kwenye maagizo yote ambayo yalichangiwa kwenye ripoti hii. Nianze na agizo namba 4. Mhe. Naibu Spika, kwenye agizo nambari 4 nimeangalia juu ya kamati inaiomba serikali pamoja na wizara juu ya Mahakama ya Ardhi kuhusiana na masuala ya jengo.

Lakini niseme tu kwamba nashauri wizara kutokana na jengo ambalo lililokuwepo la Kamisheni ya Ardhi, pale pembeni ya Benki ya *PBZ* ya zamani Ngome Kongwe, kwa jinsi ya matumizi na watu wanavyohitaji kwenda kuonana na kupata zile huduma, basi utaratibu uanze kwa mwaka wa fedha, ikiwezekana tupate jengo ambalo litakuwa nje ya mji, kwa sababu jinsi ya magari yanavyoingia katika Jimbo la Malindi au Mji Mkongwe, basi mazingira ya watu kupata ile huduma au wanachokifuata wanahitaji kuwa na nafasi ya kutosha kuweka magari yao. Kwa hivyo, naamini jengo lile linaweza kutumika kwa matumizi mengine juu ya wizara husika au wizara nyengine na serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwenye agizo namba 7, pia lilizungumziwa suala la maji. Ningependa nifahamu zaidi na ningefurahi kama kamati husika ingekuwa imefanya kazi nzuri ya kutuletea hasa kuhusiana na *pump* ambazo zilizoletwa na Kampuni ya *Ras-el-Khaimah* na kuichangia katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, juu ya mpango mzima wa kuongeza huduma ya maji. Hizi *pump* zimekwenda wapi, zimetumika wapi jamani mbona hatuoni hayo mambo ambayo yanazungumzwa na *ZAWA*, ili tukaona unafuu. Tunasikia zinaungua na tunasikia nyengine zimetoweka ndani ya *ZAWA*, lakini zimepelekwa wapi.

Mhe. Naibu Spika, agizo jengine lilikuwa agizo namba 16. Mhe. Naibu Spika, kwenye agizo namba 16 wizara imezungumzia suala zima juu ya elimu katika kujitayarisha kwenye masuala mazima ya fani ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa angalizo na moja yao ni kuhakikisha kwamba pale nafasi zinapotaka kutokezea kwa ajili ya vijana wetu kwenda kusoma, basi elimu hii wasipewe watoto wa wakubwa, wasipewe watoto wenye majina makubwa peke yao, lakini pia watoto wa maskini na watoto wenye vipaji pia katika jamii yetu kwa Unguja na Pemba, basi na wao pia wapelekwe kwenda kusoma, ili tulete mwamko mzuri kwa wananchi wetu, pawe na *transparent* na uelewa mzuri kwa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeishauri kamati wangepata kujua hawa watoto waliokwenda kusoma mpaka sasa hivi vijana wetu, basi tuhakikishe kwamba wakiingia huko mitaani katika kufanya kazi zao za kamati, basi uhakikishe na wao pia wanapata kujua na wanaipa kipaumbele, ili kuhakikisha kwamba vijana wote wanaokwenda kusoma basi wanakuwa wote wenye rika tofauti na hakuna ubaguzi unaofanyika katika eneo lote. *(Makofi)*

Vile vile, naomba kushauri pia jambo ambalo nimekuwa naliona mara nyingi ndani ya watendaji wetu katika serikali, ambapo pengine wao hawana fani kubwa juu ya mafuta na gesi au utundu

ambao watu wengine hujitokeza kujifundisha moja kwa moja. Kwa hivyo, ninashauri kwamba watendaji ndani ya serikali wafanyiwe japo kozi ndogo ndogo, hata ambao waliokuwa hawapo ndani ya wizara husika, lakini wizara ambazo watakuwa wanagusana ili kujenga uelewa mzuri juu ya masuala ya mafuta na gesi.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine wanapata mshangao mkubwa sana, unamkuta mtendaji mkubwa ndani ya serikali anang'angania kwamba *block* namba fulani lina mafuta na gesi, ukimuuliza hayo mafuta umejuaje, anakuambia yapo tu nimesikia, sasa inakuwa haipendezi. Ukimuona mtendaji mkuu ndani ya serikali anang'angania suala la kwamba sehemu fulani kuna mafuta na gesi, wakati tangu historia ya nchi hii, tangu tumetoka 1958 mpaka leo 2017 unakuta kuna *block* hazijawahi hata mara moja kupelekewa *pipe* chini, isipokuwa tu katika kutumia utaalamu wa karibuni kama mfano wa *seismic* unaonesha kwamba inawezekana *blocks* kadhaa au *block* hii au hii kuna mtazamo mzuri ambao unaonesha.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, ni vizuri watendaji wetu wanapozungumza wakawa na uhakika, sisi wengine humu ndani wajumbe wa Baraza tulipata nafasi tukafanyiwa *coaching* na aliyekuwa Mkurugenzi mstaafu wa *TPDC* Dk. Yonnar Kilagani. Nakumbuka siku ile wajumbe 12 tulikuwepo na nimpongeze mjumbe peke yake kutoka kwa mawaziri na manaibu mawaziri alikuwa Mhe. Mohammed Ahmada Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji alikuwepo na alishiriki kwa ukamilifu, naamini alifaidika na yale maelezo na elimu tuliyopata siku ile au msasa tuliopigwa na Mkurugenzi yule. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine nataka niliangalie ni agizo namba 20, ambalo linazungumzia suala zima juu ya mpango mpya ambao unaotumika sasa na wizara husika, kwa kupitia taasisi yake ya *ZURA*, ambayo ni *Zanzibar Utility Regulation Authority* juu ya kuhakikisha kwamba mafuta yanapoletwa Zanzibar sasa yatafanyiwa *build* kwa kampuni moja.

Mhe. Naibu Spika, nishauri na niwaombe kamati husika. Tunajua mara hii kampuni iliyoshinda *builds* ni *Augusta* kampuni ya kutoka Switzerland. Nishauri kwamba tuhakikishe kuwa *builds* zinapofanyika basi iwe kuna *transparency*, pawe pana *open* kwa kila kitu, pasiwe na harufu ya aina ya rushwa ambapo wananchi au sisi tukaanza kuona Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tukiwa kama wasemaji na watetezi wa wananchi, kwa sababu haipendezi kabisa kuona huduma ambayo hii nishati ni muhimu kwa wananchi basi inakuwa kazi inapokwenda sio sahihi.

Lakini niseme tu pia tunatambua kuna changamoto juu ya mpango mzima wa *BPS* ambao ni *Bulk Procurement System*, kwamba nchi nyingi au mazowea yanaonesha kwamba pale ambapo unataka kuanzisha mfumo kama huu wa *BPS*, basi mara nyingi serikali huwa ina sehemu ya *depot* yake, au *reserve system* yake na pale kama panatokea uchelewaji basi serikali huingilia katikati.

Kwa hivyo, nishauri kwamba wizara husika na viongozi wote ambao wako juu wananisikiliza basi hawakikishe kwamba mpango wowote watakaoufanya hakuna siku au saa Zanzibar wafanyabiashara na wananchi watakosa hii nishati. Lakini hapo hapo nitoe masikitiko yangu kwa kamati ambayo inahusika na wizara hii, wakati leo wanasoma ripoti sikuona eneo hata moja waliozungumza kwamba wameonana na makampuni ambayo yana- *supply* mafuta au yanauza mafuta ya taa *petrol* na *diesel* juu ya mpango huu, ili na wao tungepata kuwasikia maoni yao

ambayo walioyatoa, kwa sababu mfumo huu ni mpya basi ingekuwa ni vizuri kamati ingekuwa imewasilisha na tukapata kuona sisi kama wajumbe mpango huu.

Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika, makampuni sasa hivi haya baada ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kutangaza agizo lake juu ya viwango vipya vya kazi, kuna changamoto tayari imejitokeza katika Makampuni ya Mafuta na gesi. Kwa mfano, *Zanzibar Petroleum* wanao wafanyakazi 210, *United Petroleum* wanao wafanyakazi 240, *GAPCO* wanawafanyakazi 130.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kwa taarifa nilizokuwanazo wameshawasilisha barua rasmi kwa taasisi ambayo inasimamia ambayo ni taasisi ya *ZURA*, ili wanaomba maombi yao waongeze bei ya mafuta na gesi katika kuuza rejareja kwa shilingi 40 kutokana na mabadiliko ya kiwango kipya cha mishahara. Hili ni kama awali nilivyosema viwango vile ni kama mnyororo, utaendelea kutula sisi kidogo kidogo, kwa sababu siamini mchakato ule ulivyopangwa na waziri wa kazi ulikuwa umewashirikisha wadau wote, na nitaamini kila wizara husika nitakuwa naona na ninagusia maeneo ambayo yapo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri inabidi nikushauri uwahi kwa haraka ili sasa wananchi wapate kuelewa shilingi 40 ni pesa nyingi sana katika kuongeza tozo hii kwa ajili ya waanchi.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe pia Mhe. Waziri katika uchimbaji wa mafuta na hii sheria namba 6 ya mwaka 2016, mimi bado naamini makampuni yote haya mengi ambayo ni ya kimataifa ambayo yana uwezo wa kuchimba mafuta katika hizi *off shore drilling* kina *Axon Mobil, Shell* pamoja na wengineo, *Tat Oil*. Wengi wao sasa hivi wameanza kuhama Dar-es-Salaam kulikoni, kuna nini. Lakini tukisoma ile sheria yetu wengi tuliochagia siku ile tulitoa hofu kwamba haya makampuni ya kimataifa pale panapotokezea matatizo, *arbitration* yao wanakuwa wanapata tabu na uwoga kuelekea Vuga, na mara nyingi hawa huwenda katika *International Business Court* za Biashara ambazo ziko Paris na London.

Sasa mimi nikuombe Mhe. Waziri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja kutuona pale Kibandamaiti, alisema anataka mafuta na gesi Zanzibar yaanze kuchimbwa haraka sana. Lakini hadi leo ni mwaka tunapita sasa hatujaona makampuni au magari makubwa kutembea hapa mjini. Je, kama kuna mapungufu yoyote katika ile sheria yetu basi tuleteeni tufanye marekebisho, ili muende sambamba. Lakini pia kama kuna kamati ya wataalamu inahitajika kuundwa, kwa sababu sisi bado ni wapya tunajifunza katika sekta hii ya mafuta na gesi asilia, basi tuangalie ile sheria yetu kwenye mapungufu tuletewe turekebishe kwa sababu wananchi wetu wana matumaini.

Mhe. Naibu Spika, juzi mzee mmoja alinisimamisha akaniambia tuhakikishe kwamba Chama cha Mapinduzi pamoja na serikali yetu na wizara husika, wahakikishe kwamba tunapokwenda mwaka 2020 tayari mchakato wote wa suala la gesi na mafuta tumeanza. Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo niombe tu Mhe. Waziri na kamati husika katika kazi zao na kutimiza majukumu yao basi niombe kamati, mwenyekiti, makamu mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wapite katika viwanja vya maeneo ya Tunguu, ili kunipunguzia manung'uniko kero na maneno ambayo natupiwa mimi, hasa katika matatizo ya viwanja ambapo na migogoro inaanza kujitokeza na wasaidiane na wizara husika, ili na sisi twende sambamba na wale

wananchi waliokuwa wakiishi kule wapate kufaidika na viwanja hivi, pamoja na wale wote ambao serikali inakusudia kuwapa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe pamoja na kamati na Mhe. Waziri kwa ripoti nzuri. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu pamoja na mimi mwenyewe naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya mia. Nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Anayefuata ni Mhe. Sulaiman Makame Ali, na ajitayarishe Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Ripoti hii ya Utekelezaji wa Kamati au Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 2, kuhusu masuala ya migogoro ya ardhi. Mhe. Naibu Spika, hapa kamati iliomba Kamisheni ya Ardhi ifanye utafiti kwenye masuala haya ya migogoro ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kitu kiuhakika. Naomba uniruhusu kuinukuu barua hii niliyoletewa na wananchi wangu wa Ndagoni, kuhusu mgogoro wa ardhi, kuhusu malalamiko ya ardhi Mwambamkuu, Javini Ndagoni. Mhe. Naibu Spika, hata Mhe. Naibu Waziri nilimuuliza hapa. Je, uko tayari kufuatana na mimi twende Ndagoni kwenye suala la mgogoro wa ardhi, akanijibu sawa, lakini sikumuona mpaka hivi sasa. Sasa cha kushangaza Mhe. Naibu Spika, mimi nilimwambia Mhe. Naibu Waziri au mpaka watu wapigane mapanga, wakishapigana mapanga halafu tena iwe kupelekana polisi watu wameshauwana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Naibu Waziri na wizara yake yote pamoja na Afisa Mdhamini kama yupo, basi wahakikishe suala hili kule Ndagoni linapatiwa ufumbuzi na sehemu nyengine, kwa sababu lengo ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na hata Mhe. Rais wa Zanzibar kila siku analipigia kelele suala hili la migogoro ya ardhi, kwa sababu iko kijijini kwetu, iko majimboni kwetu, iko mawilayani kwetu na iko mikoani mwetu.

Lakini migogoro hii ya ardhi Mhe. Naibu Spika, inasababishwa na baadhi ya watendaji waliomo ndani ya wizara ile husika, kwa sababu sio kweli kwamba yeye mtu aliyekuwepo kwenye masuala ya ardhi hawezi kujua kanuni na sheria akaweza kuwaondoa wale kiutaratibu, akawafahamisha kwamba twendeni. Lakini yeye siku nyengine hudanganya wakati wakikataa au wakapewa samaki wa changu tena ndio ukaona ule mgogoro anauendeleza, kwa sababu huwa hakereki kutokana na kwamba wale wakipigana si wao wenyewe wa kijiji kimoja wameshapigana huko ni ndugu. Kwa hivyo, sivyo.

Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Naibu Waziri nakuomba tena barua hii hapa na ushahidi huu na nikakuletea na saini zao wamezitia na namba zao za simu kijiji kizima wameniandikia barua kuniomba niende mimi pale. Sasa mimi nikasema sawa nikenda, lakini lazima niwapate watu wa ardhi ili kwenda kulimaliza tatizo hili. Kwa hivyo, nakuomba tena Mhe. Naibu Waziri, suala hili la migogoro ya ardhi Ndagoni nisilisikie. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la Mamlaka ya Maji. Mhe. Naibu Spika, kamati inaomba Mamlaka ya Maji *ZAWA* ifanye uhakiki wa kutosha kukagua upotevu wa maji. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli serikali inajitahidi sana na kila siku tunapiga kelele kuhusu masuala ya maji, lakini kuna watu wanajitoa mishipa ya fahamu wanafanya makusudi. Leo mtu anaunga maji, maji kwake yanapotea kule mbele kwa mwenzake hayafiki halafu serikali inalaumiwa. Hivyo ni vyema, Mhe. Naibu Spika washirikiane na Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri na wizara yote kwa jumla washirikiane na masheha, yeyote yule ambaye anapoteza maji kiholela ili serikali ilaumiwe basi afungiwe kwa sababu yeye hayataki.

Mhe. Naibu Spika, leo utamkuta mtu amejiungia maji lakini kule kwake yanapotea *pipes* zile ni mbovu hafanyi utaratibu hata wa kumwita fundi, hata kupeleka ushauri wowote hapeleki kwa sababu kwake yanafika. Kwa hivyo, naomba sana kamati hii naishukuru kwa kuliona hili, kwa sababu lipo ndani ya mitaa mingi ukifika utakuta maji yanapotea utafikiria kumenyesha mvua ile ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana suala hili la upotevu wa maji, kwa sababu pia itakuwa tumeibebesha serikali mzigo, kule mashine inafanyakazi kwa jitihada ya kujisukuma na huku maji yanapotea kwa wananchi hayafiki. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naliomba sana suala hili.

Vile vile, kamati imetaka kwamba watu wa Mamlaka ya Maji wahusika washirikiane na viongozi wa majimbo. Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana viongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba, chini ya Mkurugenzi wake na Afisa Mdhamini Pemba, kwa kushirikiana na mimi kuhakikisha tunaliondoa tatizo la maji lililokuwa limewakumba wananchi wa Ndagoni, mpaka wale Polisi wetu wanaolinda umeme kule.

Mhe. Naibu Spika, kusema kweli mradi ule wa maji gangi lililoko Gombani ambalo lilitakikana maji yale yapelekwe Shehia ya Ndagoni, Wesha na sehemu nyengine. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli mradi ule ume-*fail* maji yale hayatoki na hivi sasa mimi imeniwajibikia kwamba kila shehia nianze tena kufanya kisima kama kisima cha Ndagoni. Kwa hivyo, naomba sana Mamlaka ya Maji na wizara husika basi wahakikishe wanafanya utaratibu mwengine mbadala wa kuweza kuhakikisha kwamba yale maji wale wananchi wa Shehia ya Wesha, Birikau, Tondooni na Kijagwani waweze kuyapata, kwa sababu ule mradi ulikuwa ni wa sehemu tatu, vijiji visivyopungua kama 15.

Lakini sasa hivi hawayapati maji yale, hayafiki vizuri na watu kila siku hawalali, kwa sababu kulala mtu anakwenda shamba akirudi keshachoka na suala la maji ni muhimu sana, aweke jembe kipembeni achukuwe ndoo aende akachote maji. Nawasikitikia sana wananchi wangu wa sehemu ya Wesha na sehemu nyengine hawapati maji vizuri, kutokana na tatizo la kwamba mradi ule ume-*fail*, ni lazima tuseme ukweli pesa zilizotumika pale ni nyingi, maji hayafiki na tangi lilopo pale hata sisi sote tumiingia mule kwenye tangi hatuonekani, lakini maji hayafiki, sababu ni nini.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, suala hili Mamlaka ya Maji pamoja na wizara husika waliangalie vizuri. Tumetoka kwenye masuala ya kuchimba visima kila sehemu, tumefanya miradi ambayo inajumuisha shehia kama tatu au nne, lakini sasa tunarudi tena kule

kule kuanzisha visima vingine. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana suala hili Mhe. Waziri ananisikia yupo, alichukuwe na alifanyie kazi, ili ahakikishe kwamba ule mradi uliowekwa kule Gombani wananchi wangu wa Shehia ya Wesha na sehemu nyengine wanaopata maji yale yafike kama yalivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia 50 na asilimia 50 nzima nazitoa mpaka atakaponipa majibu yangu Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Omar Seif Abeid, baadaya ya hapo atakuja Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo kwenye hotuba hii ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze mbele nirudi nyuma. Naomba tuangalie agizo la 25 katika ukurasa wa 8 na 9, jibu limekuja hapa. Inaonekana kwamba maagizo ya kamati imeona kuna tatizo. Kamati inaiomba serikali kwa kupitia wizara kuwa na taasisi moja tu itakayoshughulikia masuala ya uchakachuaji na ukusanyaji wa mapato. Jibu la utekelezaji likaja kwamba, baada ya kupitia sheria ya *ZURA*, Bodi ya Mapato ya Zanzibar *ZRB* na kuona ni maeneo gani yanayogongana kisheria ambayo yanaingiliana mamlaka kati ya *ZURA* na *ZRB*, kwani nani mwenye haki ya kukusanya mapato yanayotokana na hayo mafuta.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuishauri serikali kwamba ni vyema na ni busara zaidi kama kamati ilivyoagiza kuwa na kituo chetu chetu kimoja, kuwa na mtu mmoja ambaye tunampa mamlaka ya kisheria kukosa kuwa na taasisi moja tunayoipa mamlaka ndio kunakosababisha kuwa na hii migongano kila mmoja akajiona mie nina haki ya kukusanya.

Kwa hivyo, napenda na nitafurahi sana kuja kusikia kwamba mara inayokuja kwamba tayari uamuzi wa kuikabidhi mamlaka fulani uwezo wa kukusanya kodi inayotokana na mambo ya mafuta tayari limekamilika tusije tena na jibu la kuwa tutakaa tutafanya, tutaendelea kukusanya migogoro ya kila siku ni bora tuamue tumeampa *ZURA* tunampa *ZURA, ZURA* tunaitoa tunawapa *ZRB* iwe moja tu isije kuwa kila siku tunasema tutafanya lakini ikawa haijamaliza. *(Makofi)*

Lakini pia nikirudi tena hapo nyuma kwenye hiyo page ya 8 kama nilivyosema kwenye agizo hili la 21 kuna matayarisho, inasema kamati inaomba wizara husika pamoja na serikali kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya mafuta ikiwemo Bandari na Bohari ya Mafuta ya hapa nchini. Tumeona kwamba imeshatengwa maeneo ya Mangapwani kwa upande wa Unguja lakini kwa Pemba hatujaona vipi na ni vyema na busara. Hivyo, napendekeza na nashauri kwa sababu tunaingia katika mpango huu wa mradi mkubwa wa uchimbaji mafuta na gesi ni vizuri na busara tukawa na maeneo yetu ambayo tumeshayatayarisha kabla.

Mhe. Naibu Spika, tuwe na eneo letu la bandari ambayo itatumika kwa ajili ya kujenga hilo bohari kama ilivyoshauri kamati, na pia tuwe miundombinu yetu tujue wapi tutaweka matenki yetu ya kuhifadhia mali kulikoni kusubiri mpaka kazi imeanza ndio tunaanza kuhangaika hapa

na pale kutafuta maeneo ya kuhifadhia hiyo bidha yenyewe. Ni vyema na busara na naishauri wizara kuanza kulishughulikia jambo hili kwa kina mapema kabla ya muda haujafika ili ule muda ukifika iwe shauri hili tayari tumeshalitekeleza.

Vile vile, naomba nishauri ofisi, ili tuweze kwenda vizuri ni lazima tuwe na ofisi kwa pale Pemba naona *ZURA* wana kiofisi kimoja kidogo pale sijui kina wafanyakazi wangapi na hapa pia halikadhalika ni hivyo. Mhe. Naibu Spika, naomba wizara ifanye utaratibu wa kuwapatia ofisi kubwa nzuri za kudumu zinazolingana na hali ya hawa *ZURA*, kwa sababu hawa tunategemea si muda mrefu mambo yetu *Inshaallah* kwa uwezo Mwenyezi Mungu yatakuwa mazuri.

Sasa na sisi ni wajibu wetu tujipange mapema ili wakati ukifika isiwe tena hatuna ofisi hatuna nini. Kwa kweli, tukitilia maanani kwamba tutakapoanza miradi hii ya uchimbaji wa mafuta na gesi patakuja wawekezaji wengi, ambao watakuwa na pesa maeneo yatakuwa ni vigumu wakati huo kuyapata. Kwa hivyo, sasa ni vizuri tukaanza kujiwekea maeneo yetu tukayapima tukayatengenezea hati miliki tukayatengenezea na mpango kazi wake kwa kujua hapa kwa pahala hii na hapa *special* kwa kazi hii. *(Makofi)*

Lakini pia katika ukurasa wa 7 katika utekelezaji wa wizara wanasema wizara tayari imeshachukua jitihada zaidi katika kuwaorodhesha wanafunzi walioki kwenye masomo, wametakiwa kuwaajiri hawa na kwa sababu wanasomeshwa ni imani yangu kwamba wanasomeshwa na serikali. Kwa hivyo, hawa watu kwa sababu ya umuhimu wao serikali ikaona ni vyema kuwasomesha na mimi naungana na kamati kuitaka wizara iwaajiri ianze kuwaombea ajira serikalini mapema ili pale wakimaliza masomo tayari wanarudi wakiwa tayari ni wafanyakazi waliokwisha kuajiriiwa na wizara isijekuwa tena kesho au keshokutwa. Kwa kweli, tumezoea unaweza kupeleka barua leo wizara ikaomba wafanyakazi ikakaa muda mrefu bila ya kupata jibu kutoka wizara inayohusika na mambo ya utumishi wa umma kwa kuliepuka hili na mimi nakubaliana nanyi kwamba ni vizuri sana kuanza kuwaajiri vijana wetu hawa ambao wako masomoni, kufanya utaratibu wa kuwaajiri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, sawa. Lakini pia kwa hizo dakika mbili nilizobakia naomba nije kwenye suala la maji kama lilivyoelekezwa tumeambiwa tumeonekana hapa, kwamba suala la maji bado ni changamoto kwa Zanzibar yote, maeneo mengi yana mapungufu ya maji. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba wizara inayohusika italichukulia suala hili uzito unaostahiki na inaendelea kulichukulia, lakini bado ni changamoto kubwa. Pia tumeelekezwa jinsi ya malipo kwamba watu walipe kupitia kwenye simu zao za mkononi mimi naungana nao kwa suala la malipo, lakini malipo yaendane na huduma tusije tukawalipisha wananchi tukawalazimisha kulipa wakati huduma hiyo haipatikani, alipe mtu yule ambae kwamba anapata huduma tu.
Lakini kuna baadhi ya maeneo yanatimiza miezi sita hayapati maji baadhi ya maeneo sio yote. Kwa hivyo, tuwatake wale wafanyakazi ambao anasema tunao kwa wingi kule maafisa wetu waweze kuwaorodhesha na wajue kwa undani hasa nani anapata maji na nani hapati, ili wao waweze kuwaunganisha na mambo haya sambamba na malipo ya umeme. Malipo ya umeme watu wa *ZECO* wanatakiwa kurudi kwa wananchi walioko karibu kuwarahisishia na wao suala

lao la utaratibu wa malipo, kwa sababu kuwawekea vituo mbali vya malipo ni kuwaongezea *cost* wananchi wetu ambao ni masikini zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya haya baada ya mchango wangu huu mdogo ni imani yangu kwamba wizara umeyasikia na mimi sina budi kuipongeza wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya, na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa nampa nafasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameniomba dakika tano, naomba utumie dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru japo kuwa hizo dakika tano vyenginevyo vyovyote ingekuwa sikuwafanyia haki wananchi walionichagua au walionituma kuja kusema tatizo ikiwa wananchi wa Michamvi. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikilia sana tena sana kwa Shehia ya Michamvi anakotokea Waziri anayetokea Ikulu Mhe. Issa Ussi Haji Gavu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa nne agizo No. 11 Kamati inashauri Mamlaka ya maji Zawa kushirikiana kikamilifu na viongozi wa Wajumbe kwa wafadhili wanaotaka kuanzisha miradi ya maji na kutoa ushauri wa kitaalam, kabla ya kuanzishwa kwa mradi huo.

Mhe. Naibu Spika, sisi sote humu ndani shahidi maji ni kila kitu ya uhai wa binaadam hata ukifika hospitali huduma ya mwanzo ni *drip* inatokana na nini maji, Mhe. Naibu Spika, hata wewe au mimi tusingezaliwa bila ya kuwepo maji, maji ni fitina kila kitu hata soda inatokana na maji, maji ni kila kitu. Kwa kweli, nilikuwa nikipata shida sana na usingizi wangu hauji unakuja kwa vipindi kwa suala la Michamvi, narudia tena kusema na kusema na kulia na kulalamika tokea dunia kuanza mpaka leo hii sijui wamekosa nini wananchi wa Michamvi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 naomba kunukuu labda hii itanisaidia kidogo kuonewa huruma.

> Inasema "kuendelea kuimarisha usambazaji wa huduma za maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 87 mwaka 2015 hadi asilimia 95 mwaka 2020 kwa mijini na asilimia 70 mwaka 2015 kwa vijiji vijijini kama Michanvi".

Mhe. Naibu Spika, naomba nimkumbushe Mhe. Waziri na aandike hata akimkuta Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuwa akimnadi Mhe. Ussi Haji Gavu Chwaka tarehe 13/10 Mhe. Rais wa Zanzibar, alisema akirudi madarakani atahakikisha maji asilimia mia yanapatikana, sio maneno yangu haya nipo Chwaka alimchukua Mhe. Ussi Haji Gavu akamnadi pale na Dkt. Sira Ubwa Mamboya tulikuwa tuko pamoja katika kampeni hizo, basi niombeni haya si maneno yangu Michanvi kuna tatizo kubwa, muda wao watu huku hawashughulikii kilimo isipokuwa kuhangaika kutafuta huduma za maji na kumechimbwa kisima *Ras-el-Khaimah* kule kiko.
Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira aliwahi kujibu hapa kwamba serikali haiogopi hasara kwa wananchi wake, sasa inaogopa kitu gani simba, nyoka na serikali hii tukumbuke isingekuwepo madarakani bila ya kuwa na wananchi wakiwemo wananchi wa Michanvi, wananchi ndio serikali hebu tuelezeni lini huduma hii itafika kuna mahoteli, kuna wawekezaji na wawekezaji ni *priority* katika nchi hii, kuna hoteli karibu tano.

Mhe. Naibu Spika, tuangalie Buswana utapewa kiwanja msituni lakini huduma zote utapelekea ikiwemo maji, barabara, umeme mpaka laini ya simu unatiliwa, sasa wawekezaji hawa tunawajali au tumekuwa na huruma ya mdomo vitendo havipo. Mhe. Naibu Spika, hapa Ramadhani tena ndio mwezi mtukufu Mhe. Rais wa Zanzibar nimshukuru sana aliwaagiza mamlaka ya maji *ZAWA*, lakini hayo maji yalikuwa yanakwenda utafikiri *panadol*, gari tatu wiki nzima.

Kama kuna mtu wa kuja kunisuta aje anisute niko tayari Sheha wa Michanvi bwana Abeid Juma anayajua haya, mimi si kazi yangu kupeleka huduma za maji Michanvi wameichaguza kuja kuwasemea matatizo yao wananchi hapa lakini ile imani, lini huduma hii itafika kule. Kwa kweli, hichi ni kitu cha kusikitisha gari moja shilingi 60,000/= tutafanya mangapi sisi Wawakilishi tufike pahali tuwe na huruma ya mdomo sio vitendo, kitendo hichi kinaturudisha nyuma baada ya kwenda skuli mtoto anakosa masomo kwa kufuata huduma ya maji haielekei. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nafikiri Mhe. Waziri amenisikia. Lakini hapo hapo nirudi katika Kamisheni ya Ardhi kwa kumalizia nam. 2. Kamati inaomba Kamisheni ya Ardhi iandae mpango maalum kuwapatia mafunzo masuala ya ardhi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwemo masuala ya upimaji, usajili, utambuzi wa wamiliki. Mhe. Naibu Spika, kama kuna pahali palipooza Waziri anapajua Kamisheni kama wapo wenyewe huko waje watwambie anajitahidi Mhe. Waziri, lakini watendaji wake wasumbufu, ndio pale ninaposema kosa la ng'ombe wa mbele lakini anapigwa ng'ombe wa nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Waziri anasaini hati kuna sababu gani kuzitoa pale Katibu Mtendaji jamaa yangu lakini anisamehe kwetu kumoja. Mhe. Naibu Spika, naomba anifahamishe kuhusu Katibu Mtendaji wakati Mhe. Waziri anasaini hati si moja wala si mbili, kwa nini unashindwa kuzigawa. Kutokana na hali hiyo, migogoro inasababishwa na wizara, halafu wanalaumiwa Masheha, Madiwani chanzo ni wizara kupitia hii kamisheni yetu, ambayo inachukua kamisheni kiasi gani ili upate hati yako. Mhe. Naibu Spika, naomba jina libadilishwe isiitwe kamisheni tena maana yake kamisheni, unahitaji kitu imekuwa jina baya hata wasia tunapewa majina mabaya tusiwape watoto wetu yanadhuru. Kwa hivyo, naomba Kamisheni ya Ardhi iondoshwe imekuwa kamisheni kubwa inaihitaji sasa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, dakika ulizoomba zimekwisha na nyengine nimekuongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Panya Ali Abdalla, umeniomba uchangie dakika tano naomba nikupe dakika tano halafu ataingia Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata fursa hii nashukuru sana na mimi niweze kusema machache katika Wizara hii. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wa wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya, lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza wana kamati na hasa

yule muwasilishaji ambaye tulimpata leo Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ambaye amewasilisha ripoti kwa ufasaha kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kuchangia katika agizo No. 12. Kamati imeiomba Mamlaka ya Maji *ZAWA* kuhakikisha inayapima maeneo yote ya vianzio vya maji Unguja na Pemba. Kwanza nishukuru kabisa kwamba wizara niipongeze kwa hatua ile ambayo wameanza kuichukua, kwa sababu inaonesha hapa kwamba tayari wameonesha maeneo ambayo wameyapima. Kwa hivyo, niiombe tena serikali iongeze juhudi kwa sababu maeneo ya vianzio vya maji ni maeneo muhimu sana kabisa, tunapoyaacha tu yakiwa wazi maana yake ndipo unapokuja ule uvamizi sasa wa kuvamia maeneo hayo na yakaanza kuchukuliwa na kukapata wananchi usumbufu wa maji. Kwa kweli, huu usumbufu wote ambao tunaupata hivi sasa ni kwa sababu ya kuyaacha huru maeneo ya vianzio vya maji mpaka yakavamiwa, ndio yamekuwa maji sasa hayatutoshi. Kwa hiyo, naomba serikali jitihada hii ambayo imetuonesha iendelee kuonesha jitihada hii, ili iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia niendelee na pongezi zangu katika wizara hii katika ombi la kamati la kuitaka wizara kuingizwa malipo ya umeme moja kwa moja katika *account* ya *ZECO*. Kwa hiyo, niwashukuru na niwapongeze kwamba ombi hili limepokelewa ni mara nyingi hapa katika Baraza tulikuwa tukieleza tukiona katika vitabu vile vya bajeti vinaonyesha yale matumizi ambayo yamepanga wizara, lakini ukenda huku utakuta wizara inasikitika kwa sababu hakuna yale malipo ya umeme.

Lakini leo pango huu ukifanyika kwamba moja kwa moja fedha hizi tukiweka katika *account* ya *ZECO* zikaenda kutoka katika mawizara maana yake faida mbili zitapatikana. Kwanza hawa wanaolipa watapata huduma nzuri ya umeme na watakosa kukatiwa lakini *ZECO* itaweza kuingiza mapato katika shirika hili na kuweza kujikimu na kujiendesha vizuri. Kwa hivyo, nichukue fursa hii niseme kwamba hili walilolifanya liendelezwe, kwa sababu litaweza kuleta faida kubwa katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la maji kwa kweli wizara inajitahidi sana katika suala zima la maji, lakini bado suala hili tuna matatizo. Hivyo, naiomba sana serikali kwa unyenyekevu mkubwa iendelee katika juhudi zake kubwa katika mpango wake inaojipanga basi tuweze kupata maji safi na salama, ili wananchi wetu waweze kufaidika na matunda haya ya Mapinduzi, kwa sababu hii yote ni shauri ya Mapinduzi ndio wananchi wameweza kupelekewa huduma mbali mbali ambazo ni muhimu kwao.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali maji ni suala la mwanzo kabisa ambapo kila kitu kinahitaji maji hata mshauri alisema, "Maji yakiadimika viumbe tuko tabuni" Kwa maana hiyo, naendelea kuiomba sana serikali na naipongeza sana iendelee na juhudi hizi, ili wananchi tuweze kupata mafanikio mema. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa tumkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, kwa ajili ya kujibu baadhi ya hoja kabla ya kuja Mhe. Waziri Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kuchangia ripoti. Kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kutoa mchangoa ambao mengine yanataka ufafanuzi, lakini mengine ni ushauri na maelezo kwa ujumla niseme tumeyapokea lakini zaidi Mhe. Waziri akija akitoa majumuisho ni tegemeo langu kwamba anaweza akakidhi haja ya wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, nianze ile habari ya Ndagoni ya kwamba kuna tatizo la ardhi lakini pia la maji. Ni kweli kama alivyosema Mhe. Suleiman Makame Ali tulipanga na nilimuahidi hapa kwenye Baraza na niliwahi kumpigia simu kwamba ningeenda makusudi kwa ajili ya kutekeleza ile ahadi, lakini kwa bahati ikaingiliwa na ratiba ya ziara ya Kamati kwenda Dar es Salaam kwa hivyo ndio maana sikuweza kufika. Hata hivyo, napenda nimuahidi tena kwamba Mwenyezi Mungu akijaalia tutapanga na tutakwenda kwa ajili ya kuangalia tatizo ni nini, kwa sababu inawezekana kuna tatio la ardhi, lakini inawezekana imesababishwa kati ya mwananchi na mwananchi na kamisheni au wizara yetu ikawa inatajwa tu kwa vile ni wizara inayohusika na ardhi.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba nisisitize kwamba sheria haibagui ikiwa tajiri, ikiwa masikini, ikiwa mwanamme ikiwa mwanamke, siku zote sheria inamsaidia yule aliyekuwa tayari kusaidiwa. Sheria haiondoki kwenye maandiko ikaja ikakutetea huko ulikofanyiwa kosa, ni wewe mwenyewe inakuta uwe *active*, utoe ushirikiano ndipo sheria itakusaidia. Kusikia tu kwamba pahala fulani kuna mtu anafanya hivi labda ananyang'anywa ardhi na katulia, hakuna nafasi ya kuilaumu Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, katika mfumo wetu sehemu ambayo inatoa haki ni Mahakama na kwa upande wa ardhi tuna *Land Tribunal* iwapo kuna tatizo kati ya mwananchi na mwananchi juu ya ardhi basi ni sehemu ambayo upande uliokuwa haujaridhika uwende pale ukadai haki. Kwa kweli, pale *regardless* mnyonge ama tajiri ilimradi sheria itatendeka na mwenye haki atastahiki kupata haki. Sasa, iwapo Kamisheni ya Ardhi ndiyo ambayo inahusishwa na hilo, basi hilo litakuwa linakuja kwetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini upande mmoja mwananchi na upande mwengine mwananchi nadhani sehemu ya Kamisheni ya Ardhi, *just* ni kutoa ushahidi tu kama kuna hati mbili basi *this is valid* ambayo imetolewa na Kamisheni ya Ardhi. Lakini iwapo mmoja ana hati na mwengine ana hati, mmoja *fake* na mwengine halali, kamisheni haihusiki. Sisi siku zote tunatoa hati safi, kama kuna hati nyengine siyo safi ambayo inasababisha migogoro sehemu ya kutoa haki ni Mahakama.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa wananchi wote wawe na uwelewa huo, iwapo wamenyang'anywa au wana matatizo na ardhi kati ya mwananchi na mwananchi, basi waende katika vyombo vya utoaji haki. Mahakama ya Ardhi *Alhamdulillahi*, Unguja na Pemba Mikoa yote ipo isipokuwa Kaskazini Unguja tu ndiyo wanalazimika kuja Mjini Unguja.

Mhe. Naibu Spika kwenye suala la maji ni kweli na hata wakati tunajibu leo asubuhi tulisema tuna changamoto, maji yanapatikana lakini pia kuna baadhi ya maeneo maji hayapatikani vizuri. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf aliomba kupatiwa idadi ya fedha ambazo zimetumika kwa serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar lakini pia zile za wahisani zikiwa pamoja na za mkopo. Kwa kweli, kama alisikiliza vizuri tulitaja idadi kwamba bilioni 178,251,400,000/=, na

tukachanganua zipi zilitolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zipi zilitolewa na wahisani ikiwa kwa njia ya mkopo ama ufadhili.

Sasa ikiwa bado kuna suala jengine ambalo linahusiana na hili hajaridhika na hapa labda ningemshauri andike swali na alete kwa utaratibu hapa Barazani, ili tuweze kumpatia majibu ambayo anayahitaji.

Mhe. Naibu Spika, pia kwa upande wa maji tuliwahi kuulizwa hili swali kwamba zile pesa milioni 92 dola za mkopo zingegaiwa kwa majimbo kama ambavyo Mhe. Ali Suleiman Ali leo pia kalirejea. Pia tuliwahi kutoa majibu kwamba kila kitu kinachoombwa kina utaratibu wake. Haiwezekani unaomba kwa kufanya hivi pesa zikija tena ugeuze matumizi na ukizingatia kwamba tunakwenda sambamba na wale wenyewe wanaotoa ule mkopo. Sasa kwa masharti ambayo tuliyoombea ule mkopo isingewezekana kubadilisha matumizi.

Hata hivyo, tunatambua kwa kiasi kikubwa maji yanakosekana kutokana na uchakavu wa miundombinu, pesa zile kwa kiasi kikubwa zitatumika katika kubadilisha mabomba, ili tatizo lile liweze kuondoka.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf pia alizungumza kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wanategemewa wapate viwanja. Hivyo, ni vyema wasipate lakini wapate wananchi wa kawaida. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba sheria haibagui, sheria inapozungumzia Mzanzibari maana yake ni Mzanzibari, kwa sababu leo ni Mwakilishi lakini kesho ukawa ni mtu wa kawaida, leo ukawa tajiri lakini keso ukawa masikini, na masikini wa leo kesho anaweza akawa tajiri. Sheria ipo ilimradi tuzifate tu sheria, mwananchi ana nafasi ya kuomba na hauziwi ardhi, ardhi kama tunavyojua kwamba yote ni ya Mhe. Rais wa Zanzibar iko mikononi kwake kamchagua Mhe. Waziri kusudi kwa kumtumikia na mpaka sasa Mhe. Waziri *Alhamdulillahi* anakwenda kutokana na sheria zinavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, kila mwananchi anayo nafasi ya kuomba, apeleke barua yake Kamisheni ya Ardhi, lakini wasitegemee wote kupata kwa wakati mmoja kwa sababu kama viwanja mia, maombi elfu usitegemee kwamba kuna zaidi ya watu mia watakaopata ni kutokana na idadi ile. Sasa kama Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akisema hapana mimi hapana badala yangu basi mwananchi fulani aombe *Ishallah Alhamdulillah* usimsemee mwengine kila mmoja ajisemee yeye mwenyewe kutokana na mahitaji yake. Lakini hakuna mtu aliyezuiliwa kuomba, aombe na kadri nafasi na fursa inavyopatikana basi itapatikana.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kwa upande wangu ili nipate kumuachia Mhe. Waziri ili atoe ufafanuzi, kuhusiana na Hati Miliki, kwenye ripoti mbali mbali na hata hii ya leo. Niseme tu kwamba mwanzoni kulikuwa kuna utaratibu haujakamilika, lakini kwa sasa utaratibu umekamilika, na kipaumbele chetu ni taasisi za serikali, lakini na wale wananchi ambao ardhi zao hazina matatizo, tayari zimetambuliwa na kusajiliwa, tayari watapatiwa hati kwa kubadilisha zile za zamani wapate mpya lakini halikadhalika kwa wale ambao hajapata wapatiwa mpya.

Lakini hapa itambulikane kwamba kamisheni mara nyengine wanaichukulia kama ni tatizo, wanapokuwa wanafuatilia kusudi wajuwe ukweli kabla ya mtu kupewa hati, kusudi baadaye

tusijetukapata migogoro wengine wanalichukulia kama urasimu. Bora haya kuliko ya huyo, kwa maana ya kwamba tunataka kupunguza migogoro ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunaomba tusaidiane, nashukuru Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ilishauri kwamba tupate taaluma juu ya masuala mazima ya ardhi. Tumekubali hapa kutoa taaluma kwa Waheshimiwa Wajumbe wote. Imani yangu ni kwamba Wajumbe wakifahamu watatusaidia katika maeneo yetu. Utaratibu ni muhimu wale wote ambao wanahisi labda kuna tatizo, kuna urasimu, mlango wa Mhe. Waziri, wa Naibu Waziri, wa Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote ipo wazi, tushirikiane ili kusudi kwani sisi sote tunajenga nyumba moja.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana naunga mkono ripoti hii kwa asilimia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na yeye aje kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamezitoa kupitia Ripoti yangu hii ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wale wote waliochangia kwa njia moja au nyengine kuhakikisha kwamba wanaiboresha au wanatupa muongozo, ili wizara hii iweze kuwa endelevu lakini iwe ni wizara inaweza kufanikisha kazi zake kwa kila siku. Ninachoamini Mhe. Naibu Spika, kwamba kila mmoja ana dhamira safi ya kuona kwamba Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inafanya kazi zake vizuri na ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huwo naomba sana niwatambue wale wote waliochangia ili tuweza kutoa ufafanuzi wa zile hoja. Kwanza naomba niitambue Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ambayo baada ya kuwasilisha yale maagizo lakini pia waliweza kuja na hoja ambayo Mwakilishi wa Mwenyekiti, ameweza kuyatekeleza ipasavyo. Naomba niwatambue Waheshimiwa waliochangia katika Wizara yangu kama hawa wafuatao:

1) Mhe. Ali Suleiman Ali
2) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
3) Mhe. Simai Mohammed Said
4) Mhe. Suleiman Makame Ali
5) Mhe. Omar Seif Abeid
6) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
7) Mhe. Panya Ali Abdalla
8) Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Hawa wote wamechangia kwa njia ya moja kwa moja. Lakini wapo wengine ambao wamechangia pia kwa kutumia njia ya maandishi. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niwatambue.

1) Mhe. Mariyam Thani Juma
2) Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
3) Mhe. Masoud Abrahman Masoud
4) Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Hawa wote wameleta michango yao kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza nipokee yale yote yaliyoagizwa na kamati niwapongeze sana kwasababu wamekwenda Tanzania Bara na wakafanya ziara DAWASA wakaona hali halisi, kwa hivyo na sisi wakaweza kutushauri na kutupa maelekezo kwa yale ambayo wameyaona. Ni jambo zuri na sisi wizara tumefarijika leo kuyasikia na tumeyapokea na tutayafanyia kazi kwa yale ambayo yanafanyika kazi na yale mengine tutaendelea kushirikiana na kamati. *(Makofi)*

Vile vile, niende na Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele ndugu yangu Ali Suleiman Ali ambaye alitaka kujua tumefikia wapi kuhusu ule mradi wa India wa wananchi *92 billion dollars* ambayo tulizungumza kiywa kipana na kila mwananchi katusikia.

Process mchakato unaendelea na sasa hivi tumefikia katika hatua ya kutafuta mkandarasi kwa sababu waliyoomba walikuwa ni 27 kutoka kampuni za India. Lakini 27 tukaenda nao wakawa *prone* mpaka 9, katika 9 tumekwenda nao mpaka 7 na sasa hivi katika 7 tumefikia hadi mmoja. Juzi tu na jana tumekaa na Mwakilishi wa *Exim Bank*, ambaye anatoa hii pesa alikuja katika kuangalia ule mchakato na kufanya ufafanuzi na mchana wa juzi tulikuwa tunafanya *presentation* na jana katika hao wamekaa kufanya upembuzi. Tukimaliza hiyo kazi atapatikana Mshauri Muelekezi ambaye nimesema mkandarasi *before sorry*, mshauri muelekezi ambaye yeye sasa atatupa *directive* kwa hivyo hapo ndiyo tulipo fikia.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe taarifa kwamba mchakato unaendelea na kazi hii inaendelea na hii pesa ni mchakato haiji tu hivi hivi, kwa hivyo tutakwenda na zile *processes* ambao wao wametupa masharti au vigezo kwa sababu hii pesa ni mkopo kwa hivyo ndiyo tunakwenda nayo.

Vile vile alizungumzia sana suala la Agizo Nam. 7 lile la upotevu wa maji na matatizo ya mafundi. Mhe. Naibu Spika, kwa ridhaa yako na kwa ruhusa ya Wajumbe naomba niyajibu haya maswali mengi ya maji kwa ujumla wake. Katika hili naomba nijibu kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama. Ndiyo maana serikali ina jukumu kubwa katika kuhakikisha kwamba wanatafuta mbinu yoyote ili kuhakikisha wananchi wanapata hii huduma.

Sasa hivi serikali ukiacha mkopo wa na *92 billion dollars* ambayo imechukua katika Serikali ya India, lakini kuna pesa za *JICA hundred million dollars*, pia kuna pesa ya Wachina ambayo tumechukua mkopo *thirty one UFB* lakini bado tunaendelea na mchakato kuhakikisha kwamba wananchi wanapata hii huduma. Hivyo, ndio maana serikali inachukua mzigo mkubwa wakati wote kuhakikisha kwamba hii kazi inafanyika.

Mhe. Naibu Spika, tunajitahidi pamoja na mamlaka kufanya sana kazi pamoja na changamoto na mapungufu madogo madogo yaliyokuwepo, ninachoamini kwamba kila mtu anajua kila tone la maji thamani yake. Kila mwananchi ili awe na afya na aweze kuishi anahitaji kupata maji. Ingekuwa maji kabisa hatuna basi tungekuwa na tatizo kubwa, lakini kwa juhudi zile zile za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wetu wa Zanzibar basi na sisi tutandelea kuziendeleza na ndio maana hapa tulipofika tumefikia.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kusema kwamba kuna *issue* imejitokeza kwenye *ZAWA* kwenye suala la hizi *pump* za *Ras-el-Khemah*. Kweli visima 150 vilivyochimbwa hivi vyote vilikuwa na *pump*. Naomba niseme mamlaka mara nyingi inakwama na katika tatizo lile na ile nia thabit ya serikali na mamlaka ya kuwapatia watu huduma safi na salama. Inapoungua *pump* zile *pump* zilizokuwepo tunasema tuka-*rescue situation* ili watu waweze kupata huduma. Kwa hivyo, *pump* zile zinatumika.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu kila siku visima vinavyoendelezwa *pump* zinazidi kuagizwa ili pale zinapopatikana pesa kuungwa kisima kingine *pump* ile inarejeshwa. Ni dhamira safi, nia nzuri nikuhakikisha katika lengo la kwamba wananchi wetu wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama.

Vile vile, labda nizungumze suala ambalo limezungumzwa pengine limetokea, kisima kimechimbwa Tomondo lakini watu wa Tomondo hawafaidiki na ndiye tuali hili hili tunavisima vingi katibu 12 kule Bumbwisudi, lakini visima vile vinafaidisha watu wa mjini. Wakati mwengine katika *master plan* ya muundo wa maji wanamiundombinu kuna maeneo kuna maji mengi na kuna maeneo maji hakuna. Tunataka katika maeneo yenye maji mengi ifike ile huduma iwafikie watu wote siyo watu wa pale tu. Utakuta sehemu inachimbwa kisima lakini kisima kile kimechimbwa Tomondo lakini kinapelekea watu wa Fuoni maji, au watu wa Kwamtipura maji. lakini katika ile *methodology* ambayo tunaitumia ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tushirikiane katika kutoa huduma hii, lakini tushirikiane katika ku-*facilitate* kuona kwamba wananchi wetu bado tunaendelea kuwahudumia.

Jambo jengine naomba niseme serikali kulipitia mamlaka ina juhukumu la kuwahakikishia wananchi wake wanapata maji safi na salama wakati wowote. Lakini wakati mwengine tunashirikiana na Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi kuhakikisha kwamba wananchi wao katika maeneo husika wanapata maji safi na salama. Tuendelee kushirikiana, tuna jukumu kubwa lakini sote Mwenyezi Mungu katuweka hapa kutuhakikishia kwamba tunawatumika wananchi wetu ambao wametuweka madarakani. *(Makofi)*

Naomba katika hili pia niongezee suala ambalo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye ni rafiki yangu na kila siku analizungumza. Suala la Michamvi kule mimi nilikuwa sijui kumbe kuna Michamvi mbili lakini nimejua kuna Michanvi mbili na moja ndiyo yenye tatizo kubwa la maji. Katika hili Mhe. Jaku Hashim Ayoub anajitahidi sana lakini na mamlaka pia inajitahidi sana. Kwa kweli, Mhe. Jaku Hashim Ayoub anashirikiana mara nyingi na mamlaka katika kuhakikisha katika hali hii kazi inafanyika vuziri.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba niseme kuna kisima cha *Ras-el-Khemah* tayari kimechimbwa, lakini pia kuna tangi ambalo tayari limeshajengwa katika kupatiwa maji watu wa Michamvi, ila kuunganishwa miundombinu bado haijafanyika. Mhe. Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi wanaonisikiliza, kwamba serikali kama nilivyosema ina nia thabit katika mpango ule ule wa kuhakikisha, kwamba hichi kidogo tulichokuwa nacho tugawane kidogo kidogo na tunakenda hatua kwa hatua basi *Ishaallah* na Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake atatupa nguvu, ili tuweze kukiunga kisima hicho na wananchi wa Michamvi waweze kupata maji.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kuna matangi ambayo yameahidiwa kujengwa ambayo pia yapo katika *processes* na yanaweza kujengwa. Ukiangalia kule Kazini ule mradi wa China unaendelea vizuri, matangi karibu yote yameshajengwa, visima vingi vimeshajengwa na vyengine vimeshaanza kuunganishwa. Kwa hivyo, katika jitihada ile ile ya kuwapelekea wananchi maji safi na salama, basi mimi ninachoamini miradi hii yote ikeshakutimia basi maji yetu yatakuwa safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Ali Suleiman Ali aliuliza na aliwapa pongezi sana watu wa *ZECO*, pongezi tumezipokea lakini watu wa *ZURA*, lakii ile *issue* ya *transformer* ndogo bado tunaifanyia kazi, kwa sababu *transformer* ilipowekwa ilikuwa inakidhi mahitaji ya wananchi wakati ule. Sote tunakiri kwamba ukuwaji wa mji unakuwa hasa katika jmbo la Mheshimiwa. Ukenda katika jimbo la Mhe. Mjumbe utakuta mpaka njia zinakuwa wakati mwengine shida. Sasa hivi watu wamekuwa wengi kwa hivyo mahitaji yamekuwa makubwa.

Kwa hivyo, naomba nimhakikishie kwamba suala hili tumelipokea na tutalifanyia kazi, pale tutakapoona uwezo umepatikana na *transformer* imepatikana tutabadilisha *transformer*. Naomba nikupongeze sana kwa kupongeza *ZECO* na *ZURA* kwamba wanafanya kazi vizuri na nakuahidi kwamba watazidi kuongeza bidii ili kazi hizo zifanyike vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alivyojaribu kulieleza katika Agizo Nam. 6 la *FK Enterprise* aliuliza huyu ni nani. Huyu ni *FK Enterprise* ambaye alipewa *lees* katika Kamisheni ya Ardhi na amekaa kwa muda mrefu lakini likatoka agizo kwamba *lease* ile basi ifutwe atatutiwe eneo jengine.

Lakini baada ya majadiliano na kamati wakasema hapana hakuna sababu, kwani keshakiuka sheria zote na taratibu zote za umilikaji wa eneo kwa hiyo eneo lile, basi lifutwe na asitafutiwe eneo jengine na kazi hiyo imefanyika na eneo limerudi serikalini.

Lakini pia swali ulilolizungumza ni vizuri sana kwamba ardhi basi tuangalie wanyonge zaidi. Mhe. Naibu Spika, nafirikiri serikali yetu haina ubaguzi hata kidogo na serikali hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi na katika kutekeleza utekelezaji wake wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaendelea kuwa si wabaguzi na ndio maana tuko tofauti, hata hapa ndani tulipokaa tuko tofauti, kuonesha kwamba serikalii hii haina ubaguzi, lakini mtu yuko kwa kwa taratibu maalum. Kwa hiyo, naomba niseme tu kila atakayeomba na uwezo upo na kama ile ardhi ipo basi atapewa.

Lakini chengine ambacho nataka kukiongea swali la maji nimeshalizungumza kwa ujumla wake. Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la umeme mbadala kwamba serikali sasa hivi tunatumia chanzo kimoja tuu cha umeme kutoka Tanzania Bara. Lakini suala la umeme mbadala linazungumzwa kwa muda mrefu. Kwa bahati nzuri ripoti yake tuliipokea tokea tarehe 01 August mwaka huu, kwamba ule upembuzi yakinifu umefanywa na ripoti ile *study* tumefanya. Kwa mfano, kuna maeneo kama Muambe kule Micheweni lakini Makunduchi, Bambi kuna minara ambayo iliwekwa kwa watu wanaotoka maeneo yale kwa sababu ya utafiti ule. Katika utafiti ule imebainika kwamba kwa Zanzibar tunaweza kutumia umeme wa jua bila tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kupokea ile taarifa na kuambiwa kwamba sasa hivi tunaweza kutumia umeme wa jua tatizo lolote, serikali tayari imeshatoa ruhusa. Kwa hiyo, sasa hivi tuko katika matayarisho ya kuona kwamba tunatengeneza kanuni, lakini tunatengeneza vitu vya kufanya kwamba hata muwekezaji anapokuja tuweze kum-*hold* na aweze ku *capture* mazingira yetu ya Zanzibar. Kwa hiyo, hili tumelipokea na hili naomba nitoe taarifa tunaendelea kulifanyia kazi.

Kwa kweli, naamini tukishatumia umeme huo basi uzalishaji utakuwa mkubwa na hatutakuwa tegemezi sana, na huu uwekelezaji nategemea uanze mara moja tu 2018 tuwe tumeanza na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia sana suala la kukuza elimu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe mwengine walizungumzia suala la kuwapa elimu hata watoto wa wanyone. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo nchi hii si nchi ya kibaguzi kila mtu anayo haki ya kusoma na elimu ndio maana ilitangazwa bure, lakini hizi sekta pia zinahitaji na *interest* pia kwa sababu wakati wengine watu wengi hawapendi kusoma *science subjects* hasa watoto wetu wanapenda kwenda kwenye *art* kwa sababu ya urahisi wa masomo.

Lakini tukumbuke kwamba *oil and gas* ni masomo ambayo yanahaitaji mtu mwenyewe ayapende, maana yake huko kuna Jiologiya, kwani mambo ya *Petroleum Industry* yanahitaji vitu vingi. Kwa hiyo, naomba kama wapo basi bado tuendelee kushirikiana, ili waweze kupitia taasisi husika, kwa sababu sisi kama wizara hatutoi moja kwa moja, isipokuwa tunatoa mafunzo kwa ajili ya watu wetu ambao tunao ndani.

Sasa kwa wale wengine kupitia taasisi husika naomba basi tushirikiane, ili kuhakikisha kwamba hawa watoto ambao tunawahisi ni wanyonge hawana uwezo na hawako *influation*, basi tunaweza kupatia huduma hiyo na kuweza kupata elimu kwa wale wanaotaka ambao waweze kusoma kwa vizuri. Lengo la serikali la kutoa elimu bure la kujenga vyuo mpaka vyuo vikuu, ni lengo la kuhakikisha kwamba hata mnyonge anaweza kupata elimu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo alilizungumza Mhe. Simai Mohammed Said alizungumza kwa umakini sana kuhusu *issue* za kwanza agizo nam. 4. Naomba kwamba ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilioko na kwa uwezo pale inapoweza kupatikana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia alizungumzia kuhusu suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na kuangalia ndani ya makampuni. Lakini naomba niseme kwamba serikali imo katika hatua za

mwisho za mazungumzo *negotiation* na kampuni ya *Ras Gas* katika kukamilisha mkataba, ili mambo haya utaratibu yapate kuanza hizi shughuli za utafiti ziweze kuanza. Kwa hiyo, tuko kwenye *negotiation* na tumefika hatua kubwa, isipokuwa kuna mambo machache ambayo bado hatujakubaliana, lakini kwa maslahi ya taifa hili na kwa maslahi ya Wazanzibari. Kwa hivyo, tutakapokubaliana katika hili ninachoamini ni kwamba shughuli hizi za utafiti zitaanza mara moja.

Lakini pia Mhe. Simai Mohammed Said aliulizia kuhusu mfumo mpya wa waagiziaji mafuta ambao alipata wasiwasi kidogo kusikia siri ya upatikanaji wa mafuta na makampuni yaliopo waengezewe shilingi 40/= walizoziomba, ili kukabiliana na kima cha chini cha mshahara. Mhe. Naibu Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Simai Mohammed Said pamoja na Baraza kwa ujumla, kwamba mchakato wa ununuzi wa mafuta kwa utaratibu wa pamoja, yaani *Bulk Procurement System* ni wawazi siku zote katika mfumo huu unakuwa uko *very much transparent*. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi na zoezi hili limeshakamilishwa kwa kuwaalika wadau wote, waandihsi na wananchi kushuhudia hili zoezi.

Serikali itajitahidi sana kuwa mafuta hayakosekani na tarehe za kuleta mafuta kuwa zinatangazwa mapema na kueleweka, na ndio maana *ZURA* kama ni jukumu lao kutanganza. Kwa hiyo, na wao wanatangaza mapema hivyo tatizo linakuwa halipo.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuhusu maombi ya makampuni ya mafuta yaliopo Zanzibar yakuongezewa shilingi 40/= kwenye faida yao, ili kumudu gharama za malipo ya ongezeko la mishahara linafanyiwa kazi na *ZURA*, ili kuepusha athari kubwa kwa wananchi. Kwa kweli, inatubidi tuangalie pande zote mbili tusije tukaangalia upande mmoja halafu upande wa pili ikaja kuwa tunawapa mzigo mkubwa wananchi, hasa tukizingatia kama tunavyozungumza wananchi wetu wengi ni wanyonge. Kwa hiyo, hili tumelipokea na tutaendelea kulifanyia kazi na *ZURA* wamelipoka. *(Makofi)*

Pamoja hayo, Mhe. Simai Mohammed Said kwa umakini wake alizungumzia mapungufu katika Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia. Katika sheria ile sasa hivi ndio kwanza tumeanza kuifanyia kazi, kwa hiyo sisi tumeona kwamba kwa sasa hivi ile sheria bado ni nzuri na wala hatuna tatizo nayo, kama kutatokea changamoto au mapungufu yoyote ambayo baadaye tutaiona, basi hatutosida kuirejesha ndani ya Baraza hili, kwa sababu Baraza hili ndio walioipitisha sheria ile na kwa pamoja tukaweza kuifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Simai Mohammed Said kwamba ripoti hii ni yake maagizo ya kamati na sisi tumeyapokea pamoja na ushauri wako kama nilivyosema na tutaendelea kuifanyia kazi.

Lakini lile la mwisho ambalo amelizungumza kamati na wizara basi tunaone kule Tunguu, basi hili pia tumelipokea bahati nzuri na mimi nakaa Tunguu maeneo ya huko huko Jumbi. Kwa hiyo, mimi na wenzangu tunakwenda pamoja na kushirikiana na Mhe. Simai Mohammed Said kwa ajili ya kwenda kuona na tukisha kuona, basi tutashauriana na tutafanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na majumuisho ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Sasa kuna hoja ya Mhe. Suleiman Makame Ali jinsi alivyozungumzia kuhusu migogoro ya ardhi kule

Ndagoni. Hivyo, naomba niseme kwamba suala hili nimelipokea Naibu Waziri wangu alilizungumza kwa ufasaha na alijaribu kulitolea ufafanuzi mimi kwangu limekuwa *new* baada ya kunipa hiyo barua sasa hivi. Lakini naomba Mhe. Suleiman Makame Ali, kwamba sisi migogoro yote tunaifanyia kazi na nimelipokea na tutahakikisha kwamba tutalifanyia kazi na kwanza kwa hatua ya awali tutawagiza watu wetu wa Pemba basi waende kuona kuna nini na waweze kutuletea ufafanuzi unaofaa. *(Makofi)*

Lakini swali ya watendaji wasio waaminifu hasa kwenye Mamlaka ya Maji (*ZAWA)*. Kwa kweli, hili sisi tunaendelea kulifanyia kazi siku hadi siku na tunatamani kama wako, basi naomba sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla tusichoke kutoa taarifa na kama tunaudhibiti basi naomba katika hili niletewe moja kwa moja. Mhe. Naibu Spika, toka nimeingia ndani ya Baraza hili nimesikia hichi kilio kikubwa lakini naweza kuthubutu kusema nimemsikia Mhe. Ali Suleiman Ali peke yake ndiye aliyeweza kuniletea udhibiti na akaniletea huyo mtu na tukamchukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu. Kwa hiyo, naomba nitoe wito kwa wengine pia waweze kufanya kazi kama hiyo pale.....

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, punguzeni minong'ono msikilizeni Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kama tunahisi kuna watendaji sio waaminifu. Vile vile tutaendelea kushirikiana na mashehe na viongozi wengine katika maeneo madiwani, basi pia tutakaa nao ili kuona pale inapotokea tatizo basi wasiache kutoa taarifa. Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba nisema sana nampongeza sana Mhe. Ali Suleiman kwa juhudi kubwa anayochukua katika hiki hata madiwani wake amewafunza kuwa wanaweza kupiga simu na kutoa taarifa pale panapotokea tatizo wakati wowote. *(Makofi)*

Lakini pia naomba niendelee kama nijibu maswali ambayo ameyazungumizia Mhe. Omar Seif Abeid. Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumze kwa ufasaha kidogo kwa sababu alizungumzia *issue* ya *ZURA, ZRB* na *ZBS*. Kwa kweli, hivi vyombo vitatu tofauti vyenye majukumu tofauti uwezo wa taasisi za kukusanya mapato hizi zote kila mmoja ina utaratibu wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze *ZURA* yeye ni Mdhibiti. *ZURA* inasimamia masuala yote ya mafuta kuanzia wanaoagiza, wanaohifadhi mafuta lakini wanauza na kupanga bei kwa bidhaaa ya mafuta hiyo kazi ya *ZURA*.

Lakini ukija *ZRB* inahusika moja kwa moja na kukusanya kodi zilizopangwa na serikalli ndani ya mauzo ya mafuta, hiyo ndio kazi ambayo *ZRB* wanaifanya. Kwa upande wa *ZBS* ni taasisi ya viwango inahusika na ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini kuwa yanakidhi viwango viliovyowekwa kwa nchi na kimataifa. Kwa hiyo, kila taasisi inahusika na kazi yake kwenye biashara ya mafuta. Lakini kwa udhibiti bado itaendea *ZURA* kuwa ndio mdhibiti wa hiyo shughuli.

Mhe. Naibu Spika, pia aliuliza kwa sababu Zanzibar huku tusha *declare* suala zima la Mangapwani kwamba ni suala la mafuta na gesi, kule kutajengwa matangi kwa sababu ya kuhifadhia mafuta, na akauliza kule Pemba je inakuwaje. Kwa upande wa Pemba bado tutatumia Wesha itakuwa ni sehemu ya kuhifadhia mafuta, yaani mafuta baada ya kutoka Mwangapwani yatakwenda kwenye matangi ya Wesha. Sasa hivi ndio mpango ambao tumejipangia lakini kwa

sababu ametaka kujua kwa baadaye pia tutangalia namna gani basi serikali tutaweza kupitia *ZURA* tutaweza kujipanga.

Vile vile alizungumza kuhusu suala zima la uajiri wa wanafunzi ambao wanasoma mafunzo haya *oil and gas* ambao wako masomoni. Mhe. Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mhe. Omar Seif Abeid kwamba sisi kazi yetu tunaratibu tunawajua wanafunzi wote na tunawaandikia Tume ya Utumishi kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa sababu wao ndio wenye mamlaka ya kuajiri, sisi tunachofanya ni kuwandikia na kupeleka maombi kwa sababu ya kupatiwa ajira.

Lakini nimalizie labda nizungumzie swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu suala la Michamvi tayari nimelijibu. Lakini naomba nimwambie kwamba ahadi zote zilitolewa na Mhe. Rais.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, unakaribia kumaliza au vipi, kwa sababu muda wetu unakaribia kumalizika. Sasa kama bado una masuala mengi unamaliza, bado dakika tano. Kwa hiyo, naomba uzitumie hizo kwa kumalizia.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, namalizia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nataka kumfahamisha kwamba suala hili la Michamvi kama nilivyolieza mwanzo tunalifanyia kazi. Lakini ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar tunaziraatibu na tutazitekeleza ndani ya miaka mitano, naamini ifikapo 2020 suala hili tayari tutakuwa tumelikamilisha kwa sababu tayari kisima na matangi tayari yako pale.

Lakini, alizungumzia suala la hati. Kweli zile hati zikija tunazisaini lakini zikitoka pale zina utaratibu wake ndani ya Kamisheni ya Ardhi ambao unafanyika, na ndio maana anakuja kwangu anakuta haipo lakini akienda kule anaambiwa utaratibu haujakamilika.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukuwe pongezi ambazo Mhe. Panya Ali Abdalla amezitoa pongezi tumezipokea. Vile vile, tutaongeza juhudi katika maeneo yale ya upimaji hasa katika hii sekta ya *ZAWA* alozungumza, lakini hata hili la *ZECO* ambalo tunalifanyia kazi kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, basi pia nakuhakikishia kwamba tunaendelea kulifanyia kazi, lakini juhudi tutaendelea kuchukua kama alivyosema.

Mwisho kabisa ni suala la ndugu yangu Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma ambaye amelizingumzia suala la kuongezwa idadi ya wanafunzi wanaosoma mafunzo haya ya mafuta na gesi asilia. Kwa kweli, suala tumelipokea na linalifanyia kazi na tunatoa wito kwa wananchi hasa wanafunzi na vijana kuji *engage* katika suala hili na kuomba masomo ambayo yanalingana na somo hili.

Baada aya hayo Mhe. Naibu Spika naomba nikushukuru sana, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, ambao wameweza kutoa michango yao kwa ufasaha.

Mhe. Naibu Spika, kuna jibu moja ambalo naomba niliseme mwisho kidogo sasa hivi haraka haraka, kwamba kuna maeneo 34 upande wa Unguja Kaskazini Unguja ambayo katika yake

maeneo yake ya wawekezaji ambayo hayaendelezwa, liliuliza hili swali nilikuwa sikulijibu. Lakini naomba nimeliweka mwisho hivyo kuna maeneo 34 ambayo bado hayajaendelezwa na orodha kamili tunayo. Kwa hiyo, bado tunaendelea kuyafanyia kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu na yale maagizo ambayo yametolewa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kukushukuru sana naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale ambao tuliyopokea taarifa wanyooshe mikono. Ahsanteni nawashukuru sana *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa utulifu wenu pamoja na michango. Kwa hiyo, sasa hivi nasitisha kikao hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11: jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Ripoti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutuwezesha kwa mara nyengine tena kukutana tukiwa wazima wa afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi kubwa ya ufatiliaji wanayoifanya na kuwapa maelekezo na miongozo yao katika kuendeleza malengo ya kukuza biashara, viwanda na masoko hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imepokea jumla ya maagizo 50 kutoka kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi ambayo yalitakiwa kutolewa ufafanuzi na utekelezaji wake kutoka katika kila idara na taasisi zake. Maagizo hayo yanajikita katika maeneo ya ukaguzi wa bidhaa, maendeleo ya viwanda na ujasiriamali, ukaguzi wa mizani na vipimo

katika vituo vya mafuta na maduka, masuala yanayohusiana na karafuu pamoja na Kiwanda cha Makonyo na masuala mengine ya utunzaji na usimamizi wa biashara.

Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa baadhi ya utekelezaji wa maagizo haya kama ifuatavyo.

Ukaguzi wa bidhaa

Mhe. Mwenyekiti, eneo moja ambalo limetakiwa kutolewa ufafanuzi na kamati ni kuhusiana na utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi (*Pre Verification of Conformity – PVOC*) kwa kuangalia upya mgao uliopo wa asilimia 30 wanayoipata Taasisi ya Viwango na asilimia 70 wanayoipata Mawakala.

Kamati ilielezwa kwamba katika ya miundombinu na vifaa vya maabara pamoja na uwezo wa kitaalamu uliopo *ZBS* kwa hivi sasa inalazimika kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zinakuwa salama kwa afya za wanaotumia na mazingira ya Zanzibar.

Usajili wa Viwanda

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo lilitakiwa kutolewa ufafanuzi na kamati ni suala la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na kuliondosha suala la usajili wa viwanda katika serikali hiyo na kulibakisha katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati ilielezwa kwamba suala la usajili wa viwanda ni la Katiba, hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Tanzania Bara ili kuangalia njia bora ya kuweza kulitekeleza suala hili.

Utafiti wa Karafuu za Tanzania Bara

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilitakiwa kutoa ufafanuzi kuhusina na masuala ya kufanya utafiti wa kina juu ya karafuu zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara kwa Soko la Karafuu la Zanzibar. Kamati iliarifiwa kwamba utafiti wa karafuu za Morogoro na Tanga tayari umeshafanyika na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo taarifa hiyo imeshawasilisha serikalini na uingizwaji wa karafuu hizo hapa Zanzibar ulipigwa marufuku.

Kuwekwa Mashine za Kusafisha Karafuu Kisiwani Pemba

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuweka mashine za kusafishia karafuu Kisiwani Pemba nalo lilitakiwa kufanyika kwa sababu uzalishaji mkubwa wa karafuu hufanyika huko na pia litapunguza gharama na kuondoa mzunguko usio wa lazima.

Kamati ilielezwa kwamba Shirika limefikiria suala hilo na mara tu zitakapopatikana mashine nyengine katika bajeti zijazo zitanunua mashine nyengine tatu na kuziweka Pemba. Hata hivyo,

kwa mujibu wa taratibu za kusafirisha karafuu nje, hata kama karafuu zilizosafishwa zitatoka Pemba zikifika Unguja ni lazima zimwagwe ghalani na kukaguliwa kabla kupelekwa nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipokea ufafanuzi na majibu ya hoja ambazo zilijibiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kusisitiza usimamiaji wa shughuli zinazotekelezwa na wizara ili kuleta tija kwa taifa na kufikia malengo ambayo yamewekwa ya kukuza biashara, viwanda na kuendeleza masoko hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nije kutoa maelezo kutokana na hoja zote 50 kama ifuatavyo kwenye bango kitita.

Agizo Nam.1. Marekebisho ya Sheria ya Biashara yafanyike ili kuipatia fursa Taasisi ya Viwango (*ZBS*) kufanya Ukaguzi wa bidhaa zote zinazozalishwa ndani na zinazoingizwa nchini.

Utekelezaji

Sheria imo kwenye majadiliano ya ndani kwa mazingatio na kuchukuliwa hatua muafaka. Aidha, Sheria ya Viwango Na.1 ya 2011 ya Zanzibar nayo imeshaanza kupitiwa ili kubaini maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa kazi za msingi za ZBS ikiwemo ukaguzi wa bidhaa.

Agizo Nam.2. Kamati inashauri *ZBS* kubuni miradi mbalimbali ili kukabiliana na tatizo kubwa la uhaba wa vifaa linalowakabili.

Utekelezaji

ZBS tayari imeshaanza na inaendelea na hatua za utayarishaji wa kubuni miradi ili kukabiliana na kuliondoa tatizo hilo. Hadi sasa dhana za miradi mitatu kuhusu ujenzi na vifaa zimeandaliwa. Juhudi za kupata wadau na usaidizi zinaendelea kuchukuliwa. Ikiwemo kuimarisha *ZBS*.

Agizo Nam.3. Kamati inaitaka wizara kupitia *ZBS* wazitumie ipasavyo fursa zinazopatikana kwenye Shirika la Viwango la Afrika.

Utekelezaji

Kwa sasa *ZBS* ni mwanachama mwangalizi wa Shirika la Viwango la Afrika (*ARSO*) inatarajiwa kupata fursa nyingi za kiufundi, kiutaalam na itaendelea na ufuatiliaji ili kuhakikisha inanufaika na fursa hizo ipasavyo. Fursa ambazo zinazohusu upatikanaji na utumiaji wa Viwango vya Afrika, kushiriki katika Kamati za uandaaji wa viwango vya Afrika, kuwajengea uwezo wa kitaalamu maofisa husika, kubadilishana uzoefu na mawazo katika mambo ya kiufundi na Mashirika ya Viwango ya Afrika ambayo ni wanachama wa Shirika hilo. Hadi sasa mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo kuhusu viwango kupitia *ARSO*.

Agizo Nam.4. Wizara itafute suluhisho la upungufu wa watalaamu unaiokabili *ZBS* ili kuweza kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Utekelezaji

Taasisi imekamilisha kazi ya uajiri wa wafanyakazi kumi (10) mmoja kwa Pemba na tisa (9) kwa Unguja na wamo kwenye hatua za ukamilishaji kwa mwaka 2016/2017 na imepeleka maombi Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa maombi ya nafasi 14 kwa mwaka 2017/2018.

Agizo Nam.5. Utaratibu wa *PVOC* uangaliwe upya kwani hali ya sasa ya mgao wa asilimia 30 ya mapato kwa shirika na asilimia 70 kwa wakala inayoendesha ukaguzi huo hairidhishi kutokana na Zanzibar kupata kiwango kidogo cha fedha.

Utekelezaji

Utaratibu huu wa Taasisi kupata mgao mdogo utaondoka pale ambapo *ZBS* itakuwa na uwezo wa maabara zake mwenyewe zitakazo weza kupima bidhaa zinazoingia hapa Zanzibar pamoja na wataalamu mahiri. Katika hali ya miundombinu na vifaa vya maabara pamoja na uwezo wa kitaalamu uliopo *ZBS* inalazimika kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zinakuwa salama kwa afya za wanaotumia na mazingira ya Zanzibar.

Agizo Nam.6. *ZBS* ibuni miradi ndani ya Shirika ili kuweza kupata ufadhili wa majengo ya maabara pamoja na mashine na vifaa vyengine vya maabara.

Utekelezaji

ZBS inaendelea na hatua ya kubuni miradi ambayo baadhi imeshawasilishwa serikalini na kuiwasilisha kwa wadau wengine wa ndani na nje ya nchi. Miradi mitatu tayari imeandikwa. Miradi hiyo inahusisha ujenzi na vifaa vya maabara ili kupata ufadhili utakaosaidia uimarishaji wa miundombinu na upatikanaji wa vifaa vyengine vya Maabara.

Agizo Nam.7. Serikali iwe na mpango wa kuanzisha maabara ya *ZBS* Pemba kwani kumekuwa na malalamiko kwa waingizaji na wazalishaji bidhaa kuchelewa kwa majibu ya sampuli kutoka *ZBS.*

Utekelezaji

ZBS imeshafungua Ofisi yake Pemba na kuanza kazi rasmi. Aidha, mpango wa kuanzisha maabara za *ZBS* Pemba uko katika maandalizi ambapo mazingatio ya maabara za kuanzia yanaendelea. Aidha, hatua ya utekelezaji utategemea na upatikanaji wa rasilimali fedha na wataalamu ambapo juhudi za kuwajengea uwezo wataalamu zinaendelea kwa kutolewa mafunzo husika.

Agizo Nam.8. Serikali iweke bajeti maalum ya wajasiriamali ili iweze kuwasaidia katika kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Utekelezaji

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na kufanya tathmini ya mahitaji pamoja na utaratibu muafaka wa kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuweza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao. Aidha, wizara pamoja na *ZBS* inaendelea na juhudi za kuwawezesha wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye kuzingatia viwango na kufikia ubora unaotakiwa ili kuimarisha masoko ya bidhaa zao.

Agizo Nam.9. Wizara ishirikiane na Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*) katika kuimarisha suala la uwekezaji katika viwanda;

Utekelezaji

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina mashirikiano ya karibu na Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*) katika nyanja mbali mbali zikiwemo kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar, hasa katika nyanja za viwanda na biashara. Wizara inashiriki kikamilifu katika uchambuzi wa maombi ya uwekezaji wa miradi ya viwanda yanayopelekwa *ZIPA*. Mashirikiano hayo pia yapo katika kuisaidia miradi ya viwanda, kwa mfano kiwanda cha sukari Mahonda, kutatua changamoto zinazokabili miradi hiyo ili iweze kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

Agizo Nam.10. Sera na Sheria zifanywe haraka ili ziweze kutumika na ziweze kuwavutia wawekezaji.

Utekelezaji

Sera ya viwanda ya mwaka 1998 ya Zanzibar inafanyiwa mapitio makubwa kwa lengo la kupata Sera mpya inayoendana na mahitaji ya wakati huu. Kazi hiyo inafanywa na kikosi kazi cha wataalamu 16 kutoka sekta za umma na binafsi kwa mashirikiano na msaada wa kitaalamu na kifedha wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*). Vile vile kwa msaada wa Shirika hilo la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*), Wizara imeifanyia mapitio Sera ya Ujasiriamali ya mwaka 2006 (*Zanzibar SME Policy 2006*), na Rasimu ya Sheria ya kuanzisha Wakala wa kusimamia Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo na vya kati imbayo itawasilishwa Baraza kwa ajili ya kutungwa Sheria hiyo.

Agizo Nam.11. Ili tuweze kuimarisha viwanda vya ndani, unahitajika uzalishaji mkubwa wa bidhaa ili ziweze kutosheleza mahitaji ya viwanda vya ndani;

Utekelezaji

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika juhudi za kuimarisha uzalishaji na usarifu wa mwani, chumvi, dagaa, sukari na viungo. Miongoni mwa juhudi hizo ni kuimarisha muundo na utendaji wa Jumuia ya Wazalishaji Chumvi (*AZASPO*) pamoja na kusaidia katia usarifu na utafutaji wa masoko ya kudumu ya chumvi, upatikanaji wa maeneo zaidi ya kulimia miwa, usarifu wa mwani na dagaa na *branding* ya karafuu na baadhi ya viungo.

Agizo Nam.12. Serikali ifanye mazungumzo ili suala la usajili wa viwanda libaki katika Serikali ya Zanzibar badala ya viwanda kusajiliwa Tanzania Bara;

Utekelezaji

Hivi sasa viwanda vinasajiliwa na kusimamiwa na mamlaka tofauti za Zanzibar zikiwemo Mamlaka ya Vitega Uchumi (*ZIPA*), Halmashauri n.k. Kwa kuwa suala la usajili wa viwanda ni la kikatiba ingawa sera ya kusimamia viwanda sio suala la muungano, wizara inaendelea kufanya mazungumzo na taasisi za Bara ili kuangalia namna ya utakelezaji mzuri na kuendelea suala hili kubaki Zanzibar.

Agizo Nam.13. Kwa nia ya kukiimarisha zaidi kiwanda hichi, serikali inapaswa kuwapatia ardhi ya kutosha wawekezaji hawa ili waweze kuzalisha miwa ya kutosha na hatimae kulifikia lengo la uzalishaji wa kutosheleza soko la ndani na kusafirisha nje ya nchi kwa maslahi ya Taifa;

Utekelezaji

Serikali imeridhia utaratibu wa kutumia sehemu za mashamba ya vikosi vya SMZ kulimwa miwa na wapiganaji wa vikosi hivyo, na miwa hiyo kuuzwa kwa kiwanda cha sukari. Maeneo hayo ni ekari 38 katika shamba la JKU Upenja, ekari 20 za shamba la KVZ Pangatupu na ekari 29 za shamba la Vyuo vya Mafunzo Kinumoshi. Vilevile wananchi binafsi wameanza kushajiika kulima miwa katika mashamba yao na kuiuza kiwandani.

Agizo Nam.14. Kamati inaiagiza wizara kusimamia ipasavyo urejeshwaji wa nyumba za kiwanda ambazo zinatumika kwa shughuli mbalimbali kama makaazi ya watu wasiohusika ili zirudishwe kwenye mamlaka ya kiwanda na kuondoa usumbufu uliopo wa makaazi ya wafanyakazi.

Utekelezaji

Hatua za urejeshaji wa nyumba za Kiwanda cha Sukari Mahonda zinaendelea. Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri akiwemo Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko (Mwenyekiti), Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu kushughulikia suala hili. Kamati ya Wataalamu iliundwa chini ya Mwenyekiti wake Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini “B”, na kupewa kazi ya kutathmini nyumba hizo kwa kina. Kamati ya wataalamu imekamilisha kazi yake na kuwasilisha ripoti ya tathmini kwa Kamati ya Mawaziri kama ilivyotakiwa. Wakati Kamati ya Mawaziri inaendelea na kazi zake, tayari nyumba 18 zimeshakabidhiwa kiwanda cha sukari na zinatumiwa na wafanyakazi wa kiwanda hicho. Wizara itaendelea kusimamia.

Agizo Nam.15. Kamati inaitaka wizara kupeleka maombi maalum kwa serikali juu ya haja ya kukifanyia matengenezo makubwa kiwanda hicho ili kwenda sambamba na teknolojia ya uzalishaji duniani na kukidhi matakwa ya soko la ndani.

Utekelezaji

Kiwanda cha Sukari kimeshafanyiwa matengenezo makubwa na kwa sasa kina uwezo wa kukamua miwa kutoka tani 400 hadi tani 800 kwa siku.

Agizo Nam.16. Wizara ichukue hatua za makusudi za kuthibitisha uuzwaji wa mafuta ya makonyo kwa watu wasio waaminifu ambao huyanunua mafuta hayo kwa kiwango kikubwa na kuyachakachua na baadae kuyauza nje kwa njia zisizo halali. Kuendelea kwa biashara hii haramu kutapelekea kushuka kwa baadhi ya mafuta yetu kwenye soko la kimataifa na kuathiri uchumi wa Taifa letu.

Utekelezaji

Wizara kupitia Shirika la *ZSTC* tayari imeshachukua hatua za kuyafanyia usajili mafuta yote ya mimea yanayozalishwa Kiwanda cha Makonyo kwa kuyapa majina mapya. Hati za usajili zenye nambari TZ/T/2016/13 hadi TZ/T2016/21 za tarehe 07/1/2016 kutoka kwa Msajili wa Alama za Biashara Tanzania zinahusika na usajili huo. Kutokana na usajili huo mafuta hayo kwa sasa yapo salama na hayaghushiwi kwa kutumia majina yaliyosajiliwa.

Agizo Nam.17. Ipo haja kwa serikali kukiangalia kwa jicho la huruma kiwanda hicho na kukiandalia mpango maalum wa kupata umeme nafuu utakaowezesha kufanyika uzalishaji wa umeme utakaowezesha kufanyika uzalishaji kwa gharama zinazokubalika, utafiti unapaswa kufanywa juu ya njia ipi ya uzalishaji wa umeme utakiwezesha kiwanda hicho kufikia malengo yake (ya kuzalisha bidhaa bora kwa bei nafuu) ili kuweza kuhimili ushindani wa biashara uliopo katika soko.

Utekelezaji

Shirika lina mpango wa kuzungumza na *ZECO* kuangalia namna watakavyosaidia au kutoa viwango nafuu kwa viwanda kwa vile ndio dira ya nchi. Aidha, hatua zitachukuliwa kufanya utafiti wa kuangalia njia mbadala ya kuzalisha umeme nafuu.

Agizo Nam.18. Kiwanda kiendelee kujitangaza kupitia vyombo mbali mbali ndani na nje ya nchi ili kiweze kuwa na soko kubwa la bidhaa zake.

Utekelezaji

Kupitia vyombo mbali mbali vya kujitangaza tayari shirika limewasiliana na wateja wan chi za Ufaransa, India, Dubai, Pakistan, China na Uingereza ili kuweza kuyauza mafuta. Matokeo ni kwamba tatizo la soko kwa sasa halipo. Soko limepatikana sehemu mbalimbali ikiwemo China.

Agizo Nam.19. Kamati inaitaka wizara kuendelea kutoa taaluma kwa wajasiriamali ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na ziweze kuingia katika soko la ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji

Ujuzi na taaluma ya uzalishaji bidhaa bora umekuwa ukitolewa kwa wajasiramali mara kwa mara kupitia Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*), Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na taasisi binafsi zinazojishughulisha na masuala ya ujasiriamali. Taaluma zinazotolewa ni pamoja mbinu za uzalishaji, viwango vya bidhaa, umuhimu wa kutumia vifungashio kwa bidhaa, taaluma ya ujasiriamali.

Agizo Nam.20. Serikali iongeze bajeti ya wajasiriamali kwa kutoa mikopo ya kutosha, kwani wajasiriamali wanachangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Utekelezaji

Kupitia mfuko wa uwezeshaji Taifa, serikali imekuwa ikitoa mikopo ya viwango mbali mbali kwa wajasiriamali kwa lengo la kukuza miradi yao ili kujiongezea kipato na kuchangia katika pato la Taifa. Mfuko wa uwezeshaji ulianza na kiasi cha fedha shillingi 1,573 milioni lakini kupitia mfuko wa AK/JK mtaji wa mfuko uliongezeka na kufikia bilioni 2.313/=. Hadi kufikia 31 Disemba 2015, jumla ya mikopo 727 yenye thamani ya shilling 1,251.6 milioni ilitolewa kwa wajasiriamali mbalimbali nchini.

Agizo Nam.21. Wizara ya Biashara ifanye tathmini ya bidaha zinazozalishwa kwa wingi nchini na kuona ni namna gani wanaweza kulinda bidhaa za ndani ikilinganishwa na bidhaa zinazoingizwa kwa lengo la kuwainua na kuwatia moyo wazalishaji wa ndani.

Utekelezaji

Wizara inathamini mchango wa wazalishaji wa ndani kwa vile unachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa na ni wajibu wa serikali kuwalinda na kuwapatia soko kwa bidhaa za ndani pamoja na kulinda viwanda vyetu. Wizara itaweka mikakati ya kulinda bidhaa za ndani na kuongeza thamani.

Agizo Nam.22. Wizara iandae maonesho mbali mbali ili wajasiriamali wapate kuonesha bidhaa zao na kuzitangaza ili waongeze masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Utekelezaji

Wizara katika kusimamia suala hili inaandaa Tamasha kubwa la biashara la kila mwaka kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali kuzitangaza bidhaa zao na kupata masoko ya ndani na nje. Aidha, wizara inaratibu maonesho ya kimataifa ya sabasaba ya kila mwaka yanayofanyika Tanzania Bara kwa lengo lilelile la kuwawezesha wajasiriamali kutafuta masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi. Agizo la kuwa na ratiba ya maonyesho ya kitaifa ya Zanzibar kwa kila mwaka linafanyiwa kazi ili iweze kusaidia soko kwa wajasiriamali.

Agizo Nam.23. Kutokana na uzalishaji mkubwa wa bidhaa za kilimo nchini ambazo huzalishwa na wakulima pamoja na wajasiriamali, kuna haja ya kuwa na kiwanda cha kusarifu mazao kwa upande wa Pemba na Unguja.

Utekelezaji

Katika miaka ya karibuni kumekuwa na muamko mkubwa wa wananchi katika kuzalisha bidhaa nyingi za kilimo ambazo wakati wa kilele cha misimu ya uvunaji wake hupelekea kushuka sana bei au hata kuharibika kwa sehemu kubwa ya mazao hayo. Suluhisho la kudumu kwa matatizo hayo ni kuwa na viwanda vya kusarifu mazao hayo.

Suluhisho la kudumu kwa matatizo hayo ni kuwa na viwanda vya kusarifu mazao hayo. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuongeza ubora na kurahisisha uwekezaji wa viwanda ikiwa ni pamoja na kuweka vivutio vizuri chini ya Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*) na kufanyiwa mapitio Sera ya Viwanda ya mwaka 1998. Serikali itaendelea kuchukua hatua hizo za kuongeza ubora, mazingira ya uwekezaji pamoja na kuwahamasisha zaidi wawekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Kwa upande mwengine uzalishaji wa matunda na mazao mengine ya kilimo (ukiwacha mwani) bado havitoshelezi mahitaji ya viwanda viweze kufanya kazi kwa kipindi kirefu cha mwaka na kuleta faida kwa mwekezaji. Kwa mantiki hiyo, inafaa wananchi waongeze uzalishaji wa bidhaa hasa za kilimo ili wawekezaji washawishike kuanzisha viwanda vya kusarifu bidhaa hizo.

Agizo Nam. 24. Kutokana na kubainika kwa kemikali zinazotokana na dawa ya mbu inayopulizwa majumbani kwenye bidhaa za viungo (*spices*) zilizosafirishwa nchini Ujerumani, kamati inaitaka Wizara ya Biashara kuhakikisha kwamba, bidhaa zote za viungo zinazozalishwa zinapelekwa *ZBS* kwa ajili ya ukaguzi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi ili kulinda hadhi za bidhaa hizo na jina la Zanzibar kwenye soko la kimataifa.

Utekelezaji

Kutokana na kubainika kwa kemikali zinazotokana na dawa za kunyunyiza, Shirika mapema mwezi Juni, 2017 na Julai, 2017 lilifanya mikutano miwili iliyowajumuisha wataalamu kutoka Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *Zanj Spice* ya Zanzibar, Idara ya Misitu Zanzibar, Kitengo cha Ufukizaji Dawa Zanzibar, *TAZOP* Zanzibar, *ZBS* na Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar; kulishughulikia suala hilo ili kuhakikisha kwamba changamoto hio inaondoka haraka.

Agizo Nam. 25. Wizara kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika iwe na mpango maalum wa kuimarisha soko la bidhaa zinazozalishwa ndani

Utekelezaji

Wizara inashirikiana na taasisi mbali mbali katika kuongeza ubora bidhaa zinazozalishwa ndani kwa lengo la kupata masoko ya bidhaa zao. Miongoni mwa taasisi hizo ni Jumuiya ya

Wafanyabiashara, Wenyeviwanda na Wakulima ambao wamepatiwa vifaa maalum kwa ajili ya kutoa Misimbomilia (*Barcode*) ili kuziweka katika ubora unaotakiwa.
Aidha, wizara inafanya mafunzo maalum kwa wafanyabiashara ambayo huwawezesha kuyatumia masoko kwa ajili ya kuzitangaza bidhaa zao. Pamoja na hayo, wizara inaandaa maonesho ya biashara kama vile Sabasaba, Juakali, Tamasha la Biashara kwa lengo la kuweza kutangaza bidhaa za ndani.

Agizo Nam. 26. Wizara iendelee kutoa ushirikiano mkubwa kwa wakulima wa mwani kwani bei ya zao hili bado ipo chini kulinganisha na soko la mwani duniani

Utekelezaji

Ili kuimarisha uzalishaji na bei ya mwani, serikali imechukua hatua zifuatazo:

i. Kamati ya kitaifa imeundwa chini ya Afisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuangalia maendeleo, mafanikio na changamoto za zao la mwani, pamoja na kupendekeza njia mwafaka za kukuza uzalishaji na bei ya zao hilo kwa manufaa ya wakulima na taifa kwa jumla. Kamati hiyo ina ngazi ya mawaziri na ya wataalamu. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni mshiriki katika ngazi zote mbili za kamati hiyo. Taarifa ya awali ya Kamati ya mawaziri imeshawasilishwa serikalini.

ii. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Baharini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*), inaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji katika kusarifu na kuongeza thamani zao la mwani. Tayari amejitokeza mwekezaji mmoja ambae sasa anatayarisha andiko la mradi wake.

iii. Kwa mwaka huu wa fedha, wizara imetengewa fedha za kuweka angalau kiwanda cha kusindika mwani**.**

Agizo Nam. 27. Wizara iongeze nguvu ya ukaguzi wa mizani kwani kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi juu ya udanganyifu wa vipimo halisi vya mizani.

Utekelezaji

Katika kutekeleza suala hili wizara hufanya ukaguzi kwa wafanyabishara wote wanaotumia mizani pamoja na taasisi zinazotumia mizani kubwa kama vile Bandarini na *ZSTC,* kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa mizani hizo zinapima kwa usahihi.

Agizo Nam. 28. Mezani zinazoingia nchini zianze kukaguliwa kabla ya kuanza kutumika ili kubaini ubora wake mapema

Utekelezaji

Kwa mujibu wa Sheria ya Mizani na Vipimo nambari 4 ya mwaka 1983 inataka mizani ya mfanyabiashara yoyote kabla ya kuanza kutumika hufanyiwa uhakiki ili kujua kama inapima kwa usahihi na kuepusha udanganyifu kwa mtumiaji.

Agizo Nam. 29. Wizara ichukuwe hatua kwa watakaobainika kufanya udanganyifu katika mizani zao.

Utekelezaji

Wizara hufanya kazi zake za ukaguzi wa mizani kwa kutumia Sheria yake ya Mizani na Vipimo ya mwaka 1983. Sheria hii imeweka adhabu maalum kwa wale wote ambao watafanya udanganyifu katika matumizi ya mizani na vipimo vyengine.

Agizo Nam. 30. Wizara ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa bidhaa ambazo zimeshapakiwa ili kujiridhisha kuwa zinafikia uhalisia wa ujazo wake kwani tayari kuna malalamiko kuwa bidhaa za vipolo vyenye ujazo wa kilo 25 na 50 huwa hazifikii ujazo huo

Utekelezaji
Wizara kwa kusimamia suala hili huwa inafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinauzwa na ujazo ulio sahihi na mfanyabiashara hawafanyi udanganyifu. Aidha Wizara imo katika hatua za kuanza kuzifanyia ukaguzi bidhaa zilizofungashwa katika viwanda na maeneo ya bishara.
Agizo Nam. 31. Kamati inaitaka wizara kufanya thamani ya maghala yote yaliyo chini yake ili kufahamu hali yake na kubuni mbinu sahihi ya matumizi yake

Utekelezaji

Wizara imeshakamilisha tathmini ya maghala yote.

Agizo Nam. 32. Wizara ihakikishe mtu anaekodishwa ghala ndie anaepaswa kutumia ghala hilo akishindwa kulitumia alirudishe.

Utekelezaji

Suala hili linaendelea kufanyiwa kazi.

Agizo Nam. 33. Utaratibu wa ukodishaji wa maghala uwe wa wazi.

Utekelezaji

Wizara kwa sasa imebaini kuwa maghala yote yamekodishwa, Mikataba itakapomalizika itatumia Sheria ya Manunuzi katika kukodisha maghala.

Agizo Nam. 34. Wizara ifanye mapitio ya bei zinazokodishwa maghala na ihakikishe kuwa bei ya ghala iendane na hali ya ghala na sehemu liliopo ghala hilo husika.

Utekelezaji

Wizara imeanza kutumia bei mpya ya ukodishwaji wa maghala kwa kutumia mfumo wa zabuni.

Agizo Nam. 35. Wizara iandae mpango maalum wa kupitia kodi zinazotokana na maghala, kuyafanyia matengenezo maghala yote ambayo hali yake ni mbaya.

Utekelezaji

Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa ukodishwaji kulingana na bei ya soko (*Market Price*). Aidha, wizara imeyafanyia matengenezo baadhi ya maghala yake.

Agizo Nam. 36. Kamati inaitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kufanya utafiti wa kina juu ya karafuu zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara kwa Soko la Karafuu Zanzibar.

Utekelezaji

Utafiti wa karafuu za Morogoro na Tanga tayari umeshafanyika ambapo ulifanywa na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo taarifa hiyo imeshawasilishwa serikalini kwa hatua.

Aidha, suala la uingizwaji wa Karafuu kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar mapema mwaka 2015/2016 liliripotiwa Serikali Kuu na kuwekwa marufuku kwa bidhaa hiyo kuja Zanzibar. Kwa sasa tatizo hilo bado halijagundulika katika vituo vya ununuzi karafuu hapa Zanzibar.

Agizo Nam. 37. Kamati inaishauri wizara kupitia Shirika la *ZSTC* kuajiri mtu wa kudumu wa shirika ambae atakuwa ni mkaguzi wa zao la karafuu ili kuepusha mivutano ya Wakaguzi wa Wizara ya Kilimo na Watu wa Shirika

Utekelezaji

Kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Mazao ya Kilimo Zanzibar “Plant Protection Act Namba 9 ya mwaka 1997, Mamlaka ya Upasishaji, Ukaguzi wa Mazao ya Kilimo yapo kwa Wizara ya Kilimo tu. Hata hivyo, Shirika la *ZSTC* limekuwa likiweka watu wake kila kituo ili kuhakikisha kwamba upasishaji unafuata taratibu zilizopo kisheria.

Agizo Nam. 38. Kamati inaitaka Wizara kupitia Shirika la *ZSTC* kuweka mashine za kusafishia karafuu Kisiwani Pemba, ambako uzalishaji mkubwa wa karafuu hufanyika. Jambo ambalo litapunguza gharama na kuondoa mzunguko usio wa lazima.

Utekelezaji

Shirika limefikiria suala hilo na mara tu zitakapopatikana mashine nyengine katika bajeti zijazo litanunua mashine nyengine tatu na kuziweka Pemba. Hata hivyo, kwa mujibu wa taratibu za

kusafirisha karafuu nje, hata kama karafuu zilizosafishwa zitatoka Pemba zikifika Unguja ni lazima zimwagwe ghalani na kukaguliwa kabla kupelekwa nje ya nchi.

Agizo Nam. 39. Katika suala zima la usimamizi na uendelezaji wa zao la Karafuu, kamati inashauri Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo kuangalia namna bora ya kuchagua miche ya mikarafuu kabla ya upandaji wake. Pia, wizara hizi zinapaswa kufanya mazungumzo ya kitaalamu yatayopelekea kupatikana kwa namna bora ya uoteshaji wa zao la karafuu, kwani kamati imebaini kuwa miche mingi inayotolewa kwa Wakulima inakufa.

Utekelezaji

Shirika la Biashara la Taifa, *ZSTC* kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima wa kafaruu kuhusiana na upandaji wa miche ya mikarafuu.

Agizo la 40. Serikali ipige marufuku na ihakikishe inasimamia uuzaji wa karafuu za kikombe ili kudhibiti wizi wa karafuu.

Utekelezaji

Shirika kupitia katika mikutano mbali mbali ya Wakulima na Wadau wa Karafuu iliyofanyika mwezi Mei, 2017 kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa yote ya Pemba na kwa upande wa Unguja Mkoa wa Kaskazini na Kusini wameshafikisha ujumbe huo kwa wadau wote wa karafuu, ambapo pamoja na mambo mengine suala la ununuzi wa karafuu kwa vikombe limekatazwa kupitia mikutano hiyo ambayo Masheha ni sehemu ya washiriki walioalikwa.

Agizo Nam. 41. Shirika litoe taaluma kwa Wakulima wa karafuu wanaootesha miche kwenye vitalu kwa ajili ya kuliuzia Shirika, juu ya msimamo wa Shirika katika ununuzi wa miche hiyo ili kuondoa malalamiko ya Wakulima kwa Shirika kukataa miche yao.

Utekelezaji

Shirika kupitia katika mikutano mbali mbali ya Wakulima na Wadau wa Karafuu iliyofanyika mwezi Mei, 2017 tayari Wakulima walileta malalamiko hayo na ambapo Maafisa kutoka Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na *ZSTC* wamelichukua hilo kulipeleka katika taasisi zao na kuahidi kulifanyia kazi ili kasoro hizo ziweze kurekebishwa na kujua njia bora za kufuatwa ili wakulima wafaidike na miche iliyo bora.

Agizo Nam. 42. Ili kuweza kuingia katika ushindani wa Kimataifa na kuifanya karafuu ya Zanzibar iwe na hadhi ya kipekee, Shirika kupitia wizara liharakishe kukamilika kwa (*Branding*) ya karafuu ya Zanzibar.

Utekelezaji

Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa *ZSTC* 2016 -2019 lipo pia suala la "*Branding*" na ambapo mpango huo unakwenda kwa awamu tofauti kwa mujibu wa mpango huo wa utekelezaji.

Agizo Nam. 43. Kamati inalitaka Shirika la *ZSTC* kuandaa mipango madhubuti ya kuendeleza Kilimo cha viungo (*Spices*), kwani imebainika kuwa soko la bidhaa hizo ni kubwa duniani na hadi sasa Zanzibar hatujaitumia fursa hii kikamilifu.

Utekelezaji

Shirika kupitia katika mikutano mbalimbali ya Wakulima na Wadau wa Karafuu iliyofanyika mwezi Mei, 2017 tayari ujumbe huo umefikishwa kwa wakulima wote wa Zanzibar, kwamba walime mazao ya viungo soko lipo sasa hivi. Shirika liko tayari kuwasaidia kuwapa anuwani za wateja wa nje wanaohitaji viungo kama vile mdalasini, pilipili manga, pilipili hoho na viungo kama vile kungumanga, vanila na hiliki.

Agizo Nam. 44. Baraza lifanye mazungumzo na Wizara ya Utumishi wa Umma ili kuangalia namna ya kupatiwa wafanyakazi kutoka kwenye taasisi ambazo zina ongezeko la wafanyakazi.

Utekelezaji

Baraza limewasilina na wizara inayohusika na Utumishi wa Umma na imeomba kupatiwa wafanyakazi wa kada ya sheria, *ICT*, masjala, uhasibu, uchumi na biashara na mshika fedha. Baraza tayari limepatiwa Afisa Sheria na Mhasibu na linaendeleana mawasiliano kwa watumishi wengine.

Agizo Nam. 45. Katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa vitendea kazi, Kamati inalishauri Baraza kutumia fedha zake za matumizi ya kawaida (*OC*) ili kupunguza tatizo hilo hatua kwa hatua kwa kadri hali itakavyoruhusu.

Utekelezaji

Baraza katika Bajeti ya mwaka 2017/18 limetenga bajeti kwa ajili ya kununua vitendea kazi vikiwemo *computer* ya mezani, na *laptop*, scanner na photocopy. Aidha, Baraza lina mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya maendeleo ya Afrika kwa ajili ya vifaa hivyo ambao unatekelezwa katika bajeti hii.

Agizo Nam. 46. Baraza liweke utaratibu maalumu wa kuwachangia katika uendeshaji wa shughuli zake ili sekta zote mbili (Sekta ya Umma na Sekta Binafsi) zichangie gharama hizo ili, kuimarisha mfuko wa Baraza hilo

Utekelezaji

Baraza limeweka masharti kuzitaka mamlaka za utoaji leseni kulipa gharama za usimamizi (*regulatory fees*) na utaratibu wa malipo utazingatiwa katika bejeti zijazo.

Agizo Nam. 47. Kwa kuzingatia mifumo mbali mbali ya kodi iliyopo ulimwenguni, Baraza lichague mfumo sahihi wa usimamizi wa usoni utakaokwenda sambamba na mazingira ya biashara ya nchi yetu, ili kupunguza malalamiko kwa wafanyabiashara.

Utekelezaji

Mifumo mikubwa ya utoaji leseni inayotumika katika nchi zenye mazingira mazuri ya kufanya biashara ni leseni kutolewa sehemu moja na wa pili ni wa mamlaka tofauti chini ya usimamizi. Hivi sasa Zanzibar inatumia mfumo huu wa pili kama Rwanda na baada ya kufanya mageuzi ya utoaji leseni, wizara na *BLRC* itafanya tathmini ya utekelezaji wa mageuzi nakuamua mfumo bora zaidi.

Agizo Nam. 48. Baraza lichukue hatua za makusudi za kukuza mashirikiano na taasisi za usimamizi leseni za Tanzania Bara kama *TIRA* ili kupata uzoefu zaidi, hasa ikizingatiwa kwamba taasisi hizo zina uzoefu katika masuala haya.

Utekelezaji

Baraza liliandaa ziara ya kimafunzo katika Mamlaka tofauti za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano kama Wizara ya Viwanda na Biashara, *TCRA*, *SSRA*, SUMATRA na *BRELA* kwa ajili ya kupata uzoefu juu ya masuala ya usimamizi.

Agizo Nam. 49. Kamati inalitaka Baraza kujitangaza kwa kutumia vyombo vya habari kama redio na televisheni ili liweze kutambulika kwa jamii.

Utekelezaji

Baraza limeshaandaa vipindi vine ambavyo vimeanza kurushwa katika utekelezaji bajeti ya 2017/2018.

Agizo Nam. 50. Wizara ipeleke kibali maalum kwa wizara inayohusika na masuala ya utumishi ili kuomba uhamisho kwa baadhi ya wafanyakazi waliyomo katika taasisi ambazo kuna ongezeko kubwa la wafanyakazi au kuajiri wafanyakazi wapya ili Baraza liweze kutekeleza kazi ipasavyo.

Utekelezaji

Utekelezaji wa agizo hili ni sawa na agizo nambari 44 la waraka huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Ali Salum Haji (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nianze kusoma hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo

hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa min-ajil ya kuendelea na majukumu yetu ya uwakilishi wa Wananchi katika chombo hichi adhimu cha kutunga sheria nchini.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko yaliyotokana na ripoti yetu iliyowasilshwa ndani ya Baraza hili katika mkutano wa Tano uliofanyika mwezi Febuari, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu kabisa tunampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuiongoza vyema nchi yetu na kudumisha amani, utulivu na upendo tokea aliposhika wadhifa huo baada ya ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa marudio mwezi Machi, 2016 hadi leo. Tunamuomba Mola Mtukufu amzidishie hekima na busara na ampe maisha marefu ili tuzidi kupata fursa ya kunufaika na busara zake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd kwa namna anavyomsaidia Mhe. Rais katika kutekeleza shughuli mbali mbali za umma na kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za dhati ziende kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuanzia na Mhe. Waziri, Balozi Amina Salum Ali na watendaji wake wote kwa kutupatia majibu fasaha kwa maagizo ya kamati, pamoja na majibu mazuri wakati kamati inapohitaji kupatiwa ufafanuzi wa mambo mbali mbali. Aidha tunampongeza Katibu Mkuu mpya Ndugu Juma Ali Juma na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ali Khamis Juma, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa Biashara, Ndugu Bakari Haji Bakari, Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Ndugu Mohamed Jafar Jumanne na Ndugu Khamis Ahmada Shauri kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Biashara na kuteuliwa kwao na Mhe. Rais kushika nafasi hizo katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ina jumla ya wajumbe saba na makatibu wawili ambao kwa pamoja wametekeleza jukumu hili la kikanuni la kufuatilia utekelezaji wa maoni na maagizo ya kamati kwa wizara hii. Wahenga walisema “mcheza kwao hutunzwa”. Sina budi kuwatunza wajumbe hao kwa kazi nzuri waliyoifanya inayodhihirisha nyoyo zao za kizalendo walizonazo. Napenda muwatambue wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
4. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
5. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe
7. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu
9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia na utekelezaji wa agizo la kuwawezesha wajasiriamali, Kamati iliarifiwa kuwa sasa suala hili linasimamiwa na taasisi mbali mbali ikiwemo Wizra ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na hivyo kupelekea mgongano baina ya taasisi hizo. Hivyo, kamati inashauri mipango ya utaratibu wa uwezeshaji wananchi iliyoandaliwa kwa pamoja na wizara zote hizi kufanyiwa haraka ili kuzitumia rasilimali zilizopo kwa kuwanufaisha wajasiriamali wengi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuratibu matamasha ya maonesho mbali mbali nchini kwa nia ya kuwatangaza na kuwapatia masoko wajasiriamali wadogo wadogo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la kuwapatia masoko wajasiriamali hao. Aidha, kamati inashauri wizara itoe ratiba ya mwaka mzima ya matamasha mbali mbali yanayofanyika hapa nchini na kusisitiza haja ya kuwapatia wajasiriamali hao utaalamu wa vifaa kwa ajili ya kusarifu vizuri bidhaa zao ili kumudu ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa agizo la kuyadhibiti mafuta ya makonyo, wizara inaendelea na utafiti ili kuwabaini wanunuzi wasio waaminifu wanaonunua mafuta hayo kwa wingi na kuyauza nje ya nchi kwa faida kubwa kinyume na utaratibu, ili kuzima mianya ya uchakachuaji wa mafuta hayo ya makonyo. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inasisitiza wizara kuhakikisha kuwa, inalinda rasilimali zote zinazotokana na karafuu kwa kuuza wenyewe kwenye soko la nje. Aidha, kamati inasisitiza haja ya kufanyiwa matengenezo makubwa kwa kiwanda hicho kuanzia kiwanda kipya cha makonyo kitakachotumia teknolojia ya leo pindi hali itakavyoruhusu, ili kukabiliana na tatizo la uchakavu wa mashine na kushindwa kukidhi mahitaji ya wateja wa nje kutokana na uzalishaji mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza wizara kwa kupitia Shirika la Taifa la Biashara ZSTC kwa kutekeleza ipasavyo agizo la kuandaa mipango madhubuti ya kuendelea na kilimo cha viongo, yaani *spice* kwa wakulima wetu hapa Zanzibar, kwani imebainika kuwa bidhaa hizo zina soko kubwa duniani. Pia kamati inaiomba wizara kuzidi kuwapatia mashirikiano wakulima hao kwa kuwapatia anuwani za wateja wa nje wanaohitaji bidhaa za viungo vya ndani ya nchi yetu. Hatua hii ni muhimu kwa kukuza jina la Zanzibar kwenye soko la dunia na kukuza pato la wakulima na kwa taifa kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa agizo la kukabiliana na upungufu wa wataalamu unaoikabili taasisi ya viwango Zanzibar, yaani ZBS. Kamati iliarifiwa kwamba wafanyakazi 10 tayari wameshaajiriwa ambao wote wana viwango vya Shahada ya Kwanza katika fani tofauti. Tumeipongeza wizara kwa kutekeleza juu ya agizo hili kikamilifu. Aidha, kamati inashauri kuwaendeleza wafanyakazi hawa kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo ili kupata ujuzi wa kuendesha shughuli za kimaabara.

Pia kamati inaishauri Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iwe na mikakati ya muda mrefu na ya muda mfupi katika kuijengea uwezo kitaalamu taasisi ya viwango Zanzibar *ZBS*, ili kazi ya ukaguzi wa bidhaa waweze kutekeleza wenyewe kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa tunatoa shukrani kwa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha hotuba hii, ni imani yangu kwamba michango yenu itasaidia katika kujenga zaidi utendaji wa wizara hii. Kwa jumla Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuyatekeleza maoni na maagizo ya kamati kwa kiwango kikubwa, na kamati imeridhishwa sana na majibu ya hoja hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Shihata akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, maafisa na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazo ziafanya ili kuhakikisha kwamba biashara zetu zinakua siku hadi siku.

Pili Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wafanyabiashara wote wa ngazi zote kwa kazi nzuri wanazofanya hadi leo huduma nzuri tunapata katika nchi yetu, hasa tukiangalia katika sehemu ya vyakula, mahitaji mbali mbali pamoja na mambo mengine ambayo yanatuhusu kwa maisha ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kwa bahati nzuri narudia tena tumezungukwa na bahari na nchi yoyote yenye rasilimali bahari huwa inanufaika na mambo mengi. Nyuma tunakotoka zamani nakumbuka tulikuwa tunapata samaki ambao walikuwa wanatoka katika viwanda mbali mbali, walikuwa wanaitwa samaki wa vibaki. Ulikuwa unakwenda dukani unanunua wanaletwa kutoka katika nchi mbali mbali, kama sikosei walikuwa wanatoka China na nchi nyengine za nje, lakini leo utaratibu ule haupo. Kwa hivyo, nimshauri sana Mhe. Waziri na hicho huwa ni kilio cha siku nyingi bado Zanzibar tuna haja ya kuanzisha viwanda ambavyo vinakidhi haja kwa bidhaa au mali ghafi zilizokuwepo katika nchi yetu. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kama itashirikiana vyema na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi basi tunaweza tukapata faida kubwa sana kwa kupata viwanda hivi ambavyo vitakidhi haja katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku katika nchi yetu samaki huwa wamezagaa katika maeneo mbali mbali, tunaita wakati wa shwari. Samaki huwa wengi na wale tunaotembelea sehemu za Pemba, ukenda Machomanne pale, Wete, Msuka vya kuwafanya samaki watu hawana. Kumbe kama tunangekuwa na viwanda vya kusindika samaki basi wakati ule ndio wa kuwahifadhi samaki wetu, ili wakati wa kusi mkali na kaskazi mkali basi samaki wale wangekuwa wanauzwa kwa bei nafuu bila kukosa katika *season* zote za muelekeo wa hali ya hewa katika nchi yetu.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri biashara tunaweza kufanya, lakini biashara tuifuatilie ili tuifanye, tukisema tu tutafuatilia tunafanya hivi basi tutakaa muda mkubwa sana hatufanikiwi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake aliokuwa nao kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wafanye tathmini na wafanye mbinu mbali mbali ili tupate wawekezaji wa viwanda hivyo ambavyo vitakidhi haja kwa samaki wanaopatikana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukienda Ukanda wa Kaskazini Unguja Nungwi au ukienda Kizimkazi, basi ni sehemu ambazo zina samaki wengi sana Mhe. Mwenyekiti, pia ukienda Pemba kama nilivyotaja mwanzo, ukienda Msuka, Wete, Chake Chake ni sehemu ambazo zinazalisha samaki kwa wingi. Suala hili namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi hebu tufanye angalau vijana wetu wapate ajira sehemu mbali mbali, vikipatikana viwanda hivi wavuvi watakuwa wengi lakini pili, vijana wetu watapata ajira za kufanya kazi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hushangaa sana nikiangalia samaki wanaozalishwa katika viwanda vya Tanzania Bara, Mwanza na sehemu nyengine. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha wenzetu wana samaki wa minofu wanasafirisha nje sehemu mbali mbali, sisi bado tumekaa bahari imetuzunguka. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha viwanda bado tuna matunda sehemu mbali mbali na kwa wakati wake, kuna mananasi wakati wa *season* hapa vya kuyafanya hatuna, kuna maembe wakati mwengine hatujui tufanye nini, kuna machungwa na ndimu huwa tunaangalia tu yanapotea hivi hivi, kwa sababu kama kilo leo unanunua shilingi 2,000 au 3,000. Leo mfano, siku ambazo hazitakiwi ndimu au hazitakiwi tungele unaweza ukanunua mpaka mia 500/-. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri au atafute wafadhili, yaani watu wa sehemu mbali mbali wawekezaji ili waje watuwekee viwanda hivi vidogo vidogo ambavyo vitatusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kiwanda cha Sukari Mahonda, ukurasa wa 5. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali, kwa kuona kwamba hana haja ya kiwanda hichi kupewa nguvu na kuendeleza shughuli zake hizi za kiwanda.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanda hiki katika nchi yetu ni rasilimali pekee tuliyokuwanayo na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha kiwanda hiki na sasa hivi kapewa mwekezaji. Mimi naunga mkono kwa kupewa mwekezaji ili akiendeleze, tunashukuru. Katika kamati kifungu cha 15 kinasema hivi,

Kifungu cha 15

"Kamati inaitaka wizara kupeleka maombi maalum kwa serikali juu ya haja ya kukifanyia matengenezo makubwa kiwanda hicho ili kwenda na wakati, yaani kiendane sambamba na teknolojia za usalishaji duniani, kukidhi matakwa ya soko la ndani"

Lakini kwa bahati nzuri wizara imejibu kwamba bahati nzuri wizara imejibu kwamba Kiwanda cha Sukari kimefanyiwa matengenezo makubwa na kwa sasa kina uwezo wa kukamua miwa kutoka tani 400 hadi tani 800 kwa siku, hii ni sehemu kubwa sana. Kwa hivyo, serikali kwa kupitia kiwanda hiki inafaa tuipongeze kwa dhati na tumpe uwezo mwekezaji yule kwa kuhakikisha kwamba kazi zake zinakwenda vizuri, ili kunusuru upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa nchi yetu, hasa sukari.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba wenzetu hawa wana matatizo ya kupata mashamba. Naipongeza serikali kwa kupitia vikosi vyetu vya SMZ, vikosi vimekubali KVZ na JKU kutoa mashamba yao kwa kulima miwa na kuwauzia wao Kiwanda cha Sukari.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina ushauri mwengine zaidi. Mhe. Mwenyekiti, hebu tuangalie kwa upande wa Pemba kuna maeneo mengi sana yanazalishwa miwa. Kama wawekezaji hawa watakuwa tayari kutumia nafasi hiyo ya miwa kuagiziwa Pemba na meli zetu tunazo. Meli yetu nzuri ipo kubwa, Bakharesa ana meli nzuri ambayo inaweza kutusaidia kwa hali na mali, wawashauri wakulima ili kuongeza mapato yao. Kwa hivyo, miwa ilimwe Pemba iletwe hapa kama ina kiwango ambacho kinakubalika. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri watu watapata ajira nyingi na watafanyakazi za kujinasua katika umaskini.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kilimo cha mwani nimeona. Nimpongeze Mhe Waziri kwa kuliona hili, kwamba kilimo cha mwani mimi naweza kusema ni suala kubwa sana. Ingawa kuna taarifa katika ukurasa wa 10 wamesema tu kwamba angalau wanataka kuanzisha kiwanda cha kusindika mwani. Mimi namuomba Mhe. Waziri tufanye, kwa sababu tukisema angalau labda ni kama kitu kidogo sana. Suala hili tukilianzisha mheshimiwa tutafanikiwa sana na wananchi wetu kuweza kupata faida.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu liko pale pale. Mhe. Waziri Marehemu Mzee Karume Mwenyezi Mungu amrehemu alisema neno moja kubwa sana, nakumbuka wakati huo mimi mdogo aliwaambia wanafunzi pamoja na mimi wakati huo, someni leo elimu ni ya bure, mtakuja kuitafuta kwa pesa huiwezi, na kweli wamo watu wanashindwa leo kusoma, wanataka kusoma lakini uwezo hawana. Lakini akasema, nataka kuhakikisha kwamba biashara yoyote ifanyike katika nchi yetu na biashara itembee sio uifuate mjini, hapana, uitembeze ili inunuliwe.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri bado tutowe wataalamu wetu na washauri mbali mbali pamoja na kuwa hapa kuna *Taskforce* ambayo imeundwa ya watu 16. Mimi nashauri tu namuomba Mhe. Waziri bado watembee waangalie hii bei ya mwani kweli inakidhi haja, bei ya mwani iko chini sana na inasikitisha, zao la mwani ni gumu sana Mhe. Mwenyekiti, na zao la mwani kusema kweli lina kazi kubwa sana, kina mama wanapata shida na wanaumia sana katika maisha yao kutokana na adha hiyo lakini ndio maisha tu hawana la kufanya.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri, bado awatembelee na awatafute hao wawekezaji. Hapa katika ukurasa wa 10 katika majibu ya wizara kifungu namba mbili, alituambia kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Baharini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *UNIDO*, inaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji katika kusarifu na kuongeza thamani zao la mwani. Tayari nasema amejitokeza mwekezaji mmoja ambaye sasa anatayarisha andiko la mradi wake huo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, hakuna kuficha katika dunia ya leo ya utandawazi. Huyo mnunuzi au mwekezaji huyo anatoka nchi gani, na kiwanda hicho kinaitwa jina gani. Kwa sababu leo tuelewe, siku nyengine anaweza kuja katika mazonge ambayo hatuyaelewi, lakini naamini kwamba kwa kuwa serikali imekaa na imelizingatia hilo, basi Mhe. Waziri akija hapa

atueleze tu kwamba huyu tunayemtegemea ambaye atakuja kutupa angalau, hii angalau naiweka mimi, kutuongezea bei. Huyu anaweza kutusaidia sana, lakini Mhe. Mwenyekiti, atueleze moja kwa moja kwamba anatoka nchi fulani.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba kuna karafuu zinatoka Tanzania Bara, ukurasa wa 12. Kuna karafuu zinatoka Tanzania Bara, suala hili Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kamati kwa makusudi kwamba imeona tu kuwa sasa hivi karafuu zinatoka Morogoro, Tanga kwa Tanzania Bara, sijui Mkoa mwengine upi. Lakini kwa bahati nzuri niipongeze wizara inasema mpaka kufikia leo katika soko letu la Zanzibar (Unguja na Pemba) bado hazijagundulika, lakini inasemekana kwamba karafuu hizo zinataka kuletwa kwa ujanja ziingie hapa halafu zichanganywe na karafuu zetu ili zituharibie soko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba serikali kwa kuwa imeweka mkakati huo wa kuzizuwia basi izuwie moja kwa moja ili kunusuru zao letu hili la karafuu. Zanzibar tuna mambo matatu tu muhimu au mawili, tuna utalii na karafuu, la tatu ni bahari. Mimi narudia tena bahari kwa sababu ina rasilimali kubwa ambayo tukiitumia vyema itatupa utajiri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aongeze bidii, ili ulinzi wetu udumu na uimarike kuzuwia karafuu kutoka nje ya Zanzibar zisiingie katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho. Namuunga mkono na nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote, lakini pia kamati naipongeza kwa dhati kwa kazi nzuri walioifanya chini ya mwenyekiti wake, makamu wake na wajumbe wote kwa kazi nzuri ambayo wametuletea ambayo leo tunakichangia kitabu hiki. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Ali Shihata kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuita Mhe. Hidaya Ali, minong'ono imekuwa mingi na sauti zinapaa sana juu mpaka watu wa kule chumba cha *Hansard* wanapata shida. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe minong'ono ipunguwe au sauti zisizidi juu sana. Sasa namuita Mhe. Hidaya Ali akifuatiwa na Mhe. Rashida Makame Shamsi na Mhe. Simai Mohamed Said ajitayarishe.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya ripoti hii ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia salama mpaka muda huu tukiwa katika hali ya afya na uzima, bado tunaendelea na kazi yetu hii ya kuwawakilisha wananchi katika mikoa yetu yote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa haya mambo mazuri ambayo ametuwasilishia hapa juu ya maoni ya wanakamati hii. Pia kwa kutupa moyo na matumaini mazuri juu ya taarifa hii ambayo imesomwa, niwapongeze sana na wanakamati kwa kuyaona haya yote ambayo wameyawakilisha hapa. Mhe. Mwenyekiti, niwaambie sana wahongere na

Mwenyezi Mungu azidi kuwapa moyo wazidi kuyaona ili yafanyiwe kazi na nchi yetu izidi kwenda mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja na agizo namba 8. Wanakamati wamesema kwamba wanaiomba serikali iwe na bajeti maalum ya wajasiriamali ili iweze kuwasaidia katika kuthibitisha ubora wa bidhaa zao. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana wanakamati kwa kuliona hili juu ya wajasiriamali ambao ndio nguvu kazi ya taifa letu hili.

Mhe. Mwenyekiti, wajasiriamali wapo wengi sana ndani ya nchi yetu hii na tunawaona wengi wao wanafaidika, lakini kuna baadhi pia bado hali zao ziko chini kimaendeleo na ule mfaidiko basi haujakuwepo kwa upande wao, lakini niwapongeze wanakamati kwa kuliona hili na wakaiomba sana wizara iweke bajeti, au *budget* kwa Kiswahili cha mjini, maalum kwa wajarisiamali.

Mhe. Mwenyekiti kuna haja sana ya kuwatizama wajasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja sana ya kuwatizama wajasiriamali wetu kwa hali ngumu sana wanayopambana nayo ya kimaisha. Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia suala hili kwa kuwatizama kinamama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kinamama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wengi wao wanajihusisha hasa na vikundi vya *SACCOS*, lakini katika vikundi hivyo sana huwa wanajihusisha na masuala ya ukulima wa tungule. Hapa sana nawazungumzia kinamama wa Matemwe, Kijini, Nungwi na maeneo yale ya ukanda wa pwani ambako ardhi yake iko tofauti na huku kwetu kwengine kunako rutuba nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, zao la tungule katika Mkoa wa Kaskazini Unguja limepamba moto hasa katika maeneo ya Matemwe na Mkwajuni. Mhe. Mwenyekiti, wewe zunguka mji mzima usipate tungule lakini nenda Mkwajuni sokoni utakuta tungule na bei ya tungule ya Mkwajuni Sokoni huwezi ukaikuta sehemu nyengine yoyote, kwa sababu pale unaweza kukuta kisado kizima cha tungule au ndoo nzima ukaambiwa mama hiyo lete elfu mbili tu kutokana na kwamba hizi tungule pale zinalimwa sana na zinavunwa sana, kwa kweli wanajitahidi sana wajasiriamali wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwenye zao la tungule lakini faida na tija bado hawajaipata kutokana na kwamba hili zao linaonekana kama halijakuwa na umuhimu, lakini si kweli zao hili la tungule kwa kweli linahitajika sana na linalimwa sana tunapokea tungule hapa kutoka Mikoa ya bara lakini tunaacha kuithamini tungule ambayo inalimwa ndani ya visiwa vyetu hivi hivi vya Zanzibar. Na ni tungule ambayo pengine wewe unaweza kuitumia katika mchuzi wako usitafute kitu chengine limau wala bilingani, kwa kweli kuna haja kubwa sana Mhe. Waziri kuhusiana na suala hili.

Pia hapo hapo nikija kwenye agizo Na. 19 Kamati pia imesema inaitaka Wizara kuendeleza kutoa taaluma kwa wajasiriamali ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na ziweze kuingia katika soko la ndani na nje.

Mhe. Mwenyekiti, tungule zina uwezo wa kuingia ndani ya soko la nje na ndani kwa sababu kunatengenezwa Tomato *kechup*, tomato saladi kunatengenezwa kila aina ya tomato michuzi, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri wamesema hapa viwanda na Masoko kwamba kuna mashirikiano makubwa ya karibu na Mamlaka ya Uwekezaji yaani *ZIPA* basi ilione suala hili la kuwaekea angalau kijisoko kidogo cha kuweza kuona ile tija ya zile

tungule ambazo wanazilima wana wa Mkoa wa Kaskazini hususan kinamama na wanawake wanahangaika sana, nikisema kina mama na wanawake kwa sababu kinamama ni wale ambao wameshakuwa watu wazima lakini kuna vijana bado nao ni wanawake nao wanaifanya kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mkulima mmoja na mvuvi mmoja kutoka Nungwi alikwenda zake Baharini aliporudi akasema ama kweli ugali wa mhogo unono kwa Tasi na tungule za uchogo, kweli tungule za uchogo tamu. Kwa hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri tukaliangalia zao la tungule na tukaweza kuliangalia sana kwa kuwaona wajasiriamali hawa ili na wao wakaweza kunufaika na zao lao hili, wasiwekewe kiwanda maana pengine kina *process* nyingi lakini waonekane kwa hili suala la mikopo ili kuweza kujiendeleza zaidi na biashara zao hizi au na soko lao hili likaweza kuonekana Duniani kote.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende tena kwenye agizo No. 43 Mhe. Mwenyekiti, hapa nitazungumzia suala la *Spice* na viungo, suala la viungo nalo ndani ya Zanzibar yetu limekuwa ni suala ambalo linaturejesha nyuma kiufupi wakulima wa *spice*, kwa sababu tumeona katika mashamba mengi yaliyoko ukanda wa Magharibi, ikiwemo Kizimbani, Bumbwisudi, Miwani na kwengineko tunaona jitihada ya wananchi lakini pia ya wajasiriamali wale wale ambao wanajihusisha na vilimo hivi, tuwapongeze sana kwa kutokata tamaa kwanza. Kwa sababu hawakati tamaa bado wanaendelea na vilimo hivi siku hadi siku lakini faida bado kwao imekuwa ni duni kutokana na kwamba zao hili wanaofaidika nalo ni wachache ambao wanatoka nje ya nchi yetu.

Lakini wale wakulima ambao wanavuja jasho na kumiminikwa na machozi kwa kulithamini na kulienzi zao hili ikawa bado halijapotea ndani ya nchi yetu faida yao haijaonekanza, mkulima anakusanya pili pili zake si chini ya vipolo vitatu au vinne lakini pili pili bado utamkuta mkulima yule siku zote yeye yuko katika hali duni ya umasikini kwa sababu hafaidiki nayo, anakuja pale mteja kununua pilipili ile kwa kilo pengine kapata siku hiyo elfu kumi. Lakini yeye anakwenda kuuza kilo si chini ya elfu thalathini lakini pia pale pale tujiulize inafika siku Zanzibar hii hii unaitafuta pili pili manga wewe itakushinda kwa sababu bado hatujakuwa na vidhibiti maalum au lile soko ambalo litatuhifadhia hivi vitu baadae iwe tunaweza kuvitumia hata kama ile misimu ambayo havipo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti tulione sana suala hili Mhe. Waziri kuna haja ya kuweza kuweka viwanda hivi wawekezaji watafutwe na hayo maelewano ya karibu yawe ya karibu zaidi ili waweze kutuwekezea katika nchi yetu, viwanda viwepo hatujatosheka tu na kiwanda cha muwa Mkoa wa Kaskazini lakini na viwanda vyengine ila na masoko basi yawepo karibu na wale wananchi, kwa sababu tunaona bidhaa nyingi zinapotea zinapokwenda nje ya ule mji ambao unalimwa yale mazao yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, machungwa, mapera na mengineyo yote mazao haya yote ni makulima ya wajasiriamali ambao wanapambana kuhakikisha wanajikimu kimaisha, wajasiriamali hawa wanahangaika sana. Basi kwa vile kamati wameliona hili hii mikopo ifikishwe kwao ili waweze kufaidika na mazao haya lakini waweze kuona faida ya mazao haya wanayohangaika kuyalima, pia waone kwani ndani ya nchi yetu kuna kitu ambacho kinatujali kama sisi wajasiriamali, lakini pia inatuona kwa hali zetu duni na za kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi ya kuzungumza juu ya kamati hii niwapongeze sana wana kamati kwa mawasilisho yao haya mazuri ambayo Mhe. Waziri yuko makini na nina hakika atayafanyia kazi, ili yaweze kuleta manufaa, yaweze kuleta tija kwa wananchi wetu wote tukiwemo na sie humu tuliokuwemo ndani, maana wakinufaika wao na sisi pia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache niseme naiunga mkono hotuba hii ya Kamati ya utekelezaji asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuichangia ripoti hii ya Utekelezaji wa maagizo ya kamati inayohusiana na Wizara hii ya biashara, awali nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya mpaka kuweza kukusanya maelezo ambayo yametosheleza juu ya hoja za kamati kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yao.

Lakini pili nichukue fursa hii vile vile kuipongeza kamati ya Fedha Biashara na Kilimo kwa kuweza kufuatilia mpaka kuwa na maagizo ambayo wameiagiza Wizara inayohusika, vile vile niwashukuru wenzangu ambao wametangulia katika kuichangia ripoti hii Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Muwakilishi makini wa Jimbo la Kijitoupele, lakini vile vile Mhe. Hidaya Ali Makame muwakilishi wa vijana katika Mkoa wa Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika michango yangu katika ripoti hii nije katika agizo No. 7 katika ukurasa wa 3 ambalo limeanzia ukurasa wa pili kumalizia wa tatu ambalo linahusu Shirika letu hili la viwango *ZBS*. Mhe. Mwenyekiti hoja inasema Serikali iwe na mpango wa kuanzisha maabara ya *ZBS* Pemba na wenzetu wamejibu hapa kwamba tayari wamekwishafungua Afisi yake Pemba kwanza niwapongeze sana kwa kuweza kuitikia agizo hilo la kuweza kufungua ofisi hii ya Shirika la Viwango Zanzibar katika upande wetu wa pili wa visiwa vyetu. Ni jambo zuri kwa sababu Pemba nayo ni sehemu ya eneo ambalo bidhaa zinaingia kutoka sehemu mbali mbali, kwa hivyo kuwa na Shirika hili la viwango ni jambo zuri sana tuwapongeze sana wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili wenzetu wametwambia kwamba tayari wako katika kufikiria maabara gani waanzishe, hoja yangu tu ilikuwa katika mipango yao labda Mhe. Waziri akija atuambie kwamba wanafikiria kuanza na maabara gani katika kitengo hichi ambacho kitakuwepo Pemba.

Lakini walizungumzia suala la wataalam ambapo juhudi za kuwajengea uwezo zinaendelea nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja atwambie ni wataalam wangapi na wataalam wa fani gani ambao wamefikiria wanaowaendeleza ili kuweza kufanya kazi katika ofisi hizo za *ZBS* kule Pemba, na zaidi wanawalenga katika fani gani. Katika hili nishauri tu kwamba pamoja na kuanzisha Ofisi hizi Pemba lakini juhudi ziendelee katika kuona ofisi zetu zinakuwa na maabara ambazo zinakidhi haja ya bidhaa ambazo zinaingia Zanzibar, ili kuepuka usumbufu wa kuweza kuzifanyia uhakiki bidhaa hizi katika Shirika la Viwango Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika agizo No. 22 ukurasa wa 8 ambalo linahusiana na maonyesho mbali mbali ya wajasiriamali, hoja inasema Wizara iandae maonyesho mbali mbali ili wajasiriamali wapate kuonyesha bidhaa zao na kuzitangaza ili waongeze masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Mhe. Mwenyekiti, majibu ambayo yametolewa na Mhe. Waziri ni

majibu mazuri napaswa kumpongeza lakini linalojionyesha kwa wajasiriamali wetu mara nyingi wananeemeka na maonyesho zaidi yale ambayo yako nje ya visiwa vyetu, hata katika jawabu ambayo imetolewa hapa kwamba aidha Wizara inaratibu maonyesho ya kimataifa ya saba saba ya kila mwaka yanayofanyika Tanzania Bara, lakini vile vile inaratibu maonyesho ya kitaifa kwa kila mwaka na linafanyiwa kazi ili kuweza kusaidia soko la wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inakua kibiashara na wajasiariamali wetu tunawahimiza tunawashajihisha kila siku na kwa kweli wanaitikia wito, lakini suala ambalo mimi bado najiuliza kwamba nchi yetu bado mpaka leo hatujafikiria kuwa na eneo ambalo tunaweza kufanya maonyesho ya kudumu ya kila mwaka. Hili nafikiri Mhe. Waziri ulichukue ili kwa pamoja tuweze kulifanyia kazi kwa sababu nchi hii mimi nakumbuka mwaka 1981 Rais aliyekuwepo kwa wakati ule alikuwa na lengo hilo na akanzisha pale Mwanakwerekwe mabanda ya maonyesho ya biashara, lakini vile vile maonyesho yale ya biashara kutokana na uhitaji wa mambo ya kielimu basi yakafa, lakini katikati tena Rais aliyekuwepo akaanzisha majengo ya kudumu ya maonyesho ya biashara Tunguu nayo hivi sasa imekuwa ni Chuo Kikuu *SUZA* sasa inaonekana kila mtawala anayekuja haoni umuhimu wa kuwa na sehemu ya maonyesho ya biashara.

Lakini nafikiri umefikia wakati kuona kwamba Zanzibar ina eneo la kudumu la kuweza kufanya maonyesho ya biashara hii inaweza ikasaidia kukuza biashara za wajasiriamali wetu hata biashara za wale ambao watafungua viwanda tunataka kuelekea katika uchumi wa viwanda, lakini kama hatuna maeneo hasa maalum ya kudumu ya biashara nafikiri itakuwa ni ndoto. Kwa hivyo hili tulichukue Mhe. Waziri ili tuone kwamba linafanyiwa kazi na hatimae Zanzibar nayo iwe na sehemu hiyo na wafanya biashara kutoka sehemu mbali mbali nao waje hapa kuweza kuonyesha biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti nije sasa katika agizo No. 39 ukurasa wa 13 juu y suala zima la miche ya karafuu, kuna tatizo hili la miche ya karafuu kwa wakulima kwamba inakuwa haina ubora mimi nafikiri miche ya karafuu ambayo wakulima wanaipata kuna vyanzo viwili, kuna vile vitalu ambavyo vinaandalia na Serikali au katika maeneo ya Wizara ya Kilimo lakini siku hizi kuna vitalu ambavyo vinaandaliwa na wakulima au watu binafsi, mimi nafikiri umeshafika wakati kwamba hii miche ya mikarafuu ambayo zaidi inatolewa na wakulima binafsi kuna haja kwamba iweze kuangaliwa ubora wake, kwa sababu inawezekana wanazalisha hiyo miche lakini wakati mwengine inakosa ubora na ndio maana pengine wakulima haiwasaidii sana na mingi yao pengine ndio inakufa. Kwa hivyo kabla ya kuiuzia Wizara yetu ya Biashara miche hii lazima tuone kwamba inafikia katika viwango na hii naomba sana Wizara ya Biashara ishirikiane na Wizara ya Kilimo ili kuona miche inayotoka katika vitalu vya watu binafsi inakuwa na ubora na kuwasaidia wakulima.

Lakini vile vile wale wanaopewa miche yenyewe hili nasisitiza mara kwa mara kuweza kufanya *follow up* ya kuweza kuona kwamba wanaishughulikia ili kuweza kuondoa haya malalamiko, kwa sababu wengine pengine hawaishughulikii vizuri halafu malalamiko yanakuwa makubwa kwa hivyo pande zote mbili ziweze kuangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika ukurasa wa 15 katika agizo No. 43 Mhe. Mwenyekiti, agizo hili linahusiana na uendelezaji wa kilimo cha viungo yaani *spice* kwani imebainika kuwa soko la

bidhaa hizo ni kubwa duniani na hadi sasa hatujaitumia fursa hii kikamilifu. Mhe. Mwenyekiti mimi nishauri katika hili ukweli ni kwamba Zanzibar inazungumzwa na sisi tunajisifu wenyewe *Zanzibar is Space Island* tunajisifu kila mara, lakini ukweli ni kwamba viungo au mazao ya viungo tunayozalisha ni kidogo sana na yanalimwa katika hali ambayo utaalamu haujatumika vizuri, wakulima wetu ni wadogo wadogo wanalima visehemu vidogo vidogo hata wakati mwengine eka mbili hazitimii. Lakini Zanzibar inaonyesha kama ukulima huu utakwenda kitaalam tuna uwezo wa kuzalisha pilipili manga nyingi, pilipili hoho nyingi, vanila nyingi, hiliki nyingi, na zao la mchai chai kwa wingi mchai chai unakubali kila pahala.

Sasa nafikiri wakati umefika Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuweza sasa kuwa na mashamba ya mfano ya kuweza kuona kwamba huu ukulima unawezekana, sasa kwa sababu masoko yapo na mazao haya yanakubali mimi nafikiri hakuna sababu hivi sasa kubaki katika hali hiyo ya umasikini kwa wakulima wetu wakati mazao haya yanakubali katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru baada ya kusema haya niseme tu naunga mkono ripoti hii nzuri na tumtakie kila la kheri Mhe. Waziri, kuweza kuyasimamia haya ili tuone kwamba suala zima la biashara linakuwa katika visiwa vyetu ahsante sana.
Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said, atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wangu wa jimbo la Tunguu kwa kuniwezesha mimi kufika hapa leo kuwa msemaji wao na niweze kutoa mawazo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Balozi Amina Salum Ali (Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) kwa jinsi alivyosoma hotuba yake pamoja na kiongozi wetu Mhe. Mnadhim ambaye pia ndiye aliyesoma ripoti hii kwa niaba ya Kamati. Pia niwapongeze sana wote walionitangulia waliotoa maoni yao na mawazo yao kuweza kumshauri Waziri husika mwenye dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda moja kwa moja kwa sababu sina mengi nina madogo tu, lakini maamini haya nitakayoyatoa yataweza kumsaidia Mhe. Waziri na Kamati husika ili tuweze kuishauri serikali kutimiza majukumu yake. Nimejaribu kuangalia ripoti na kumsikiliza Waziri lakini maeneo mengi yamegusa masuala ya karafuu, *ZBS* na maeneo mengine. Kwa hivyo mimi nitajaribu kuchangia maagizo kwa ujumla ili yale mawazo yangu niyapate kuyaweka kwa pamoja na yaweze kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuja na Sheria hii mpya tuliyoipitisha juzi hapa ya Baraza la Biashara ambalo naamini itakuwa moja katika sehemu kubwa sana ya kuweza kutatua changamoto, lakini pia kuleta ukaribu baina ya sekta binafsi na sekta ya umma na kuweka majadiliano ambayo yataweza kuleta tija na kusaidia nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia maeneo ambayo yamegusa kiwanda cha Mahonda na jinsi changamoto zilizokuwepo zamani kama za wakulima. Pia nimejaribu kuangalia kitabu cha *House hold budget survey* kwenye *main report* 2014/15 kwenye ukurasa wa 15 unasema hivi:

"Most employ people are subsist farmers, fishers or hunters ni asilimia 41.8,

The second large occupation katika kazi ambayo *ni 16.5* ina *consist of street venders, cleaners, manufacturing and labours.*

Lakini *The third category is services, serve workers* ni *15% and the majority of whom probable involve in the tourism sector hotels, step bum and waiters* wamo katika hiyo *15%*

Na mwisho wanasema *directors chief executives* wapo kwenye 0.7%."

Mhe. Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu kima cha chini kilichotangazwa na Mhe. Waziri ipo athari au changamoto iliyojitokeza katika kiwanda cha Mahonda hasa kwa wakulima na katika jinsi ya kutekeleza agizo la kuwalipa wakulima Sh 25,000/= kutoka Sh. 7.000/= na Sh.10,000 kwenda mpaka Sh.30,000/= .

Mhe. Naibu Spika, kiwanda hiki kinahitaji wakulima wengi hasa hawa katika kusimamia kazi zao za kila siku. Malengo ambayo wenyewe waliyokuwa wamejipangia na ukiangalia ripoti hii ya ukurasa wa 15 mkiunganisha yote, mimi nashauri kwamba Wizara ya Biashara na Waziri husika aangalie utaratibu wa kuangalia katika Sekta ya Biashara hasa katika maeneo ya viwanda kuangalia utaratibu mpya ya kupanga mishahara pamoja na viwango vya kima cha chini ili hawa watu waliokuwa kwenye viwanda waweze kufanya kazi zao na kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana ni kiwanda kimoja ambacho tunakiona sasa hivi lakini naamini ni viwanda vingi sasa hivi watu wanapoteza ajira zao, lakini pia uhakika wa kibarua au wa kazi unakuwa haupo. Nashauri masuala ya kupanga mishahara katika viwanda kama hivi, aangalie utaratibu pamoja na wizara husika ili yale malengo yote anayoyakusudiwa yaweze kutimizwa.

Mhe. Mwenyekiti, masuala la *EPZ* nahisi pia yangepewa kipaumbele kwa kushirikiana pamoja na *ZIPA*. Ukiangalia kwenye agizo Nam. 9 japokuwa wamekiri kwamba wanashirikiana katika mikutano ili kuleta ukaribu wa majukumu yao. Ukiangalia kwa yale yote ambayo Wizara hii ameweza kuyakusudia kuna umuhimu mkubwa sana kuwa na Maofisa ambao ndani ya Wizara pamoja na taaisi yetu ya *ZIPA* ili yale mambo ya kufanya kazi kwa *speed* ili kuweza kutatua changamoto na kuondoa hii *rate* au *bureaucracy* inapokuwa kati kati anapokuja muwekezaji hatima yake anasema bwana mimi naondoka nimeshindwa kwa sababu muda niliokaa, muda niliopoteza hakuna kinachoenda.

Sasa lazima mambo haya zinapotokea hizi *opportunities* twende kwa *speed* ili tusikae tukasema kwamba kuwekeza Zanzibar ni lazima, lakini tutambue kwamba kuna maeneo mengine, kama ninavyokumbuka juzi nilisema hapa nchi kama Rwanda wanakwenda kwa haraka sana katika usajili wa Makampuni. Leo Waziri wa Fedha alikiri katika kutatua matatizo haya alipokuwa anazindua suala la *One Stop Center* kwa Zanzibar *ZIPA* wanachukua mpaka siku 21. Inawezekana hata ni zaidi. Sasa haya yote tusiache pia kuyafanyia kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sehemu moja nimejaribu kuangalia japokuwa zimetajwa *spice* nyingi. Nimejaribu kuangalia suala la pilipili. Mimi tangu mdogo nasikia Kwa Adinani utakuta kuna

urojo na pilipili, ukienda Forodhani utakuta kuna chakula na pilipili, ukienda katika Mahoteli yote utasika kuna chakula na pilipili.

Nimpongeze sana Mhe. Waziri hivi karibuni tumeanza kuona pilipili ambayo ukenda kununua kwenye maduka ya *Super Market* baadhi ya chupa za pilipili zimeandikwa *made in Zanzibar*. Lakini kitu kimoja kinachonipa hofu ile aina ya chupa inayotumika inaendana na chupa za maji ambazo zinatumika pia, samahani mtanisamehe kwa ninachokisema, lazima ziwe tofauti. Kwa sababu chupa hizi hizi ndogo ndogo zinazotumika kutia pilipili zinatumika pia watu kufanyia *urine test* wanapopeleka mahospitali. Wakati mwengine mtu anapotaka kununua anapata hofu je, hii chupa ni ile ile au ni tofauti. Tuangalie katika *packaging* vitu tunavyotumia viwe ni tofauti na vile ambavyo tunavyotaka kuvilepeka katika masoko yetu. Hasa kama tukiamua kupeleka katika masoko ya nchi kama za Oman pamoja na Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, pili pili ya kutoka Zanzibar watu Arabuni wanapenda sana kuliko hata madoriani, ukiwaambia pilipili kutoka Zanzibar na kama tutapata *supplier* mmoja mzuri wa kupeleka naamini pilipili ya Zanzibar itakuwa ni nzuri sana. Hakuna mwana mama yeyote akayepika chakula Zanzibar akiweka ukwaju wake, akiweka mambo pale baada ya wali, na akaweka mchuzi wake chukuchuku na pilipili, basi naamini ukiwa mgeni kwenye nyumba utauliza bwana, hebu na huu mchuzi upo na mimi nitilie kidogo, kutokana na ile harufu. Pilipili na mapishi yetu naamini na sisi tukiweza kuyaunganisha haya tutakwenda mbali sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la biashara ya mwani. Jana wakati Waziri anazungumzia masuala ya biashara ya mwani alisema kama kilo imekwenda kwa Sh.400/- mwaka jana wakati nachangia kwenye Mkutano wa Bajeti nilisema kwamba Philippines pamoja nchi nyengine za huku far Asia wameanza kulima mwani kwa kasi sana. Nikatoa hofu kwamba inawezekana bei itazidi kushuka kwa upande wa visiwa vyetu kutokana na wao jinsi wanavyolima mwani na jinsi wanavyousimamia tangu baada ya kutoka baharini mpaka unakwenda kuwa *packaged* na moja kwa moja kwenda kuuzwa.

Mimi niseme kwamba hofu bado ninayo kwamba ikiwa leo kilo Sh.400 sasa ikiwa ni sahihi na huko mbele tunakokwenda endapo soko hili litaporoka, mimi labda Mhe. Waziri anambia amejipanga kuwasaidia hao wakulima kuja na mawazo gani mbadala ili tuhakikishe hasa kwa upande wa Pemba na Unguja watu hawaathiriki. Natambua kwamba ukiwa na biashara ya mwani Pemba wana *produce* karibia tani 12,000 na Unguja karibia tani 3000. Ukiangalia watu wengi sana wamejiajiri katika hii biashara ya mwani. Endapo kwamba kila soko litazidi kushuka hasa katika bei inawezekana wananchi wetu wakaathirika vibaya sana. Akina mama ndiyo watakuwa wa mwanzo katika kuathirika hasa katika biashara hii. Mimi kwa upande wa jimbo langu kwenye kisiwa cha Uzi, Unguja Ukuu, Kikungwi na Bungi wanasimamia sana masuala ya biashara ya mwani. Nimuombe Mhe. Waziri pamoja na timu yake wote wawe wabunifu waanze kujipanga ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nilipoangalia katika *summary* hii ya *House hold budget survey 2016* na ya 2014/15 inasema hivi: "Watu Zanzibar karibia 54% wameowa na 22.8% nyumba zinaendeshwa na wanawake na *literacy rate* iko 83.7 na 55% ni watu wenye umri wa miaka 15 wamekwenda katika skuli za sekondari na nyumba mbili katika kila nyumba tano kwa 55.4% ukiangalia wanaendesha biashara, asilimia 44.6% wapo kijijini. Kubwa zaidi ambalo limenishtua ambalo

kama wenzangu Waheshimiwa Wajumbe kama mnalitambua kwamba katika *House hold budget survey* imetambua kiasi cha bilioni 6.3 ni fedha ambazo zimeingia kutoka Tanzania Bara au Zanzibar *in cash or some kind*. Lakini pia kwa wale wana *Diaspora* Wazanzibari wenzetu wanaoishi nje ni bilioni 6.2.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kinachosema ni kwamba fedha ambazo tunasaidiwa au ndugu ambao wanawatumia ndugu zao kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar ni nyingi kuliko zile ambazo zinatoka kutoka nchi za nje. Hapa tuangalie jinsi ambavyo biashara hii inavyofanywa katika nchi yetu pamoja na wananchi wetu wanavyofaidika. Hawa Wazanzibari wakati mwengine wanaoishi kutoka nchi za nje inawezekana wapo katika nchi za Kiarabu, wengine wapo Ulaya pamoja na Marekani. Wana bidhaa ambazo wanataka kuzileta Zanzibar lakini wanapata changamoto sehemu mbili.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya kwanza uhalali au jinsi ya fedha zitakuwa na usalama kwa sababu inawezekana kuna migogoro ya kifamilia. Mimi nataka nikushauri Mhe. Waziri kwamba katika lile Baraza la Biashara na wale viongozi wote wa *Diaspora* waliokuwepo katika nchi za Ulaya tuwatafutie utaratibu wa kuanzisha katika maeneo huru kuwawekea maeneo ambayo wao wenyewe wanaweza kuleta bidhaa zao waweze kuja kuuza Zanzibar. Huu wakati wa kuleta mafriji, *microwaves*, pasi, ambayo yapo chini ya viwango yanaweza kuleta mende, tuangaliae vitu ambavyo tunaweza tukafanya vikatusaidia katika biashara,

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilimsikia Mkurugenzi wa Tanzania *Private Sector Foundation* ambaye ataondoka tarehe 9 kwenda China akasema kwamba kuna mashine za kutengenezea misumari China zinauzwa dola 3000. Sasa hebu tuseme ikiwa kuna mashine nyingi kama hizi za kuwasaidia wananchi wetu kuwaletea hapa inawezekana sasa tukafanya biashara nyingi watu wa *Diaspora* kwa sababu ya wananchi wetu, Wazungu wanasema *teach a man how to fish*, au siyo. Mimi nashauri tuangalie ubunifu sana wa kuwatumia Diaspora kuanzisha viwanda vidogo vidogo au mashine ambazo zitaweza kuwasaidia Wazanzibari ili tuweze kuweza kuunganisha biashara yetu na tukaangalia mfumo mzima wa *value chain analyses* wa nchi yetu kwa umoja kwenda Tanzania Bara na Zanzibar katika biashara nzima ya sekta ya biashara na yale maeneo ambayo tumeyataja katika *Vision 2020* pamoja na MKUZA ambao ni *tourism trade and services*.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona mkono wako uko karibu, nimalizie kwa kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikilia. Ahsante sana naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe**.** Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa kuichangia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mimi nitachangia mambo mchache ambayo yanayoihusu Wizara hii katika taarifa yao waliyoileta hapa. Nitaanza na *page* Nam. 4.

Wizara ya Biashara, Biashara Viwanda na Masoko ilitakiwa kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala la kufanya utafiti wa kina juu ya karafuu zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara kwa soko la karafuu Zanzibar. Kamati iliarifiwa kwamba utafiti wa karafuu za Morogoro na Tanga tayari umeshafanyika na Ofisi ya Mkemia Mkuu Serikali ambapo taarifa hiyo imewasilishwa serikalini na uingizwaji wa karafuu hizo hapa Zanzibar ulipigwa marufuku.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar karafuu zetu zinatambulikana kwamba ni karafuu *grade* yake nzuri, tuna karafuu zipo maarufu na zenye harufu nzuri. Sasa kwa suala hili ambalo linafanyika wakati karafuu ni katika mazao ya Zanzibar naweza kusema namba moja yanayoingiza kipato kikubwa katika upande wa masoko ya kilimo.

Karafuu ndiyo tunayoringia Zanzibar kwa upande wa kilimo, sasa vipi wataweza ku-*control* ningependa kujua, karafuu ya Zanzibar wanaigundua vipi katika vipimo vyao na zile karafuu zinazotoka Tanzania Bara. Je, kwa wale ambao wanaliosababisha kuja kuchanganya karafuu zao za Tanga na sehemu nyenginezo kuja kuzileta Zanzibar kupitia mgongo wetu kwa kuwa zetu sisi *grade* yake nzuri na kutafuta *market* ambayo itaingiliana na Zanzibar, wamewachukulia hatua gani na ni kampuni gani iliyofanya vitu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kusema la ukweli Wizara ya Biashara kwa kuitamka utahisi ni ndogo lakini Wizara ya Biashara ndiyo Wizara kubwa naweza kusema kuliko Wizara zote hapa Unguja. Biashara ni vitu vyote, Wizara ya Utalii biashara, ukisema Wizara ya Kilimo inaangukia kwenye biashara, ukizungumza Wizara ya Fedha inaangukia kwenye biashara. Bila ya biashara mapato hayapatikani, *investment* ya utalii inaingia kwenye biashara hii Wizara ni nzito na nikubwa. Mimi kwenye suala la karafuu nimemaliza nitaomba niende kwenye *topic* yangu ya pili *page* hiyo hiyo Nam. 4.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo lilitakiwa kutolewa ufafanuzi na Kamati ni suala la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na kuliondosha suala la usajili wa viwanda katika serikali hiyo na kuikabidhi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati ilielezwa kwamba suala la usajili wa viwanda ni la Kikatiba, hivyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Tanzania Bara ili kuangalia njia bora ya kuwekeza kuweza kulitekeleza suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kufichana Zanzibar kama Katiba iliyopendekezwa kwa mara hii ya pili ukiacha Katiba ya mwanzo ya Jamhuri ya Muungano ambayo ina mambo 22 ya Muungano na sasa hivi yamebakia mambo 15 ambayo 7 yameondoshwa muhimu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, tunachongojea ni kura ya maoni ili iweze kupita rasmi, bila ya kuja kuanza Katiba hii mpya ambayo imeondoshwa vitu 7 ndani yake, Zanzibar Shirika la Biashara au Wizara ya Biashara itahangaika kufanya kila kinachofanya biashara zitakuwa ngumu maisha. Hili liko wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, biashara ya Zanzibar itakuwa ni ngumu zaidi kwa sababu kwanza nchi ndogo, mapato yake madogo, haina *income*, vile vitu ambavyo vina *income* kodi yake kubwa sana. Zanzibar inajitegemea kiupande fulani wakati Tanzania Bara kodi zake ni nchi kubwa yenye vitega uchumi vingi, vyenye mambo mengi, lakini kodi zake ndogo ulikilinganisha na Zanzibar.

Hii peke yake inaonyesha kwamba Zanzibar kwa upande wa uchumi ni mbovu kabisa, utakuwa ni mgumu bila ya hili suala kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona kuna mambo wakati wa Mheshimiwa Mstaafu Dkt. Salmin Amour, Zanzibar kwenye suala la biashara lilikuwa liko vizuri sana kuliko awamu zote mbili hizi tulizokuwa tunazo sasa hivi kiuchumi, tukizungumza kiukweli kihaki Lillahi, wakati wa Dkt. Salmin Amour biashara Zanzibar ilikuwa ipo vizuri lakini kuanzia wakati wa Dkt. Amani Karume kuja mpaka sasa hivi serikali tuliyokuwa tunayo, biashara huwezi kulinganisha na wakati wa Dkt. Salmin ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Joseph Magufuli, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Tanzania, Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, suala hili wajaribu kwenda kuongea haraka iwezekanavyo ili kura ya maoni ipigwe haya mambo yaliyoondoshwa saba yaweze kusukuma Zanzibar kwenye masuala ya uchumi. Hii peke yake ndiyo itakayokuwa njia mahsusi kabisa ya Zanzibar kuweza kuja juu zaidi kuweza kuja juu zaidi kwenye suala la biashara la siyo hivyo Mhe. Waziri namuonea huruma sana kwa hivi tunavyokwenda tutazidi kubinya watu kwenye masuala ya kodi serikali ipate *income* lakini ile biashara yenyewe mzunguko ni mdogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, tungeomba sana Mhe. Magufuli anazungumza kila siku kwamba yeye ni Rais wa wanyonge na Zanzibar wanyonge wanaumia kwenye masuala haya ya kodi. Kodi Zanzibar ni kubwa, biashara ngumu, vitu vya Zanzibar kwenda Tanzania Bara vina ugumu. Mimi ningependa kuzungumza tu kama kwa nini vitu ambavyo vinazalishwa Zanzibar kwenda Tanzania Bara inakuwa vigumu wakati vya Tanzania Bara kuja Zanzibar inakuwa wepesi mimi ningependa hapa nije nipewe jibu nipate nifahamu kwasababu inaonekana kwenye *TBS* ya Tanzania na *ZBS* kwamba *ZBC* ya Zanzibar haiaminiki vizuri kwa viwango vyake labla hakuna elimu au vifaa walivyokuwa navyo sio vizuri.

Lakini hili ni jambo ambalo moja linaangusha Zanzibar kiuchumi tuangalie Zanzibar imekuwa *connected* na nchi gani, nchi ya mwanzo ambayo iko *connected* Zanzibar ni Tanzania bara itakayotegemea kuuza vitu vyake ipate *market* na baadaye kutoka nje, sasa ikiwa kuanzia hapo Tanzania Bara ni mambo magumu kodi unapigwa hapa unapigwa huko tena ni mambo ambayo sio mazuri.

Lakini ningependa vile vile lipelekwe ombi langu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba mbali ya haya yaliokuwepo lakini pia ifikiriwe *TRA* Zanzibar ifikirie iombwe kibinadamu kabisa na naamini watu wa Jamhuri ya Muungano wabunge, Mhe. Rais na Viongozi wote ni watu wazalendo wanawatakia mema Wanzanzibari tunaomba sana *TRA* ikiwezekana iondoke Zanzibar ile *percent* tunayopata iwe kwenye *ZRB* kwasababu hatuwezi kwenda na makodi mawili mawili na mbali nyenginezo ukiangalia Wizara ya Vikosi ya Mhe. Haji Omar Kheri wizara yake ina makodi Manispaa sijui nini.

Wizara ya Fedha *ZRB*, ukienda Wizara ya Biashara wanakodi, *TRA* wana kodi Zanzibar ukiangalia tunalipa *more than fifty percent* ukijumlisha hivi vitu vyote vidogo vidogo kwa kweli

ipo haja ya viongozi wetu wa juu ndani ya nchi yetu na taifa letu kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa na kodi ndogo ili mambo yawezekwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kwengine kuzungumzia kwenye *page* namba 7 Serikali aha! siyo *sorry* nitaenda *page* namba 8 wizara iandae maonyesho mbali mbali ili wajasiria mali wapate kuonyesha bidhaa zao na kuzingatia ili waongeze masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, wizara husika ya Biashara inachotakiwa *base* za hapa Zanzibar kufanya maonyesho na Tanzania bara, sasa hivi imefika wakati wakutafuta wajasiria mali wakubwa wa Unguja kuwakusanya na wale wadogo wakachukuwa wao vifaa wakapeleka wakafanya maonyesho ikiwa Dubai katika *Middle East* kwa sababu Dubai ndio *Centre* na Dubai ndiyo nchi katika dunia nzima ya *Middle East* iko katikati ndiyo inayotegemewa kwa masuala ya uchumi wakafanye maonyesho yao vitu vya Zanzibar Dubai wakodi eneo kama *hall* watangaze hivi vitu sio lazima kuchukuwa watu wote ili *market* izidi kukubalika.

Na vile vile waangalie vipi wataweza kukubaliwa *market* yao nchini dunia na sio ku-*focus* kwenye Tanzania Bara na sehemu nyengine kama ilivyo karafuu, iko haja sasa hivi hawa wajasiria mali wote kuwatoa sasa katika hili janga la Afrika kuwapeleka huko *Middle Continent* ya *Middle East* na *American* na sehemu nyenginezo na *Asia* na *Europe*. Tukifanya hivyo Zanzibar wajasiriamali watakuja juu kidogo kidogo na kufikia sehemu nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye *page* namba 10 kwenye Wizara iendelee kutowa ushirikiano mkubwa kwa wakulima wa mwani wa bei ya zao hili bado iko chini kulinganisha na soko la mwani duniani, hii ni kweli mwani dunia una pesa nyingi sana na mimi ningependa kushauri kwamba mwani ni chakula kinafanywa *salad* kinapikwa kwenye chakula kwa nchi za wenzetu, nchi za Uturuki wapi mimi binafsi nishaenda nishakula *restaurant very expensive* unakuta mwani. Na mwani wa Zanzibar ni *quality* nzuri sasa kabla ya kuanza *market* hii kuipeleka nje sana tuanze kwenye hoteli za Zanzibar tuanze kupeleka waanze na wao kutumia hii masuala ya mwani kupikia, kutanganza ndani ya nchi yetu halafu tutowe na nje ya nchi yetu tuweze kuwasaidia hawa walima mwani wafanikiwe katika masuala yao.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nitaendelea kidogo kidogo hivyo hivyo kwenye masuala kuna *point* nyengine hapa, wajumbe wanahamu niongeee nakushukuruni sana endeleeni kupiga makofi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mhe. Waziri na *management* yake ambayo inajitahidi Zanzibar ambavyo kama nilivyozungumza siwezi kumlaumu kwasababu swali la biashara kuliinua Zanzibar sasa hivi ni sawa sawa kutoka kwenye kiza kwenda kwenye muangaza, lazima hivi vitu nilivyovitaja hivi vikamilike ndio watapata wepesi zaidi kwenye maswali ya biashara mimi Mhe. Mwenyekiti kusema la ukweli nina mambo mengi nahisi sasa nikizunguza mbiombio na muda wetu mdogo nitakuwa naharibu isipokuwza nitamtafuta Mhe. Waziri yale ambayo nahisi nataka nimshauri nitamshauri na mengine nitayajua kutoka kwake nitapata kuyajua nakushukru sana ripoti hii mimi naikubali asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid na atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali ameniomba dakika tano na mchangiaji wetu wa mwisho kabisa kwa siku ya leo atakuwa Mhe. Waziri Said Soud na baadaye tutampa nafasi Mhe. Waziri aje kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja walizotoa wajumbe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia lakini awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuajalia tukakutana jioni ya leo toka asubuhi mpaka sasa hivi muda mwingi wenzetu kutoka asubuhi mpaka sasa hivi wameshabadilishwa majina wameshaanza kuwa marehemu, wengine wameshatiwa kwenye makaburi.

Namuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema utujaalie katika nchi utuongezee imani na upendo tulionao na uwape hekima na busara viongozi wetu waweze kutuongeza na kulitumikia taifa hili kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wote, amina.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nataka nianze mchango wangu katika agizo namba 20 *page* ya 7 naomba kulinuu kidogo.

> "Kamati ilitoa maagizo kwamba Serikali iongeze bajeti ya wajasiri mali kwa kutoa mikopo ya kutosha kwani wajasiria mali wanachangia pato la taifa kwa kiwango kikubwa"

Wizara ikajibu kwamba kupitia Mfuko wa Wawezeshaji wa Taifa Serikali imekuwa ikitowa mikopo ya viwango mbali mbali kwa wajasiria mali kwa lengo la kukuza miradi yao lakini kujiongezea kipato na kuchangia katika pato la taifa.

Mfuko wa Uwezeshaji ulianza kwa kiasi cha fedha shilingi bilioni 1,573,000,000 lakini kupitia mfuko wa AK na JK mtaji wa mfuko huo uliongoezeka hadi kufikia shilingi bilioni 2,313,000,000 na hadi kufikia Disemba 31 mwaka 2015 jumla ya mikopo 727 yenye thamani ya shilini bilioni 1,251.6 milioni imeshatolewa kwa wajasiria mali mbali mbali, ni jambo la kufurahisha na ni habari nzuri iliyokuwa ya kutia moyo.

Lakini nilitaka kujua kidogo Mhe. Waziri huu mfuko wa kuwaendeleza hawa wajasiria mali mpaka leo bado unaendelea au haupo tena na kama upo mpaka sasa uimeshafikisha kiasi gani cha fedha za mtaji ambao upo kwenye mfuko huo, kwasababu tuliona kipindi hiki hadi kufikia Disemba una shilingi bilioni 2,300,000,000 na bila shaka wanaokupeshwa na wao wana wajibu wa kulipa ili wapate wengine wakopeshwe tena.

Sasa nilitaka kujua huu mfuko bado ungalipo na wajasiria mali wanaendela kukopeshwa kwa sababu leo asubuhi wakati nilipokuwa nikichangia nikiuliza swali nilipata jibu kwamba mradi wa kuendeleza wa kilimo cha matone cha umwagiliaji ni ghali ambacho wakulima wadogo wadogo hawawezi kukimudu, lakini kama mfuko huu wa wajasirilia mali upo kwa nini usitumike kwa kuwakosesha watu wakaendeleza hicho kilimo cha *green house* ambacho kinaonekana kina manufaaa makubwa kwa wakulima wetu hilo la kwanza. Na nasema hivi kwa sababu gani nasema hivi kwasababu ukitowa hesabu shilingi bilioni 2,313,000,000 ukitowa shilinigi bilioni 1,251.6 utakuta kuna shilingi bilioni 1,061,400,00 zimebaki kwa kipindi hicho, sasa kwanini

pesa zibaki wasikopeshwe wajasiria mali zipo kama zipo kwanini wasipewe wajasiria mali wakakopeshwa wakaweza kujiendeleza.

Kwa hiyo mimi natoa wito na naiomba Serikali ikiwa hizi pesa bado zingalipo ni wakati muwafaka wa kuwasaidia wajasiria mali wakawakopesha wakaweza wakaanzisha hicho kilimo cha *spice* kama kilivyotajwa kwa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa nikitoka hapo miye nakwenda zangu kwenye agizo namba 38 *page* ya 13 naomba kunukuu.

> "Kamati inataitaka Wizara kupitia Shirika lake la *ZSTC* kuweka mashine za kusafishia karafuu kisiwani Pemba ambapo uzalishaji mkubwa wa karafuu hufanyika jambo ambalo inapunguzia gharama ya kuondoa mzunguko usio wa lazima"

Nakubaliana na mimi mawazo ya kamati ni mawazo ya busara ambayo yanapunguza gharama lakini Shirika limekuja na jibu likasema Shirika limefikiria swali hili na mara tuu zitakapopatikana mashine nyengine katika bajeti zijazo zitanunua mashine nyengine tatu na kuziweka Pemba. Hata hivyo kwa mujibu wa taratibu za kusafirisha karafuu nje hata kama karafuu zitasafishwa kutoka huko Pemba kabla ya kusafirishwa lazima zikaguliwe kabla ya kupelekwa nje.

Sasa mimi najiuliza kitu kimoja Pemba na Unguja ni ile ile Maafisa wetu ni wale wale kwanini iwe ikitoka Pemba lazima ije amwage tena hapa ichekechwe tena, sasa pale Shirika halioni kwamba linajiingiza gharama zisizo na lazima kwani kama ni hivyo Shirika lisiwatoe wataaalamu hapa wale ambao kwamba wanaaminika hawa wanaweza, wana ujuzi, wana uwelewa wakufanya mambo ya *packing* wakawapeleka Pemba ambapo karafuu nyingi ziko kule wakazi-*pack* hata zikitoka kule zikawa ziko hapa kwa ajili ya kusafirishwa tuu kulikoni kuchukua gharama kwa mara ya pili wakazitoa karafuu Pemba zikaletwa Unguja zikaja zikasafishwa ikisha ndio zikapelekwa tena kusafirishwa.

Jee, huoni kwamba tunajiingiza gharama zisizo na mimi naiomba sana Wizara kupitia Shirika la *ZSTC* iangalie hili iliangalie sana na utekelezaji wake usichukuwe muda ikiwa ikikosekana kwenye msimu huu msimu ujao wazo hili liweze kutekelezwa, kufanya hivyo kutapunguza gharama, jee waangalie ni gharama ni shilingi ngapi zinaweza kutumika tunaweza kuzi-*save* kuziokoa kwa mambo kama haya.

Lakini pia niende katika agizo la 41 Shirika kupitia mikutano mbali mbali kwa wakulima na wadau wa karafuu uliofanyika mwezi wa Mei wakulima walileta malalamiko hayo ambapo maafisa kutoka Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na *ZSTC* walichukulia hilo na kulipeleka katika Taasisi zao na kuahidi kulifanyia kazi ili kasoro hizo ziweze kurekebishwa na kujua njia bora za kufuatwa ili wakulima wafaidike na miche iliyo bora, tumewasihi mara nyingi na tungekuwa tukiwashauri mara nyingi kuhusiana na suali la miche ya mikarafuu.

Mara nyingi mimi ninaposimama hapa huwa natawo mawazo juu ya miche ya mikarafuu nashukuru kamati imeliona jambo hili wameliona na wamelisikia na wakulima wenyewe

wametoa malalamiko yao ingawa ukweli hawajataka kukiri kwamba miche inayopandwa inayotolewa na Wizara ya kilimo bado inatatizo la kuwa mingi yao inakufa kama wakulima walivyozungumza, ushauri wangu kwa *ZSTC* na Shirika na Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo kuwatumia wakulima wenyewe ili wakulima hawa wanajua wapi wanaweza kuipata miche iliyo bora kwasababu miche ya mabotea bado imo mashambani waitumie wataipata kwa gharama nafuu kulikoni kuendelea kuitegemea Wizara ya Kilimo kwasababu miche ya Wizara ya Kilimo miye kama mkulima wa karafuu najua bado ina tatizo la kuweza kustahamili ukilinganisha na miche ambayo ni ya kung'oa yaani mabotea.

Mheshimiwa nakwenda katika agizo la 43 ukurusa wa 15 kamati iliitaka Shirika la *ZSTC* kuandaa mpango madhubuti wa kuendeleza kilimo cha viungo swali langu na swali hili limeshazungumzwa na watu wengi, wachangiaji wengi wamelizingumzia suala la kilimo cha viungo kwa kweli sipendi nirudie tena lakini asubuhi nilizungumza suala la vanilla nikazingumza suala la pilipili manga, suala la mdalasini na viungo vyengine, sasa jamani tufikeni wakati tukubali kwamba viungo vya Zanzibar kama alivyosema Mhe. Rashid Makame kama bidhaa zetu ni bora viungo vinavyotoka Zanzibar ni bora na ndio maana mpaka inaitwa *Spice Island* kwanini tusiwawezeshe wakulima wa viungo tukaweza kwa kuwapatia mitaji wakaweza kujiendeleza hawa wako wengi leo tumekuta vikundi 727 tuu ndio vilivyopewa na huku tunaambiwa pesa zilikuweko kwanini hizi pesa wasingepewa wakulima wakajiendeleza. *(Makofi)*

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika mchango huu mimi nitaunga mkono tuu pale nitakajua kwamba ni lini wakulima watawezeshwa kulima viungo, wakulima watawezeshwa lini kwasababu *ZSTC* wako na ni Shirika la Serikali na wale ni wananchi lini tutaweza kuwakopesha tukawaendeleza wakaweza kuongeza zao la karafuu, mikarafuu inahijika ipandwe mingi zaidi maeneo yako ya kupanda mikarafuu.

Ahsante sana Mheshimiwa naunga mkono kwa asilimia hamsini baadaye nitamalizia hamsini ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na atafuatia na Mhe. Said Soud.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja ukurasa wa 7. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeza sana kamati kwa kuliona wanasema kwamba hapa Serikali iongeze bajeti ya wajasiria mali kwa kutoa mikopo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niipongeze Wizara kwa jitihada wanazozichukua nao pia wa kusilikiliza wazo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku moja nilikuta *carry* imeandikwa "*Nikiwa mkubwa nitakuwa Fuso"*, maana yake nini kwamba ile *carry* ikijichuma itanunua hilo fuso hiyo ndio maana yake, ni

kwamba huyo mjasiria mali akiwezeshwa ndiye anayekuwa mkubwa kibiashara akawa mfanya biashara mkubwa ikiwa anachukua bidhaa kutoka nje kuleta hapa ndani ili Serikali kuweza kupata mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 8 tunasema kwamba kamati ilitaka kwamba Wizara kutokana na uzalishaji mkubwa wa bidhaa za kilimo nchini kuanzishwa na wakulima pamoja na wajasiria mali.

Mhe. Mwenyekiti, kwamba iandae viwanda Mhe. Mwenyekiti sisi kule Pemba huzaliwa embe mpaka kusema kwa ukweli watu wakawa hawana vya kulifanya ndio ikafika shilingi 500/=.

Mhe. Mwenyekiti, tukuanzisha viwanda hivi ikiwa kama hatusemi yaani tufanye kwa vitendo isiwe ni maneno tuu, basi tutafika mbali Mhe. Mwenyekiti viwanda hivi vidogo vidogo vya kuweza kusarifu haya maembe, kusindika na mambo mengine kwasababu ndio ajira yenyewe hizo vijana watapata ajira na nchi itapata mapato na tutaendele mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe sana wizara hilo walichukue kama ilivyoshauri kamati ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye nchi ya viwanda lakini isiwe ni kusema tu, itekelezwe kwa vitendo. Mhe. Mwenyekiti, ifikapo 2020 alau Zanzibar tuwe na viwanda vya kuweza kujakutumika na kule kwenye kampeni tuseme kwamba tumefanya moja, mbili, tatu, nne, tano mwenye macho haambiwi tizama ataona, na atakubali yale tunayomwambia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe sana wizara hapa walichukulie hili na walifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 12, kamati inaitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kufanya utafiti wa kina juu ya suala la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika sana kuona kwamba kuna wahujumu wa uchumi, maana mimi nasema wahujumi wa uchumi wanaotuchukulia karafuu zetu hizi kutoa karafuu huko wakatuingizia karafuu hapa, kwa sababu karafuu za Zanzibar ndio karafuu bora na zenye viwango duniani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, leo kama kutatoka watu huko watachukua karafuu tuseme Comoro na sehemu nyengine kutuletea hapa Zanzibar ili tu kutuharibia soko letu kusudi. Mhe. Mwenyekiti, mtu huyu akikamatwa na ushahidi kama huu ashitakiwe kwa sababu huyo ni muhujumu wa uchumi na asiweze kupewa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi kwa sababu hii kamati niseme la ukweli Mhe. Hamad Abdalla Rashid ni mjumbe hii kamati ina majembe, tena majembe ya kufanya kazi kweli kweli. Mimi naipongeza kamati hii na nawaomba sana wazidi kufanya bidii na waendelee zaidi ili kuhakikisha kwani kazi yao ni kuibua changamoto zilizoko kule na kuzifanyia kazi na sisi watuletee hapa ili tuweze kuwaunga mkono, tuweze kuisimamia serikali kuhakikisha kwamba haya waliyoomba yaweze kufanyiwa kazi na sisi tuko pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali, kabla sijamwita Mhe. Waziri Said Soud Said, Mhe. Makame Ali Ussi ameniomba dakika tano kwa hiyo naomba nimpe nafasi hii na mwisho kabisa nitampa Mhe. Waziri.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa maalum ya kuchangia mada hii, kwa sababu muda ni mfupi na sikuwepo tangu mwanzo nitajaribu sana kuchangia kwa kifupi sana na nitajikita kwenye viungo na nitaelezea karafuu tu sitaeleza viungo vyengine, kwa sababu mambo ya *processing* kwa viungo vyote yanafana. Isipokuwa *by product* ndio zitakuwa tofauti.

Kwanza nianze kwa kukushukuru Mhe. Mwenyekiti kunipa hiyo fursa na pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa ripoti yake hii ya kina inayoeleza kwa urefu mambo mengi sana, nashauri tu kitu kidogo sana mara nyengine ni vizuri najua *statistics* zimo humu zimeelezwa. Lakini wazidishe *statistics* kwa sababu ukiweka *statistics* ndio tunaanza kujipima jinsi tunavyoendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote tukitaka kupata faida kubwa kwenye zao hasa kama la karafuu lazima tufanye zile *value addition* yaani tupate mazao tofauti au *product* tofauti kutoka zao hilo. Hivi sasa tuna kiwanda chetu cha makonyo kilichopo Machomane kule Pemba, kiwanda hiki kwa kweli kinahitaji kuboreshwa zaidi kwa sababu pale tulikwenda kama miezi miwili iliyopita au mwezi mmoja na nusu uliopita kiwanda kile kimekuwa kero kwa sababu ya moshi mzito sana unasambaa pale kwenye eneo lile. Kwa hiyo, nashauri sana bidii ifanywe ule moshi upungue, halafu pia kiwanda hiki kifanyiwe uboreshaji kiweze kuzalisha mafuta kwa wingi, zaidi ya hapo nashauri pia kuwe na viwanda vyengine vinavyoweza kutengeneza *by product* nyengine za karafuu kama mafuta mazuri, madawa ya aina mbali mbali pamoja na madawa yale ya *massage* ya kujichulia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea anasema zao la karafuu linahitaji baada ya kuvunwa na linataka kwenda kusafirishwa nje, lazima liwe safi sana. Maana likipata mavumbi kidogo tu wakati wa kuzifanyia uchunguzi linaweza likapunguza thamani au linaweza kupunguza ubora wa zao hilo. Kwa hiyo, nashauri sana vipatikane vifaa maalum, vifaa hivyo duniani vipo vya kusafishia karafuu ili ziende nje kwa usafi ili ipatikane ile *core quality* ya karafuu zetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mikarafuu yetu ina matatizo ya uzalishaji kutokana na uzee. Siku hizi kuna usafi na usafi ulikuwa unarudisha pia uzalishaji, lakini siku hizi mikarafuu mengi iko safi kwa hiyo tatizo hilo kidogo limepungua. Sasa kuna tatizo la umri wa mikarafuu kuwa mikubwa sana, kuna mikarafuu mengine ina umri wa miaka zaidi ya mia. Sasa mikarafuu inapokuwa na umri mkubwa hata uzazi wake unapungua huanza kwa kukauka majani. Sasa zamani tulikuwa na watibabu wa mikarafuu wanatibu *diabetes* na *satan death* maradhi hayo ya mikarafuu. Wakawa wanakata matawi makavu wanatia dawa na karafuu zikaaza kidogo kuja juu. Sasa nashauri wale watibabu wa mikarafuu tunao na bado wapo wengine wameshakuwa wazee lakini bado wapo wanaweza kufundisha vijana wakaweza kuwa watibabu wazuri. Kwa hiyo, turudieni utibabu wa mikarafuu huku tukipanda mikarafuu mipya na huku tutibu mikarafuu yetu ili haya maradhi yasiathiri zao letu hili la mikarafuu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulieleza ni hili linalohusu mambo ya kukatwa. Ni kwamba mikarafuu inakatwa hilo ni tatizo wavunaji wakati mwengine wanaikata na ukikata tawi unaweza ukasababisha maradhi pale ulipopakata ukapasababisha maradhi mkarafuu ule ukapata misukosuko pia. Kwa hiyo, nashauri wale watu wa *extension* ya mikarafuu wafanye kazi za

kupitia wakati wa kuvuna ili kuhakikisha mikarafuu hii haikatwi ili tuweze kupata mazao mengi ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa sababu umenipa muda wa dakika tatu na dakika tatu hizo nadhani zimekwisha, naomba nirudie kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa juhudi kubwa anazochukua kuliendeleza hili zao la karafuu na mazao mengine ya biashara ambayo yatatusaidia sana kwenye uchumi wetu wa Tanzania. Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango, sasa mchangiaji wetu wa mwisho kabla sijamwita Mhe. Waziri naomba nimwite Mhe. Waziri Said Soud Said.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nafasi ambayo nitaichukua kwanza kwa kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za kuimarisha maisha ya Wazanzibari ili yawe bora. Vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia vyema jitihada za serikali ili kufanikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, pia natoa shukurani kwa Wajumbe wote wa Kamati za Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi yao vizuri na kuleta ripoti hii hapa na kuisaidia serikali ili kuweza kuona makosa na yale ambayo yamefanyika. Kamati hizi ndio sabuni ya serikali, kwa hiyo sisi tunapongeza sana Kamati za Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi zao vizuri na tunaahidi kama serikali yale mapungufu yote tutayafanyia kazi ili kuifanya serikali ifikishe malengo yake kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ningetaka pia nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya Biashara kwa kusimamia vyema biashara katika visiwa vya Unguja na Pemba, kwa kusimamia vyema biashara kati ya Tanzania Bara na visiwani, kati ya Zanzibar na Afrika Mashariki na Kati, kati ya Zanzibar na nchi nyingi za dunia ambazo zinafanya biashara na nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii imefanikiwa sana sana katika mazingira ya kuwaonesha wananchi wa Zanzibar njia hasa pale ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipoanzisha Baraza la Biashara. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Biashara ni mkombozi wa Wazanzibari pindi Wazanzibari wakilitumia vizuri Baraza hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba nawaambie wajumbe pia kwamba wenzetu Tanzania Bara baadhi yao wanasafirisha mpaka muhogo mbichi kupeleka Marekani, Ujerumani, Japan si chini ya tani sitini elfu wana-*export* muhogo mbichi. Sasa basi, ni kazi yetu sisi wawakilishi kuwaelimisha wananchi Baraza hili jinsi gani linaweza kufanya kazi ya kutoa vitu katika nchi na kuingiza pesa za kigeni. Tuna matunda aina mbali mbali katika nchi yetu, tuna embe, tuna mananasi, tuna ndimu ambazo hizi tunaweza tuka-*export* na ku-*export* kwetu tuta-*export* kwa madhumuni ya kutafuta masoko ya uhakika. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi kama wawakilishi kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wananchi namna ya kujinasua katika Baraza hili la Biashara. Hili sio Baraza la Biashara la kukaa watu wakafikiria tu kwamba labda Kiwanda

cha Makonyo, labda Kiwanda cha Samaki hapana, hili ni Baraza la Biashara la kumnasua Mzanzibari kutoka alipo na kumsogeza kwengine.

Kwa vile sasa wale wafanyabiashara waliokuwa wana uwezo mkubwa iko haja kuanzisha ku-*export* mali hizo ili kuifanya nchi hii ipate *foreign*. Na wale ambao bado hawajakuwa na uwezo kujiunganisha vikundi mbali mbali na kuweza kufanya utaratibu wa ku-*export* hata muhogo mbichi kuupeleka Ulaya. Ndege zetu zinakuja nyingi mno hapa yanakuja madege hayana bidhaa za kuchukua, sasa watu wakiweza kuji-*organize* wakatafuta ma-*agent* katika nchi za Ulaya, mimi nahakikisha kwamba Zanzibar inaweza kupiga hatua. Na ule utaratibu wa kukaa watu barazani wakazungumza kesho, kesho kutwa, mwezi ujao nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti haya yataondoka kama watalitumia Baraza la Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, sasa yote haya yamekuja kutokana na utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ilani ya Chama cha Mapinduzi bado nataka kusema tena kwamba kama tutakuwa tunaifuata basi umasikini katika nchi hii utapotea. Kwa sababu hakuna mtu atakaa barazani angojee kudanganywa asubuhi, kesho, Jumapili, Jumatatu, mwezi ujao eeh watu hawana kazi nchi hii sasa. Lakini hebu tutumie hili Baraza la Biashara, wawakilishi sisi ni kiungo na wananchi wan chi hii. Kwa hiyo, tutumie nafasi yetu kuwaelimisha wananchi kutumia Baraza la Biashara ili kuweza kujinasua na hali mbaya ya kimaisha kwa kutumia uwezo wetu wa kusafirisha matunda kupeleka nje na hatimae kuweza kupata pesa za kigeni kwa kunasua maisha yetu.

Mhe. Mwenyekiti, bado nataka niseme tena kwamba dhamira ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ni kumkomboa Mzanzibari na jitihada hiyo inaendelezwa na serikali iliyoko madarakani hivi sasa chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Sasa ni wajibu wetu wawakilishi kutumia fursa hii kuitangaza Zanzibar kibiashara, Baraza la Biashara ni vyema mwaka ujao tukalizungumza kwamba limeweza kuruhusu Wazanzibari kadhaa ambao wamekuwa tayari wana leseni za ku-*export* matunda kutoka nchini na kupeleka nchi za nje. Jambo linawezekana wenzetu Kenya wanasafirisha mpaka chungwa, na nataka niwaambie ile chungwa inapigwa sopu sopu ile inaingizwa kwenye tissue halafu inaingizwa kwenye sanduku inapelekwa Ulaya. Sasa sisi hapa tumekaa tu tunangojea kesho, kesho kutwa, mwezi ujao, mwaka ujao hakuna kitu bwana, hakuna kitu hapa, hapa mpaka 2020. Sasa acheni hiyo fanyeni kazi ya kuzalisha na kutafuta mbinu za kuiboresha Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri Said Soud Said kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili atoe ufafanuzi baadhi ya hoja zilizotolewa na wajumbe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wote ambao wamechangia katika taarifa yetu hii ya maagizo ya Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo wote kwa ujumla wao ni wajumbe 12. Wajumbe 10 wamejieleza na wajumbe 2 wamechangia kwa maandishi. Waliochangia kwa maandishi ni.

1. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) na
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Waliochangia binafsi ni.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Hidaya Ali Makame
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Simai Mohammed Said
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
6. Mhe. Omar Seif Abeid
7. Mhe. Suleiman Makame Ali
8. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
9. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kwamba michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni mizuri na muhimu na imetupa sisi uwezo mwengine zaidi wa kuweza kutafakari kwa kina zaidi masuala ambayo yanatuhusu yaani yakiwemo Wizara ya Biashara ya kuendeleza viwanda na sekta zote ambazo zinahusiana na mambo haya mawili.

Mhe. Mwenyekiti, mengi ambayo yaliyozungumzwa na wajumbe katika michango yao, yamezungumzwa pia katika wakati wa bajeti, na wizara yangu imeyapokea kwa kina kabisa na inayafanyia kazi. Kuna yale ambayo tumeshayafanyia kazi kwa mujibu wa taarifa tulizoleta na kuna yale ambayo tunayafanyia kazi hatujayaletea taarifa lakini yamo katika process ya kuyafanyia kazi. Naomba niseme kwamba wizara yangu iko makini na naomba niseme wazi kabisa nimshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa sababu wizara yangu imepata mabadiliko kati kati, nasema kwa siku hizi nimepata watendaji majembe, sasa hivi tuna watendaji watatu katika level ya Makatibu Wakuu na Wakurugenzi safi kabisa. Kwa kweli nina imani kubwa sana kwamba wizara yetu kipindi hiki kilichobakia tutafanya kazi nzuri zaidi na wenyewe mtaona vitu tunavyofanya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais kama ninavyopenda kusema siku zote ni kiongozi ambaye anaunga mkono moja kwa moja Zanzibar iwe nchi ya viwanda. Na mimi napenda kusema kwamba yeye ni *champion* ingawa si neno zuri linalotumika hapa Zanzibar lakini kimataifa unapokuwa champion ina maana kwamba wewe ndio kiongozi wa mbele na wengine wote wanakufata. Namshukuru sana Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika michango yetu nitajaribu kwa ufupi kwa sababu kama nilivyosema mengi ambayo yamezungumza tumeshayazungumza na tunayafanyia kazi. Nizungumze kwa ufupi kabisa sekta ya biashara, sekta hii wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu sekta ya biashara. Ningependa niseme tu sisi kama watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tunaangalia sekta ya biashara tulikotoka, sekta ya biashara tulipo sasa hivi lakini pia sekta ya biashara tunakotarajia kwenda. Tukisema tulipotoka mnajua historia ya biashara sitaki kusema sana kwa sababu wote mnaelewa. Huko nyuma kabla ya Mapinduzi mpaka baada ya Mapinduzi, serikali ilikuwa inadhibiti uchumi wakati ule, biashara zilikuwa chini ya mikono ya serikali. Tumetoka huko tukaingia katika uchumi ambapo wafanyabiashara wote wanaendeshwa na soko ndipo tulipo sasa hivi.

Kikubwa ambacho nataka niseme kwamba biashara haiwezi kwenda bila ya kuwa na vyombo vya kuendesha biashara na vile vile kuwaangalia wafanyabiashara. Sasa hivi tulipo Mheshimiwa ni kwamba vyombo vikuu vya kusimamia biashara na kuendesha biashara, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaviweka ndani ya mikono ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa hiyo, sisi tulio ndani ya Wizara ya Biashara hatuna wasiwasi kabisa kama huu ni mpito tuliokuwanao matatizo ya wafanyabiashara wetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyazungumza tumo katika mpito, lakini nina hakika kabla ya miaka ya kumalizia MKUZA huu na kuingia MKUZA mwengine tutaweza kuwa katika mahali pazuri. Kwa sababu suala zima la leseni limezungumzwa katika ripoti yetu, tumeeleza kwamba leseni serikali imeunda Baraza la kuangalia leseni za biashara zote na Baraza hili limeshaanza kutoa vigezo kwa ajili ya kurahisisha utaratibu wa kufanya biashara, utaratibu wa kuweza kupata leseni ambayo itakuwa ni rahisi haina usumbufu na itawalenga wale wadogo wadogo ili waweze kufanya biashara zao kwa ufanisi.

Pia jengine ambalo muhimu katika biashara ni usajili wa biashara. Hapa linakuja suala la kwamba usajili wa viwanda, usajili wa biashara, usajili wa mahoteli na makampuni na kadhalika, nalo hilo serikali imeliamulia tumekabidhiwa Wizara ya Biashara *register* au Mamlaka ya Kusajili Biashara na Makampuni ambayo nayo keshokutwa tutaanza ku-*launch* utaratibu mzima kabisa wa kusajili makampuni, utaratibu mpya, rahisi, utakaowawezesha wananchi wetu wafaidike bila ya usumbufu. Pia nayo inasaidia katika kuuza biashara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine suala zima la kuwafanya wafanyabiashara na serikali kukaa pamoja, wakiwa wanazungumzia mambo ambayo yanawasumbua ndio maana Baraza la Biashara juzi tu limepitisha sheria ya kuanzisha mfumo mpya wa Baraza la Biashara ambao utatuwezesha kukaa mpaka mikoani kuzungumzia njia gani bora ya kuendesha biashara.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia hiyo haikutosha, tumekabidhiwa kitengo cha biashara halali na kumlinda mlaji. Kitengo hiki hivi karibuni kiko mbioni kuanzishwa masuala mengine ambayo yanahusu biashara, ubora wa bidhaa zetu, utaratibu mzima wa kufanya biashara bila ya kuoneana, uwazi wa biashara, kulinda biashara na kadhalika haya yote yatasimamiwa. *(Makofi)*

Jengine ambalo nataka niliseme kwa ufupi kuhusu suala la maonesho. Maonesho ni sehemu ya biashara bila ya kujitangaza huwezi kuwa na biashara. Yote ambayo yamesemwa na Wajumbe tumeyapokea na tunayafanyia kazi pamoja na changamoto zao. Kwa sababu maonesho lazima uwe na uwezo wa kuweza kupeleka bidhaa zile zinakohusika, lakini matatizo ya wafanyabiashara wa Zanzibar hasa wale ambao wajasiriamali hawana uwezo wa kukidhi soko. Kwa hiyo, tunatakiwa tuhakikishe kwa upande wa pili bidhaa zetu zinazalishwa kwa wingi na ziwe za uhakika, za ubora unaokubaliwa na usafi unaokubaliwa ili ukitakiwa upeleke *order* mahali basi uweze kupeleka *order* kwa wakati unaotakiwa, kwa kiwango kinachotakiwa na kwa ubora unaotakiwa. Jambo hili ndio ambalo linatushinda sasa hivi na kama nilivyosema huko tunakotaka kwenda tunataka kuwa na wafanyabiashara ambao watakuwa na uwezo huo wa kuweza kukamilisha na kutimiza matakwa ya wanunuzi wao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa ufupi nije katika suala zima la viwanda. Mhe. Mwenyekiti, viwanda ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi, nchi ambayo haina viwanda haiwezi kwenda mbele. Lakini pia Mheshimiwa suala la viwanda sio la serikali peke yake, suala la

uendelezaji wa viwanda inatakiwa iwe jamii nzima kuanzia chini mpaka juu wawe wanazungumza suala zima la uendeshaji na ukuzaji wa viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, lazima kuwe na mpango wa kitaifa wa kuendeleza viwanda. Sisi Wizara ya Biashara kama tulivyosema katika agizo la kamati, tumesema tunapitia sera ya viwanda, lakini kupitia sera ya viwanda peke yake haitoshi lazima tuwe na mpango wa kitaifa wa kuendeleza viwanda ambao mpango huo utaeleza jinsi ya kuvilinda viwanda vya ndani lakini pia na kuvilea viwanda hivyo na kuweza kuwaalika au kukaribisha viwanda vya nje.

Mhe. Mwenyekiti, unapozungumzia viwanda huwezi kuitoa sekta binafsi, huwezi kuitoa sekta ya umma, lakini pia huwezi kutoa mchango wa taifa letu. Lakini pia unapozungumza viwanda Mheshimiwa lazima kuwe na misingi muhimu ambayo inatakiwa tuizingatie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi lazima nikiri katika kipindi tulichokaa kifupi na wataalamu wetu tumeangalia njia bora ya kuweza kwenda katika utaratibu mzima wa kuendeleza viwanda hapa Zanzibar. Njia bora hiyo ningependa nim-*quote* huyu Rais Xi Jinping wa China. Rais Xi Jinping alisema hivi: "Lazima kunako viwanda *think big*, fikiria vitu vikubwa", lakini akasema "*start small*", yaani uanze kidogo kidogo kwa vitu vidogo vidogo kwa vile ambavyo unavyo uwezo navyo na vimo katika himaya yako. Lakini pia akasema "nenda kwa kasi", ndio maana Mhe. Mwenyekiti, tukazungumzia masuala ya *spices*, tukazungumzia masuala ya samaki (uvuvi), tunazungumzia masuala ya viwanda vya kilimo, hivi ndivyo ambavyo tunavyo tunamiliki navyo ndani ya mikono yetu, lakini tuna mawazo makubwa sana ya upeo mkubwa na tunaamua kwenda kwa mbio za kasi kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndio dhana ambayo tunakuja nayo kwa ajili ya kuendeesha na kuendeleza viwanda katika Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la viwanda tulivyonavyo sasa hivi kwa mfano, tumezungumza Kiwanda cha Mahonda. Mhe. Mwenyekiti, ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi wakapata muda na niko tayari kuwafanyia utaratibu waende wakaangalie Mahonda tunayoizungumza Mahonda sio ile ya zamani. Hii Mahonda mpya, ina kazi mpya, ina mashine za kisasa na inatoa bidhaa safi na za kisasa. Bidhaa ya sukari ya Mahonda haiwezi kulinganishwa na sukari ya kokote hapa katika *East Africa*. Lakini bado Mahonda ina changamoto na hizo ambazo wamezizungumza wenyewe na tutazifanyia kazi na tuko pazuri, tuna imani kubwa mwaka 2020 au tukitoka 2020 basi 2023 Kiwanda cha Mahonda kitakuwa kinafanya faida kubwa sana na kitaweza kuwagusa wananchi wengi walioko Zanzibar. Mimi najionea fahari kubwa sana kwamba sasa hivi tunao wawekezaji ambao tukiwaelekeza vizuri tutaweza kuwa na kiwanda cha mfano hapa Zanzibar.

Pia hiyo haitoshi, Pemba kuna uwezekano wa kuwa na viwanda vya sukari wanaita, *mini super plan*, vidogo vidogo kwa kuwezesha kuwa na sukari maalum. Sukari mnayoiona hapa hii kuna sukari aina nyingi, kuna sukari ya *brown*, sukari nyeupe, sukari ya viwandani, kuna aina mbali mbali za sukari. Kwa hivyo, tukiwa tuna-*specialize* yaani kuwa na mikakati maalum tukaweka viwanda kule Pemba na hili tunalifanyia kazi tutaweza kufanya mambo ya msingi kwa nchi yetu.

Suala la mwani. Naomba niseme moja kwa moja viwanda navitaja moja kwa moja kwa sababu mwani kwa mfano, mwani unaajiri zaidi ya wananchi wetu 26,000 au zaidi na wote hawa wengi wao ni wanawake. Suala la mwani kwa kweli tusikubali kuwa na maamuzi rahisi, kwa sababu mimi napenda kusema mara kwa mara unapokuwa unataka maamuzi rahisi yana gharama zake, lakini bora tuwe na maamuzi ya uhakika na sahihi ambayo yatatupa thamani kubwa zaidi kwa maendeleo yetu. Tatizo la mwani kwamba soko la mwani limeinamiwa na wazalishaji wakubwa wa mwani wakiwemo Philippines.

Vile vile soko la mwani limekamatwa na wanunuzi wadogo kidogo ambao hao ndio wanaoweka bei, lakini serikali zimesema humu katika jawabu letu kwamba, kuna kamati zina kazi kubwa tumezifanya. Naomba nikuhakikishieni ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba suala la mwani linafanyiwa kazi. Umoja wa Mataifa mashirika yao yote wameamua kwa kauli moja kwamba *sector* ambayo naisimamia kipindi hiki itakuwa ni sekta ya zao la mwani, wakiwemo *IFU, UNIDO, UNDP* na wote hao Shirika la Kilimo. Kwa hiyo, ningeomba nihakikishe tu kwamba, suala la mwani tutalifanyia kazi na tutaweza kufika mahali pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba nijibu kuhusu ujasiriamali. Ujasiriamali ni kitu muhimu sana, lakini ningeomba kidogo niseme ujasiriamali huwezi kulinganisha wanatofautiana, ujasiriamali wa kilimo na wajasiriamali wa kiwanda na wa sekta nyengine wanatofautiana, hata kunako hoteli Mheshimiwa ukiangalia wale wa *guest house* ni wajasiriamali kwa sababu wale wadogo. Kwa hiyo, wanatakiwa kuwa na sera maalumu ya kuwasaidia na kuwavusha na ndio maana sisi kama Wizara ya Biashara tumebadilisha sera ya wajasiriamali, vile vile tunaanzisha shirika ama *agency* ya kuweza kusimamia biashara wafanye viwanda vidogo vidogo na kadhalika.

Sasa wajasiriamali ni kweli bajeti yao inatakiwa iongezwe. Mfuko huu wa Uwezeshaji umewasaidia sana wajasiriamali, lakini pia kwa sasa hivi kwa kushirikiana na wizara tatu, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko tumeshakaa na vyombo mbali mbali vya fedha kuona kwa kiasi gani tutaweza kuwasaidia wajasiriamali. Kwa sababu siri kubwa ya maendeleo ya viwanda vya Zanzibar kwamba sehemu kubwa asilimia 95 ya viwanda vya Zanzibar ni wajasiriamali. Lakini kama nilivyosema pale mwanzo wanatakiwa hawa walindwe na walelewe.

Mimi ninao mfano, kwa sababu hakuna nchi hata moja iliyoendelea kiviwanda ambayo haikuweza kulinda na kuvilea viwanda vyake. Huyu Rais wa Marekani Abraham Lincoln alisema hivi: "Unapokuwa na viwanda mkawa mnaagiza bidhaa kutoka nje viwanda vyenu hamvishughulikii, mnachofanya kitu cha kwanza nyinyi mnapata bidhaa, nyinyi kule mnawapa watu fedha zenu", lakini tukiwa na viwanda ndani ya nchi tunakuwa na bidhaa zetu na tunakuwa na fedha zetu tutazifanyia mambo mengine. Kwa hiyo, ujasiriamali ni muhimu sana na mimi nakubaliana na michango ya wajumbe kwamba wapewe fedha kwa ajili ya kufanya kazi zao, lakini pia wapewe elimu kwa ajili ya kuendesha biashara zao na elimu kwa ajili ya kuendesha viwanda vyao kwa kuwa na ubora unaotakiwa na kuweza kuwa na *package* inayotakiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia suala la *packaging* kwamba *packaging* nayo ni muhimu. Kwa hiyo, yote haya mafunzo yote haya na vile vile kuwa na wabia wa kuwaendeleza

lakini pia kuwa na eneo la kufanyia biashara, yote haya ni muhimu. Kwa hivyo, tumeyapokea kwa roho kunjufu.

Jengine lililozungumzwa katika suala hili ni uwekezaji katika suala la mbogamboga na matunda ikiwemo tungule na matunda mengine. Katika mkakati wa viwanda wa Zanzibar sekta hii ya mbogamboga na matunda imepewa kipaumbele, mazungumzo tunafanya sasa hivi na baadhi ya wawekezaji kama wataweza, tayari wajasiriamali wameshaanza kutengeneza vitu kutumia tungule. Kwa mfano, sasa hivi *tomato*, sasa hivi kuna machupa makubwa ya kutengeneza *tomato paste* na kadhalika, jambo tunalotakiwa tulifanye sasa hivi ni kuvinyanyua viwanda hivi vifikie viwe katika viwango vikubwa zaidi na kuweza kuwafikia wananchi walioko ndani na vile vile wa nje.

Jengine Mheshimiwa kuhusu uwekezaji kwa jumla na kuhimiza sera hii ya *One Stop Center*, yaliyozungumzwa hapa ni ya msingi na serikali kupitia wizara kwetu na wizara zinazohusika kama Wizara ya Fedha kwa hiyo tutazifanyia kazi kupitia kuangalia mfumo mzima wa uwekezaji, vile vile kuangalia yale manufaa tunayowapa wawekezaji wa nje na kuwalinganisha na wawekezaji wa ndani. Hayo yote Mhe. Mwenyekiti, tunayafanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inaingia katika kuwa nchi ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la *ZBS*. *ZBS* suala la maabara na tumelijibu vizuri sana katika ripoti yetu, kuna masuala ya nyongeza nayo kuhusu maabara ya Pemba ni maabara ya aina gani. Kwa kweli maabara ya Pemba yatakuwa yanaangalia zaidi bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali na bidhaa zinazoingizwa nchini, kama mfano chakula na sabuni. Wataalamu watakaohitajika katika sekta hii zaidi ni katika watu wa sayansi, watu wa vyakula na mambo ya kemia na vile vile vimelea (*microbiology*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano *ZBS* lilizungumzwa suala la bidhaa zinazoingia Zanzibar kwamba ziwe zina viwango vizuri vya uhakika, hiyo ndio kazi ambayo wanafanya wenzetu hawa wa *ZBS* kwa kushirikiana na *TBS* iliyoko Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine lililozungumzwa ni kuhusu usajili wa makampuni Zanzibar na kwamba suala hili ni muhimu. Ni kweli ni muhimu kwa sababu niunganishe na tatizo moja liliopo la biashara, lakini yote haya kama tulivyosema katika ripoti yetu tunayapeleka katika ngazi husika na tutayazungumza na natarajia mimi tutakuwa na uwezo wa kupata ufumbuzi wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa *ZSTC*. Ningependa niunganishe suala zima la karafuu, mafuta ya karafuu, mafuta ya makonyo na kiwanda chake na mazao mengine ya ziada ya mafuta na *spices*. Kwa upande wa *spices* wengi wajumbe walizungumzia suala la *spices*, pale mwanzo niliposema kwamba moja ya jambo ambalo tulitizame la kuanza kidogo kidogo ni kuangalia zao hili la viungo. Zao la viungo tutizameni Waheshimiwa katika Afrika nzima ni Zanzibar, Madagascar na Comoro; lakini nchi mbili hizi hazitufikii sisi katika uzalishaji wa mazao haya ya *spices*, matatizo yaliopo wananchi hatulimi mazao haya, lakini pia kunahitajika kuwa na utaalamu wa kulima mazao haya kwa kisasa, lakini pia tuangalie unapolima *spices* lazima kuwe na uwezo wa kuweza kutengeneza mazao mengine yanayotokana na viungo, huwezi kusafirisha

pilipili manga kama ilivyo, pilipili manga lakini iwe katika *spices* zile za kupika au iwe katika *powder* ya kuweza kuchanganyishia katika vyakula vya nyama, samaki na kadhalika.

Kwa hiyo, hapa kazi tuliyokuwa nayo sio tu kuongeza thamani ya vitu vyetu vya viungo, lakini pia nitie tena vile vile hima kwamba Wiara ya Kilimo na sisi tunashirikiana vizuri zaidi, lakini na mikoa sasa hivi tumepeleka madaraka mikoani na mawilayani, tutakaa na viongozi wa mikoa na wilaya kuzungumza kiasi gani tutaweza kuongeza mazao haya ya *spices*. Kwa kweli hali ya mazao haya bado iko chini hairidhishi na kuna mifano kama aliyotoa Mhe. Hidaya Ali Makame. Kaskazini walikuwa wakitoa *spices* nyingi, tangawizi ilitokea Kaskazini, Hiliki ilitokea Kaskazini, Manjano Kaskazini, Pilipili Manga Kaskazini, hatuzioni hakuna. *(Makofi)*

Napenda kutoa mifano hiyo kwa sababu soko lipo lakini mazao haya hakuna ya kutosha. Kwa hiyo, lazima tukae na uongozi wa mikoa na wilaya kuona kwamba mazao haya tunayapa kipaumbele na kazi hiyo Waheshimiwa Wawakilishi tutaianza kipindi hiki mara moja kuona katika mwaka huu 2017 kuona tunaongeza mazao haya na kuweza kuwa na viwanda vya kutengeneza hata kama viwanda vidogo vidogo lakini uwezo huo tuwe nao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu miche ya karafuu nimekubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na waheshimiwa kwamba ipo haja. Ni kweli miche ambayo inatoka sasa hivi haikai miezi 18, ulimaji wake haitayarishwi vizuri, mche wa mkarafuu unatakiwa uubembeleze kama mtoto, uutie mbolea, uufunike kwenye kivuli na kadhalika. Hivyo vitu havifanywi matokeo yake miche hii inakuwa haina nguvu haiwezi kukua.

Tatizo jengine la miche ya mikarafuu serikali inatoa miche ya karafuu bure na hawa watu binafsi wanauza, lazima tukae tutengeneze utaratibu wa kuweza kuona kwa kiasi gani tutaweza kuangalia, tutoe pesa kwa ajili ya kuwashajihisha watu binafsi wawe na miche mingi lakini pia na serikali iendelee kutoa miche hii bure kwa kuwashajihisha wakulima.

Mhe Mwenyekiti, jengine kuhusu karafuu za Bara. Kweli karafuu za Bara zilikutwa Zanzibar mara moja tu mpaka sasa hivi hatujasikia tena habari kama karafuu za Bara zimeingia. Tafauti ya karafuu ya Bara na ya Zanzibar iko tofauti Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu karafuu ya Zanzibar ni nene na ni ndefu halafu inanukia na ni kali zaidi kushinda karafuu ya Bara na karafuu ya Bara ni nyembamba, lakini ukiangalia mafuta yaliomo ndani ya karafuu hizi mbili, karafuu ya Zanzibar mafuta yake ni mengi zaidi na huo utafiti umefanywa na Mkemia Mkuu. Kwa hiyo, kama ukichanganisha karafuu mbili hizi utashusha thamani na ubora wa karafuu za Zanzibar ndio maana tukakubaliana kwamba karafuu hizi zisiingie Zanzibar tuendelee na kuhakikisha kwamba karafuu za Zanzibar zina ubora unaotakiwa. Mpaka sasa hivi karafuu nilivyosema msimu huu hatujapata taarifa kwamba karafuu za Bara zimeingia.

Mwisho Mheshimiwa Kiwanda cha Makonyo. Kiwanda cha Makonyo cha zamani nadhani kimejengwa katika miaka ya 1970 mpaka 1980, hata hao waliotengeneza kiwanda kile kiwanda kimefungwa huko Ufaransa, Kiwanda kile cha Wafaransa lakini hakipo. Kwa hiyo, *spare* zake vile vile itabidi tununue India, hivyo hata udhalishaji wa mafuta ya makonyo unakuwa vile vile sio wa kawaida. Tatizo la moshi ni kwa sababu tuliambiwa tuongeze kile kinu cha juu kinachotoa moshi, lakini tumeongeza isipokuwa bado hauridhishi. Kwa hiyo, taarifa ambayo naomba niwajuilishe wajumbe serikali imekubali kwamba tujenge kiwanda kipya cha makonyo

ili kishughulikie sio tu makonyo, lakini kiwe makonyo na bidhaa nyengine ambazo ni muhimu kama mafuta ya mlangilangi, mafuta mengine ambayo tunazalisha yatoke pale na utaratibu wa kisasa haitumii utaratibu wa kuchemsha, utaratibu wa mashine za kisasa wanatumia madawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kusema haya niseme tu, tuko pazuri na kwa ushauri wanaotupa waheshimiwa tutaendelea kuwa pazuri na tutafanya kazi nzuri zaidi naomba watuunge mkono na wakati wowote kama kuna jambo la kutaka kutuelekeza tunawakaribisha Wizara ya Biashara tuko tayari kukupokeeni kwa mikono mirefu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakushukuru lakini naona hujatoa hoja kwa hiyo nakuomba utoe hoja hapo hapo ulipo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Nimetoa.

Mhe. Mwenyekiti: Umetoa, sawa nashukuru ahsante sana, maana naona makofi yalikuwa mengi. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana waliochangia lakini pia nimshukuru sana Mhe. Waziri.

Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji, naona hoja imepokelewa na imeshinda, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe kwa wale wote waliochangia na pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri na ninatumai Waheshimiwa wote wamekusikiliza kwa makini na tunakutakia kila la kheri katika ufanisi wa kazi zako.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kika mnatakiwa Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi baada ya kumaliza tu Baraza hapa mbakie kuna mambo muhimu yanataka kuzungumzwa. Kwa hiyo, nawashukuru sana kimeakhirishwa mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Kikao kiliakhirishwa mpaka
tarehe 05/10/2017 saa 3:00 asubuhi)